

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Kwanza – Tarehe 4 Septemba, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

WIMBO WA TAIFA

(Hapa Wimbo wa Taifa Ulimbwa)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

*(Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge
wa Upinzani hawakuwepo ukumbini)*

SPIKA: Hawa rafiki zangu wako wapi? Ahsante sana.
Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI-KATIBU WA BUNGE:

KIAPO CHA UAMINIFU

Mbunge afuataye aliapa Kiapo cha Uaminifu:

Mhe. Eng. Christopher Kajoro Chiza

SPIKA: Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI-KATIBU WA BUNGE:

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, baada ya kumaliza Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge letu, tulipata msiba wa kuondokewa na Mbunge mwenzetu, Marehemu Stephen Hillary Ngonyani aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Korogwe Vijijini ambaye alifariki tarehe 2 Julai, 2018 katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili alikokuwa anapata matibabu. Mazishi ya Marehemu Ngonyani yalifanyika Kijijini kwao Kwamndolwa tarehe 5 Julai, 2018.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na taarifa hiyo na kwa kuwa leo ndiyo kikao chetu cha kwanza tangu msiba huo utokee, naomba tusimame kwa dakika moja kwa ajili ya kumkumbuka Marehemu Stephen Hillary Ngonyani.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walisimama kwa dakika
moja kama ishara ya kumkumbuka Marehemu Mhe.
Stephen Hillary Ngonyani)*

SPIKA: Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi, amina. Naomba mkae.

Waheshimiwa Wabunge, pia katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge, Bunge lilitisha Miswada miwili ya Sheria ya Serikali. Muswdaa wa Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2018/2019 (*The Appropriation Bill No.3, 2018*) na Muswada wa Sheria ya Fedha (*The Finance Bill No.4 , 2018*).

Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa hii, napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba tayari Miswada hiyo mwili imepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa Sheria za Nchi zinazoitwa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali Na.3, 2018 (*The Appropriation Act No.3, 2018*) na Sheria ya Fedha ya Mwaka 2018 (*The Finance Act No.4, 2018*).

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI-KATIBU WA BUNGE:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):-

Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kuhusu Muswada wa Sheria ya Kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi wa Mwaka 2018 (*The Dodoma Capital City (Declaration) Bill, 2018*). (*Makofi*)

MHE. GEORGE M. LUBELEJE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimponegeze sana Mheshimiwa Christopher Chiza kwa kurudi tena Bungeni. (*Makofi*)

Maoni ya Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Muswada wa Sheria ya Kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi wa Mwaka 2018 (*The Dodoma Capital City (Declaration) Bill 2018*). (*Makofi*)

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI JUU YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:-

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kuhusu Muswada wa Sheria wa Kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi wa Mwaka 2018 (*The Dodoma Capital City (Declaration) Bill 2018*). (*Makofi*)

SPIKA: Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI-KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, swali la kwanza linalelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Angelina Malembeka, kwa niaba yake Mheshimiwa Saada Mkuya nimekuona.

Na.1

**Wabunge wa Viti Maalum kwa
Kuzingatia Asilimia za Majimbo yao**

MHE. SAADA MKUYA SALUM (K.n.y. ANGELINA ADAM MALEMBEKA) aliuliza:-

Baadhi ya Wabunge wa Majimbo walihama Vyama vyao na kujiunga na vyama vingine hivyo Chaguzi Ndogo zikafanyika na Chama cha Mapinduzi kikashinda Majimbo hayo:-

(a) Je, ni nini hatma ya Wabunge wa Viti Maalum walioingia Bungeni kuititia asilimia za Majimbo yao ya Uchaguzi?

(b) Kwa kuwa Chama cha Mapinduzi kimeongeza idadi ya Majimbo zaidi, je, ni lini Wabunge wa Viti Maalum wapya wa CCM kuititia Viti Maalum wataingia Bungeni?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Antony Mavunde, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 78(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imemeanisha bayana kuwa vyama vya siasa vilivyoshiriki Uchaguzi Mkuu na kupata angalau asilimia tano ya kura zote halali za Wabunge vitapendekeza kwa Tume ya Uchaguzi majina ya wanawake kwa kuzingatia uwiano wa kura ambazo kila chama kimepata katika uchaguzi wa Wabunge ili Tume iweze kuteua miongoni mwao Wabunge wa Viti Maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa msingi wa sheria hii, idadi ya Wabunge wa Viti Maalum kwa kila chama inapatikana wakati wa Uchaguzi Mkuu ambao hufanyika kila baada ya miaka mitano. Hivyo, mabadiliko yoyote yanayotokea wakati wa Uchaguzi Mdogo hayaathiri idadi ya Viti Maalum vya chama husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali imeendelea kupokea maoni na ushauri kuhusu jambo hili hivyo kutokana na hali ilivyo hivi sasa, Katiba na Sheria za Nchi vitaendelea kuwa msingi mkuu wa ufanuzi na mgawanyo wa Viti Maalum Bungeni.

SPIKA: Mheshimiwa Saada Mkuya, swali la nyongeza.

MHE. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake, hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa utaratibu huu uliopo hivi sasa na *tendencytunayoionna*, je, Serikali haioni inanyima fursa uwakilishi wa wanawake hapa Bungeni kutokana na ongezeko la Viti hususani kwa upande wa Chama cha Mapinduzi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa sababu mwongozo huu unatokana na sheria, sasa ni lini Serikali italeta mabadiliko haya ya sheria hapa Bungeni ili tuweze

kurekebisha tuone kwamba idadi ya wanawake inaongezeka hapa Bungeni? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu. Swali hilo ni muhimu sana, lini unaleta sheria ili wawe wanapungua? (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA

VIJANA): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Saada Mkuya, kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya awali, msingi wa mgawanyo wa Viti Maalum unatokana na Ibara ya 78(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kama ilivyo ada, pamekuwepo na marekebisho mbalimbali ya Katiba kutokana na mahitaji. Inapotokea haja ya kufanyika hivyo basi Serikali tutaona umuhimu wa kuona jambo hili kwa uzuri zaidi ili iweze kubadilishwa kuendana na mazingira ya wakati husika, lakini kwa hivi sasa msingi unabaki kuwa Ibara ya 78(1) ya Katiba ndiyo ambayo inatuongoza.

SPIKA: Sasa mnataka kuuliza nini tena Waheshimiwa? Haya Mheshimiwa Pauline.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa taratibu zetu, Wabunge wa Viti Maalum wanapokuwa wamechanguliwa na vyama vyao na NEC imewapitisha wanakuwa wamechagua Halmashauri zipi wahudumu na huko wanakuwa wameapishwa na wanashiriki kama Madiwani na stahiki zingine wanazipokea. Naomba kufahamu inakuwaje Mbunge wa Viti Maalum anatoka kwenye Halmashauri ya awali anakohudhuria anahamia kwenye Halmashauri nyingine na anachukua posho kwenye Halmashauri mbili tofauti yeche mwenyewe, je huu siyo wizi? (*Makofii*)

SPIKA: Swali hilo haliendani na swali la msingi kabisa, liko nje, kwa hiyo tunaendelea na maswali mengine. Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti uliza swali lako.

Na. 2

Tume Huru ya Uchaguzi

MHE. MARWA R. CHACHA aliuliza:-

Ili kuinusuru amani ya nchi yetu baada ya Uchaguzi Mkuu ni kuwa na Tume Huru ya uchaguzi:-

Je, ni lini itaanzishwa Tume Huru ya Uchaguzi kwa mujibu wa sheria?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 74(1)-(15) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo imemainisha na kufafanua kuhusu muundo, majukumu pamoja na uhuru wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika utekelezaji wa majukumu yake ya msingi.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwa Mfumo wa Vyama vingi vya Siasa nchini mwaka 1992, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeratibu na kuendesha kwa ufanisi chaguzi tano za Rais, Wabunge na Madiwani pamoja na chaguzi ndogo mbalimbali za Wabunge na Madiwani.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huu, Tanzania tayari inayo Tume Huru ya Uchaguzi.

SPIKA: Mheshimiwa Marwa Chacha, swali la nyongeza.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba yetu ya nchi hii ya 1977, Afisa wa Tume ya Uchaguzi hapaswi kuwa mwanachama wa chama chochote cha siasa. Wakurugenzi na Watendaji wanaosimamia chaguzi ni wanachama wa CCM kwa ushahidi. Wengi waligombea Ubunge, walioshindwa wameteuliwa kuwa Wakurugenzi na hakuna sehemu yoyote ambapo wamejiuzulu uanachama wao na ndiyo wanaosimamia chaguzi hizi na imepelekea wagombea wa vyama vya upinzani wanaongombea Ubunge na Udiwani wananyimwa ama fomu ama wakirudisha fomu Wakurugenzi wanajificha. Je, hii ndiyo Tume Huru ya Uchaguzi? Hilo ni swali la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mimi mwenyewe nimeshiriki kwenye hizi chaguzi. Nimeenda sehemu moja inaitwa Nyabubinza kule Maswa Magaharibi. Mimi Mbunge, Mkuu wa Wilaya, *Ma-green guard* na Polisi wanadiriki kututeka tunaofanya kampeni kutoka upinzani. Hivi hii ndiyo Tume huru ya Uchaguzi? Huko mnakotaka twende ni wapi? Mnataka mpaka damu imwagike?

SPIKA: Marwa Chacha.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mnataka mpaka damu imwagike? Swali la pili...

SPIKA: Unakoelekeea ni kwingine kabisa.

MHE. MARWA R. CHACHA: Sawa, naenda.

SPIKA: Unakoelekeea ni uchochezisasa. Maswali mawili tayari umeshauliza.

MHE. MARWA R. CHACHA: Bado.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Marwa Chacha Ryoba, Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza alitaka kujua kama kweli hii ni Tume Huru ya Uchaguzi kwa mifano aliyotoa. Nikirejea katika majibu yangu ya msingi unaipimaje Tume ya uchaguzi ni huru. Uhuru wa Tume ya Uchaguzi unapimwa kutokana na majukumu ya Kikatiba yaliyopo ambapo utekelezaji wake ndiyo unaashiria kwamba Tume hii ni huru au siyo huru.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye Ibara ya 74(6) imemeanisha majukumu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambayo Kimsingi hasa majukumu hayo yakiingiliwa ndiyo unasema Tume hii imekosa uhuru. Jukumu mojawapo ni kubwa ni la kuratibu na kuendesha uchaguzi ambao ndiyo umefanya hata Marwa Ryoba Chacha leo yuko Bungeni. Kwa hiyo, sitaki kuamini kwamba majukumu haya ya Tume yanaingiliwa kwa mujibu wa swali ambalo amelileta. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili anasema kwamba alikwenda kwenye kampeni Maswa wakatekwa na je hii ndio Tume Huru ya Uchaguzi? Waheshimiwa Wabunge wenzangu hapa tuelewane kimsingi kabisa, tukizungumza Tume ya Uchaguzi maana yake ni Tume ambayo inayotokana na Ibara ya 74(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Unazungumza kuhusu kutekwa jambo ambalo la kijinai na ulipaswa kuliripoti Polisi lichukuliwe hatua na siyo jukumu la msingi la Tume la kushughulika na kutekwa kwa watu. (*Makofii*)

SPIKA: Sasa Mheshimiwa Marwa kama Tume hiyo siyo huru, mbona ilikutangaza wewe kuwa Mbunge wa Serengeti. (*Makof*)

Tunaendelea na TAMISEMI swali la Mheshimiwa Lusinde, kwa niaba yake jirani yake Mheshimiwa Badwel atauliza swali.

Na. 3

Barabara ya Mpunguzi – Ilangali

MHE. OMARY A. BADWEL (K.n.y. MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE) aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya kutoka Mpunguzi kupitia Nagula, Mpwajungu, Ituzi hadi Ilangali itapandishwa hadhi kuwa ya Mkoa ambayo itasimamiwa na Mkoa kwa maana ya *TANROADS*?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Josephat Kandege, Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mbunge wa Jimbo la Mtera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mpunguzi – Ilangali yenye urefu wa kilometra 88.3 ni barabara mjazo yenye tabaka la changarawe na udongo, ambayo inaunganisha Wilaya ya Dodoma, Bahi, Chamwino na kwa upande mwingine inaunganisha Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Iringa, Wilaya ya Iringa Vijiivji. Upande wa Dodoma Jiji ina kilometra tatu, Bahi kilometra 18.3 na Chamwino kilometra 67.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, Serikali ilitengeneza sehemu ya Mpunguzi hadi Nagulo kwa kiwango cha changarawe yenyе urefu wa kilometa 21.3 kwa gharama ya shilingi bilioni 3.032 katika mwaka wa fedha 2015/2016 kwa ufadhilli wa *DFID*. Aidha, barabara ya Mpunguzi – llangali katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali kupitia *TARURA* iliifanyia matengenezo ya sehemu korofи kwa urefu wa kilometa 17 yaliyogharimu shilingi milioni 86.2 na katika mwaka wa fedha 2018/2019, *TARURA* Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imetenga shilingi milioni 170 za kuifanya matengenezo ya muda maalumu kwa urefu wa kilometa 8.5 na kazi hii ipo katika hatua za manunuzi.

Mheshimiwa Spika, maombi ya kupandishwa hadhi barabara ya Mpunguzi – llangali kwa sasa yapo ngazi ya Mkoa. Pindi yatakapowasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana na kuonekana kwamba yanakidhi vigezo vilivyowekwa na sheria, barabara hii itapandishwa hadhi.

SPIKA: Mheshimiwa Badwel.

MHE. OMARY A. BADWEL: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa kuwa Serikali imeunda chombo kinaitwa *TARURA* na wakati huo kabla ya kuunda *TARURA* barabara zilizokuwa zinahudumiwa na Halmashauri ikaonekana utekelezaji wake si bora. Kwa kuwa tayari Serikali imeunda chombo hiki *TARURA* na lengo lake lilikuwa ni kuzifanya hizi barabara za mijini na vijijini kufikia hadhi kama hii ambayo tunaiomba kupandishwa hadhi kwa barabara. Je, nataka kujuu bado kuna haja ya kuendelea kuomba kupandishwa hadhi barabara zetu au *TARARU* ielekezwe kuchukua nafasi ya kutengeneza barabara hizi vizuri kama ilivyokuwa inatengeneza *TANROADS?* (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali imeunda chombo hiki kwa ajili ya kuboresha hizi barabara lakini bado kuna tofauti ya *TARURA* na *TANROADS* kwa

maana ya asilimia ya fedha wanazopewa na Serikali ambapo *TANROADS* wanapata asilimia 70 na *TARURA* wanapata asilimia 30. Je, ni lini sasa Serikali itazigawia sawa kwa sawa taasisi hizi mbili kwa maana ya *TARURA* wapate asilimia 50 na *TANROADS* wapate asilimia 50 ili utengenezaji wa barabara hizi uwe katika kiwango kinachokusudiwa? (*Makofj*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Josephat Kandege, Naibu Waziri TAMISEMI, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Badwel, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na kilio cha Waheshimiwa Wabunge kutaka barabara zao zipandishwe hadhi ili ziweze kuhudumiwa na *TANROAD*. Pia ni ukweli usiopingika kwamba tangu tumeanzisha chombo hiki cha *TARURA* ambacho kimsingi kinafanya kazi nzuri, kuna umuhimu wa kutathmini kama iko haja ya kutaka kupandishwa tena barabara hizi. Naamini kinachotakiwa ni kuhakikisha kwamba barabara hizi zinajengwa kwa viwango ili zilingane na zile ambazo zinazojengwa na *TANROADS*.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili kuhusu mgawanyo, iko haja lakini ni vizuri pia tukazingatia kwamba barabara nyingi ambazo zinajengwa na *TANROADS* zinajengwa kwa kiwango cha lami na barabara ambazo zinazojengwa kwa kiwango cha lami zinauhitaji mkubwa wa fedha ukilinganishwa na ambazo nyingi zinajengwa kwa changarawe na udongo. Kwa hiyo, ukifika wakati ambapo haja ikawepo kwamba tugawanye 50 kwa 50, naamini kwa mujibu wa taratibu zitakazofuatwa na Bunge lako likiidhinisha kwa mujibu wa sheria tutafika huko kwa siku za usoni.

SPIKA: Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Sonia Jumaa Magogo, uliza swali lako.

Na. 4

Msongamano wa Wanafunzi katika Darasa Moja

MHE. SONIA J. MAGOGO aliuliza:-

Je, Serikali inasaidiaje watoto wa Shule za Msingi Wilayani Handeni ambao wamekuwa wakisongamana sana kwenye darasa moja?

SPIKA: Mheshimiwa Sonia alipata mtihani mkubwa sana wa kiafya lakini sasa tunamshukuru Mwenyezi Mungu. (*Makofii*)

Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Joseph Kakunda.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba uniruhusu nimkaribishe Mheshimiwa Sonia kwenye kazi za Bunge baada ya kuwa ameugua kwa muda mrefu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sonia Jumaa Magogo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ongezeko la wanafunzi katika shule za msingi na sekondari ni moja ya changamoto iliyotokana na utekelezaji wa Sera ya Elimu Bila Malipo. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali ilikamilisha ujenzi wa vyumba vyta madarasa sita kwa kiasi cha shilingi milioni 40.96 katika shule za msingi Kwazala, Ugweno na Gumba na Mbunge wa Handeni Mheshimiwa Mbuni Mhita, kupitia fedha za Mfuko wa Jimbo alikamilisha ujenzi wa madarasa saba kwa gharama ya shilingi milioni 37.63 katika shule za Kabuku Mjini, Gole, Mnyuzi na Msilwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imejenga vyumba sita vyta madarasa kwa

gharama ya shilingi milioni 120 katika Shule za Mhalango, Kitumbi na Komkonga na kukamilisha ujenzi wa vyumba sita vya madarasa kwa gharama ya shilingi milioni 23.5 katika Shule za Kwachaga na Kibundu. Aidha, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 137.2 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba sita vya madarasa na matundu 12 ya vyoo katika Shule za Msingi Kiselya na Mhalango.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kujenga miundombinu ya elimu katika Halmashauri ya Handeni na inawaomba wananchi na wadau kushiriki kikamilifu katika juhudhi za kupunguza tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa, maana Serikali peke yake haitoweza kuwa na bajeti ya kutosheleza mahitaji yote ya Ujenzi wa miundombinu ya shule kwa kipindi kifupi.

SPIKA: Mheshimiwa Sonia.

MHE. SONIA J. MAGOGO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha na kujenga nyumba za walimu ili kuondoa adha ya tatizo hili ambalo limekuwa kubwa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha miundombinu ya majengo ya shule nyingi ambazo kipindi cha mvua watoto wamekuwa wakipata wakati mgumu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Joseph Kakunda, TAMISEMI, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sonia Jumaa Magogo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama tulivyojibu kwenye jibu la swali la msingi ni kwamba tunayo changamoto kubwa sana katika nchi ambayo ilitokana na kutekeleza mpango wetu wa maendeleo wa elimu ambao sasa hivi kuanzia mwaka 2015 mwezi Desemba, tunatoa Elimu Msingi Bila Malipo. Hiyo imevutia wanafunzi wengi zaidi kudahiliwa katika shule kuanzia elimu ya awali, elimu ya msingi na sekondari. Kwa hiyo, tuna uhaba mkubwa sana wa madarasa, nyumba za walimu na vyoo.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Serikali imejenga vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, matundu ya vyoo katika shule za msingi 6,200 nchi nzima na kazi bado inaendelea, tunaendelea kufanya hivyo kwa kushirikiana na wananchi. Katika shule za sekondari tumezifikia shule za sekondari 3,159, hii ni kazi kubwa na ndiyo maana nikatoa wito kwamba jambo hili haliwezi kufanywa na Serikali peke yake, tuna jumla ya shule 22,000 za msingi na sekondari. Sasa kama tumefikia shule 9,000 bado tuna kazi kubwa ya kufanya, tunataka mpaka ifikapo mwaka 2020 angalau tuwe tumezifikia shule 17,000, hatuwezi kuzifikia shule 17,000 peke yetu bila ushirikiano wa wananchi.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Salma Kikwete, tafadhali swali.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona, naomba niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Shule ya Msingi Majimatitu ina wanafunzi zaidi ya 4,000 hali ambayo husababisha wanafunzi wasipate haki yao ya msingi kitaaluma. Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka kuhakikisha shule hii inaongezewa madarasa pamoja na kwamba amesema kuna shule nyingi zinaongezewa madarasa? Ahsante. (*Makof!*)

SPIKA: Looh! Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, kama umesikia hiyo takwimu ya Mheshimiwa, Shule ya Msingi Majimatitu ina watoto 4,000. Karibu kwa majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Salma Kikwete, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, shule ambazo zina wanafunzi zaidi ya 1,500 ni shule ambazo kwa kweli zimezidiwa na wanafunzi wanaohitajika kuwa katika shule moja. Kwa maana kwa viwango ambavyo vinakubalika shule ikiwa na wanafunzi 4,000 kwa kweli ni suala ambalo linahitaji tulishughulikie haraka sana. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Kikwete na wadau wengine wote wa hii Shule ya Msingi Majimatitu kama kweli ina wanafunzi 4,000 basi tutapeleka jicho letu haraka sana ikiwezekana basi tuigawanye ile shule ziwe shule mbili.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Salma Kikwete ni Mbunge wa Kuteuliwa siyo Mbunge wa Viti Maalum. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, TAMISEMI.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Naibu Waziri wangu kwa majibu mazuri sana ya awali.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kuongezea tu kidogo, ni kweli shule ya Msingi Majimatitu mwaka jana darasa la kwanza peke yake walikuwa wanafunzi 1,200 na hii ni kutokana na programu ya elimu bure ambapo watoto wengi waliokuwa wanakosa fursa ya elimu wameenda pale. Serikali tulichokifanya ni kutafuta eneo lingine kwa ajili ya kujenga shule pacha jirani. Naomba niseme kwamba Serikali itafanya kila liwezekanaloo ili ile shule pacha iweze kukamilika haraka

iwezekanavyo tupunguze idadi ya wanafunzi walioko katika Shule ya Msingi Majimatitu.

SPIKA: Mheshimiwa Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, Shule ya Msingi Iputi iliyoko Kijiji cha Mbunga katika Jimbo langu la Ulanga ina msongamano mkubwa sana wa wanafunzi. Sisi tumejenga wenyewe shule nyingine, tumejenga ofisi ya mwalimu kwa kushirikiana na Mbunge wao, tunachoomba usajili na kutuletea walimu. Je, Serikali ipo tayari? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu Mheshimiwa Waziri, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA TAWALA ZA MIKOZA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Godluck Mlinga, Mbunge wa Ulanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ametupa habari hapa Bungeni kuhusu Shule ya Msingi Iputi ambayo tayari wananchi kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge wao wameshaanza ujenzi wa miundombinu ya shule hiyo katika Kijiji cha Mbuga. Nataka nimhakikishie kwamba, naomba ushirikiano wake tutitoka hapa Bungeni leo tuwasiliane na wenzetu wa Wizara ya Elimu ili shule ile tuanze taratibu za kuisajili na tukishaisajili tutaipatia walimu.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Kilimo na swali la Mheshimiwa Jamal Kassim Ali.

Na. 5

Ukosefu wa Mitaji ya Kilimo

MHE. JAMAL KASSIM ALI aliuliza:-

Idadi kubwa ya Watanzania wanajishughulisha na kilimo ili kujipatia mapato na moja kati ya changamoto kubwa wanayokabiliwa nayo ni ukosefu wa mitaji ya kuwezesha shughuli zao kuwa na ufanisi na tija zaidi:-

Je, Serikali ina mikakati gani kupitia Benki ya Kilimo kuwasaidia wananchi hao kupata mitaji ya kilimo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jamal Kassim Ali, Mbunge wa Jimbo la Magomeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto za upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya shughuli za kilimo kutokana na taasisi nyingi za fedha kuweka masharti magumu hususan kwa waombaji kutoka sekta ya kilimo. Kutokana na umuhimu wa mitaji kwa ajili ya shughuli za kilimo, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali, kama kuhamasisha uanzishwaji wa Vyama vya Akiba na Mikopo (*SACCOs*), *VICOBA* na Mfuko wa Taifa wa Pembejeo. Mikakati mingine ni pamoja na kufungua Dirisha la Kilimo katika Benki ya Rasilimali (*TIB*) na kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Maendeleo ya Kilimo ilianda Mpango wa Biashara ambao umeainisha mikakati na hatua za kuchukua. Benki pia inatoa mikopo kwa muda mfupi, muda wa kati na mrefu kwa riba nafuu kupitia vikundi vya wakulima wadogo. Benki imejikita katika utafuta vyanzo vipyta vya mtaji ili kuimarisha uwezo wa benki. Aidha, Serikali

imeshaipatia benki hiyo mkopo wa gharama nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika wa shilingi bilioni 103.

Mheshimiwa Spika, mikakati mingine ambayo imeshaanza ni pamoja na kuratibu utoaji wa dhamana kwa mikopo itakayotolewa na mabenki na taasisi nyingine za fedha kupitia Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo (*Smallholder Farmers Credit Guarantee Scheme*) ambapo kiasi cha fedha *USD* milioni 20 kimetengwa; kufadhili miradi ya ubunifu vijijini kupitia Mfuko wa Ubunifu Vijijini (*Rural Innovation Fund*) ambapo kiasi cha fedha *USD* milioni 5 kimetengwa.

Mheshimiwa Spika, mikakati mingine ni kuanzisha Progaramu za Uwezeshaji wa Vijana wa Wanawake na kupanua huduma za kibenki kwa kuanzisha Ofisi za Kanda sita (6). Hadi sasa Benki imefungua Ofisi ya Kanda ya Kati Jijini Dodoma na Ofisi ya Kanda ya Ziwa Jijini Mwanza. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 itafungua Ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Jijini Mbeya na Ofisi Ndogo ya Kanda ya Magharibi Mjini Kigoma. Aidha, Kanda tatu zilizobaki ambazo ni za Kusini, Kaskazini na Zanzibar zitafunguliwa baadaye.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Julai, 2018, Benki imeshatoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 48.67 ambayo imewanufaisha wakulima 527,291 katika Mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Morogoro, Tanga, Manyara, Kagera, Arusha, Zanzibar na Mikoa ya Kanda ya Ziwa. Aidha, Serikali itaendelea kuongeza mtaji wa Benki ya Kilimo na kuhamasisha uanzishwaji na usimamizi wa vyama vya ushirika ili kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa wakulima.

SPIKA: Mheshimiwa Jamal Kassim Ali, nilikuona.

MHE. JAMAL KASSIM ALI: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Naibu Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya. Pamoja na majibu mazuri aliyotoa nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, kwa vili Sera ya Serikali yetu ni kwenda kwenye uchumi wa viwanda na viwanda vingi vimekuwa na uhaba wa malighafi ambazo zinatokana na bidhaa za mazao na kupelekea viwanda vyetu kuagiza malighafi kutoka nchi za nje, je, Serikali ina mkakati gani kupitia benki hii sasa kuanza kukopesha wakulima wakubwa ambao wataongeza uzalishaji wa malighafi ambazo zitaenda kulisha viwanda vyetu?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, benki hii imekabiliwa na uhaba wa mtaji, ilianzishwa kwa mtaji wa shilingi bilioni 60 lakini lengo lake ilikuwa kufikia mtaji wa shilingi bilioni 80. Je, nini *commitment* ya Serikali kuhakikisha kwamba mtaji wa benki hii utaongezeka ili kusaidia kuongeza idadi ya wakopeshaji lakini pia kuongeza *single borrow limit* kama ambavyo maelekezo ya *BOT*yameelekeza?

SPIKA: Majibu ya swalii hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Jamal, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nieleweke kwamba Benki yetu ya Kilimo ni benki ya kisera tofauti na zile benki zingine za kibashara. Benki hii ya Kilimo ambayo ni ya kisera ilikuwa imeundwa kwa makusudi maalum kwa ajili ya kusaidia wakulima wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika swalii lake hili kuhusu wakulima wakubwa, ni kweli hawa *Niche Farmers* kwa maana ya wakulima wakubwa sera na sheria yetu ni katika kuhakikisha kwamba na wenyewe wanafanya na wakulima wadogo kwa maana ya *outgrowers* ili kuweza kuongeza ule mnyororo wa thamani katika mazao yetu ya kilimo. Katika Benki yetu ya Kilimo ni kwamba wenyewe tunaposema ni benki ya kisera ni kwa sababu riba yao ni ndogo zaidi kutoka asilimia 8 hadi asilimia 12 kulingana na wakati ule ambao

wao wenyewe wanaomba kama ni muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ambao unafika miaka 15.

Mheshimiwa Spika, katika swalı lake la pili kuhusu mkakati pamoja na mtaji, kama nilivyo sema hii ni benki ya kisera kwa maana hiyo Serikali imewekeza asilimia 100 katika benki hii ili kuhakikisha kwamba inawakomboa wakulima.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na swalı la Mheshimiwa Janeth Massaburi. Kwa niaba yake aliyejiaandaa, Mheshimiwa Dkt. Chegeni nimekuona.

Na. 6

Chuo cha Uvuvi Mbegani - Bagamoyo

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI (K.n.y. MHE. JANETH M. MASSABURI) aliuliza:-

Je, Serikali haioni kuwa kusuasua kwa Chuo cha Uvuvi Mbegani - Bagamoyo na vyuo vingine kutokana na kukosa bajeti ya kutosha ya kuiyendesha vyuo hivyo kumechangia kupoteza ajira kwa vijana ambao kama wangepata mafunzo ya ufugaji samaki wangeinuka kimapato?

SPIKA: Majibu ya swalı hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swalı la Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi kwa kuwa ni

kiongozi wa mfano kwa ufuatiliaji na kitendo chake cha kuwalipia watoto wake wawili kupata mafunzo ya ufugaji wa samaki katika Chuo cha Mbegani kwa muda wa wiki moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha mafunzo ya uvuvi kwa kuanzisha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (*FETA*) mwaka 2012 ambapo udahili umeongezeka kutoka wanafunzi 714 mwaka 2011/2012 hadi kufikia wanafunzi 1,196 katika mwaka wa 2016/2017. Pia, *FETA* imekuwa ikipokea fedha kutoka Serikalini ambapo katika mwaka wa fedha 2017/2018 ilipatiwa jumla ya shilingi milioni 246 kwa matumizi ya kawaida, katika mwaka huu wa fedha wametengewa shilingi milioni 580 kiasi ambacho ni zaidi ya mara mbili ya kile walichokipata katika mwaka uliopita.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa ya maendeleo iliyofanyika katika kipindi hiki cha miaka sita ya uhai wa *FETA* ni pamoja na kukarabati miundombinu ya vituo vya Mikindani - Mtwara, Kibirizi - Kigoma, Mwanza South pale Mwanza na Gabimori – Rorrya. Vituo vya Mwanza South na Kibirizi tayari vimeanza kutumika kutoa mafunzo ya ufugaji wa samaki wakati vile vya Mikindani na Gabimori viko tayari kuanza kazi ya utoaji wa mafunzo na Serikali kupitia Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma tayari imekwishafanya kazi ya zoezi la usaili ili kupata wakufunzi 18 watakaopelekwa katika vituo hivyo ili kuviwezesha kuanza kazi katika mwaka huu wa fedha wa 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya mazungumzo na Jumuiya ya Ulaya (*EU*) ambayo imekubali kusaidia Wakala wetu hii *FETA* katika kujenga uwezo wa kitaasisi ili kupanua mafunzo ya kiufundi yanayolenga kuongeza idadi ya vijana watakaojajiri ama kuajiriwa katika sekta ya ufugaji samaki. Utekelezaji wa mradi huu unaanza katika mwaka huu wa fedha 2018/2019 kwa kuandaa mitaala, miundombinu ya kufundishia na kujifunzia pamoja na kuwajengea uwezo wakufunzi wetu.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Chegeni, nilikuona.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Wazir, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ajira kubwa sana ipo kwenye sekta ya kilimo na uvuvi na Tanzania tumejaliwa kuwa na rasilimali hii ya ziwa pamoja na bahari lakini majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri naona amajielekeza kidogo kutokujibu swal la msingi la Mheshimiwa Massaburi, ambaye ye ye alitaka kujua pamoja na mafunzo yanayoendelea au mazungumzo yanayoendelea na *EU* nini mkakati wa Serikali kuongeza udahili wa hao wanafunzi? Maana yake 1,100 ni namba ndogo sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Mikoa ya Kanda ya Ziwa ikiwemo Wilaya ya Busega ni wadau wakubwa sana wa Ziwa Viktoria na zoezi la uvuvi haramu limeathiri sana vijana na hawana ajira. Nini mkakati wa Serikari wa kuwasaidia vijana hawa ambao sasa hawana ajira waweze kupata ajira? (*Makof!*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swal lake la kwanza ni juu ya mkakati wa Serikali wa kuongeza udahili. Kama nilivyojibu katika swal letu la msingi tumehakikisha tunaimarisha vyuo vyetu vilivyo chini ya Wakala huu wa Uvuvi kwa maana ya *FETA* vile vya Gabimori na kule Mwanza, Mtwara na Kigoma. Kwa hivyo, kazi kubwa tuliyonayo katika mwaka huu wa fedha ni pamoja na kwenda na mpango wetu wa kushirikiana na wenzetu wa *European Union* ili mradi tuweze kuongeza uwezo wa kitaasisi ambao utapelekeea kuendelea kuongeza idadi ya wanafunzi katika vyuo vyetu lakini kuwa na uwezo wa kitaaluma na kiteknolojia pia. Kwa hivyo, Mheshimiwa Mbunge ahakikishe tu kwamba wanafunzi au vijana waliopo

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

katika Jimbo lake wawe tayari na wao kuweza kuingia katika vyuo hivi hasa kwa yeye palepale Mwanza Nyegezi ambapo watapata elimu hii na kule Rorya vilevile.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni mkakati gani tuliona kama Serikali, baada ya kuendesha Opesheni Uvvi Haramu na vijana wengi kuwa wamekosa ajira tunawasaidiaje ili waweze kurudi katika ajira yao. Mkakati wetu Mkuu ambao umeelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Ibara ya 25 mpaka ya 27 ni kuhakikisha kwamba tunawaunganisha vijana hawa katika vikundi vyatayari na kazi hii tumeshianza.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati njema sana tunashirikiana vyema na Shirika letu la Umma la Hifadhi ya Jamii ya NSSF, tunao mpango unaoitwa Wavuvi Scheme. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Chegeni kwamba niko tayari kwenda kutoa elimu hii na wataalam wangu pale Busega ili vijana wa pale Busega wajunge katika ushirika, kisha waweze kupata faida ya kuweza kupata mikopo na faida zingine zinazotokana na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

SPIKA: Mheshimiwa Neema William Mgaya, leo Waheshimiwa ni kwa sababu ya muda tu ndiyo maana mnaona nakimbia kidogo.

Na. 7

Uhitaji wa Kiwanda cha Maziwa katika Shamba la Kitulo

MHE. NEEMA W. MGAYA aliuliza:-

Halmashauri ya Makete ni mionganini mwa Halmashauri zinazozalisha maziwa ya ng'ombe kwa wingi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kiwanda cha Kusindika Maziwa katika shamba la Ng'ombe la Kitulo Makete - Njombe?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri Mifugo na Uvubi, Mheshimiwa Abdallaah Ulega, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shamba la Mifugo la Kitulo linalomilikiwa na Serikali lipo Wilaya ya Makete, Mkoa wa Njombe na lina mifugo kwa maana ya ng'ombe wa kisasa wapatao 799. Ng'ombe walioko Kitulo utumika kuzalisha mitamba pamoja na maziwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ina mpango wa kuboresha Shamba la Mifugo la Kitulo kwa kuboresha kosaafu za ng'ombe kwa kununua ng'ombe bora wa maziwa aina ya *Holstein Friesian* majike 400; kuongeza ng'ombe bora wa maziwa kutoka 450 waliopo hadi kufikia ng'ombe bora wa maziwa 1,200; kuongeza uzalishaji mitamba ya kuuza kutoka mitamba 80 kwa mwaka hadi mitamba 213 kwa mwaka; na kuongeza uzalishaji wa maziwa kutoka lita 400,000 kwa mwaka hadi lita 3,350,816 kwa mwaka ifikapo mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Njombe una Kiwanda cha Kusindika Maziwa cha *Njombe Milk Factory*, wakati Mkoa wa jirani wa Iringa una viwanda vya *ASAS Dairy* na *Mafinga Milk Group* ambapo kwa pamoja viwanda hivi vina uwezo wa kusindika lita 56,600 za maziwa kwa siku lakini vinasindika lita 18,300 tu kwa siku. Hivyo, wananchi wa mikoa hii wanayo fursa kubwa ya kuongeza uzalishaji wa maziwa ili kuweshe viwanda hivyo kusindika kulingana na uwezo wa viwanda hivi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri ya uanzishwaji wa viwanda ikiwemo kuboresha miundombinu ya barabara; kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika; kuondoa kodi kwenye mitambo na vifaa vya kupoozesha na kusafirishia maziwa;

pamoja na kuhamasisha viwanda hivi kununua magari maalum ya kusafirisha maziwa ili viweze kufikia wafugaji katika maeneo yao.

SPIKA: Mheshimiwa Neema, nilikuona swali la nyongeza.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, nimekuwa nikihamasisha sana wananchi wa Mkoa wa Njombe hususani akina mama kufuga ng'ombe wa maziwa. Je, ni Serikali itawasaidia kina mama hawa wa Mkoa wa Njombe katika suala la kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kusindika maziwa ili kuweza kuinua uchumi wa nchi yetu? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, Tanzania tumebarikiwa kuwa na ng'ombe wengi sana, je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuweza kuanzisha mashamba ya ng'ombe wa maziwa katika Wilaya mbalimbali ikiwemo Wilaya ya Chato - Mkoani Geita, Wilaya ya Busega - Mkoani Simiyu na Kilolo - Mkoani Iringa? (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Neema, yaani hukuweza kutaja hata Kongwa pia? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema Mgaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Neema Mgaya. Katika hili aliloliomba Serikali na kuiuliza nini mkakati wake juu ya kuanzisha viwanda vidogo vidogo, yeye amekuwa *champion* wa jambo hili. Katika mwaka huu tumemshuhudia akiwapa *support* akina mama wa Mkoa wa Njombe kwa kuwapa vyerehani

ambavyo tunavitafsiri kuwa ni viwanda vidogo, kwa hivyo nampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, nataka nimhakikishie tu kwamba Serikalini hasa Mkoa wa Njombe umekuwa ukipata faida kubwa sana ya ushirika wa vyama vidogo vidogo ambavyo vinafanya kazi ya usindikaji wa maziwa. Pale Mufindi viko vyama vidogo vidogo vingi sana. Naomba pia uniruhusu niwapongeze Wabunge wa Mufindi karibu watatu, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mheshimiwa Mendrad Kigola na Mheshimiwa Cosato Chumi wa Mufindi. Nimekuta pale kuna vyama vingi vya ushirika na hivyo nataka nimuombe Mheshimiwa Neema Mgaya na yeye aweze kushirikiana na Wabunge hawa wa Majimbo waweze kuvisaidia vyama vile vya ushirika viweze kusindika maziwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni jambo linalohusu ni lini Serikali itakwenda kuanzisha mashamba katika Wilaya mbalimbali. Bahati njema sana katika wilaya hizi alizozitaja tayari tuna shamba kubwa katika Kanda ya Ziwa la Mabuki, ambalo lina ng'ombe wazuri na bora kabisa. Naomba nitangaze kwa Waheshimiwa Wabunge wote shamba letu la Mabuki sasa lina ng'ombe wa kuza, wanyama na wa maziwa wazuri ambaao kwa kusema ukweli hata wateja sasa wamebungua sana. Tunawahamasiheni karibuni mnunue ng'ombe pale kwenye shamba letu. Ng'ombe wazuri wanaanza Sh.1,500,000 mpaka Sh.1,800,000 kwa ajili ya nyama na maziwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mgaya kwamba kwa upande wa eneo hilo tunalo shamba zuri na kwa Kilolo kule tuna shamba zuri lile la Sao Hill. Hapa Kongwa kwa Mheshimiwa Spika pia tunayo Ranchi yetu ya Kongwa ambayo ina ng'ombe wazuri na Spika na wananchi wa pale Kongwa ni mionganini mwa watu ambaao wanawenza kufaidika kwa ng'ombe wale wazuri kwa ajili ya ufugaji bora. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, tafadhali ulizwa swali lako.

Na. 8

Kutafuta Soko na Kuboresha Zao la Mwani

MHE. ZAYNAB M. VULU aliuliza:-

Kilimo cha mwani kinalimwa baharini na asilimia kubwa ya wakulima wa zao hilo ni wanawake:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha zao hilo?

(b) Je, Serikali inamsaidiaje mkulima wa mwani kupata soko la uhakika hususani nje ya nchi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, bado tuko Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kilimo cha zao la mwani kinachofanyika katika mwambao wa Bahari ya Hindi ni mionganoni mwa shughuli za sekta ndogo ya ukuzaji wa viumbe kwenye maji ambapo jumla ya tani 1,197 zenye thamani ya shilingi milioni 412 zilivunwa na kusafirishwa nje ya nchi mwaka 2016/2017. Aidha, tani 1,329 zenye thamani ya shilingi milioni 469 zilivunwa mwaka 2017/2018. Mwani hulimwa zaidi na wanawake wanaokadiriwa kuwa asilimia 90 ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005 Serikali ilianda Mpango Madhubuti wa Maendeleo ya Mwani kwa lengo la

kukabiliana na changamoto za kilimo cha mwani zikiwemo kiasi kidogo cha mwani kinachozwalishwa na wakulima pamoja na mapato duni. Malengo mahsus ya Mpango Madhubuti wa Maendeleo ya Mwani ni pamoja na kujenga uwezo wa wakulima kujitegemea; kuongeza mwamko juu ya kilimo cha mwani kama shughuli inayozalisha mapato mazuri; na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji ambayo yanachochaea uwekezaji wa kisasa na kudumisha matumaini ya wadau wote wa tasnia ya mwani.

(b) Mheshimiwa Spika, mwani unaozalishwa nchini unauzwa katika masoko ya nchi za Ufilipino, Uchina, Ufaransa na Denmark. Pia kiasi kidogo cha mwani husindikwa hapa nchini na wadau kwa kutengeneza sabuni za mche, sabuni za maji na *shampoo*. Pia, mwani husindikwa ajili ya chakula na dawa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaongeza kasi ya utekelezaji wa Mpango Madhubuti wa Maendeleo ya Mwani ikiwa ni pamoja na kuongeza uzalishaji; kusaidia wananchi kuingia mikataba yenye tija na makampuni ya mwani; pamoja na kutafuta masoko mapya ya nje ili kusaidia wakulima kupata bei bora zaidi.

SPIKA: Mheshimiwa Zaynab, swali la nyongeza.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa kilimo cha mwani kimekuwa hatarishi kutokana na mazingira kinapolimwa na kinalimwa na wanawake wanaoishi katika visiwa na ukanda wa bahari. Kutokana na mazingira hayo hatarishi, je, Serikali ina mpango gani kuititia benki, mashirika au taasisi zinazoendesha masuala ya bima ili kuweza kwenda kuwafikia wanawake hao na kuwapa elimu ya kuweza kuwapatia fedha za kutosha ili waweze kujikwamua katika vifaa na halikadhalika kuweza kujikinga na athari zozote

zinazotokana na kilimo hicho kwa kuwa kinakuwa bahrini?
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kwa kuwa kilimo cha mwani mavuno yake ni mengi sana kutokana na zao lenyewe linavyofyonza maji mengi, je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha viwanda vidogo vidogo ili zao hilo liweze kuchakatwa na kuweza kusafirisha kwa wingi na kupata bei inayoweza kumkomboa mkulima wa mwani?

Mheshimiwa Spika, nashukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swalii hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Abdallah Ulega, hata kule Mkuranga wakulima wa mwani wapo.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya mama yangu, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoani kwetu Pwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ni uhatarishi wa kilimo chenyewe cha mwani ambacho kinalimwa kama ulivyo sema Msheshimiwa Spika ni pamoja na Jimboni kwangu Mkuranga katika Kata ya Kisiju kwenye Kisiwa cha Koma.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati njema sana Shirika letu la Bima la Taifa (*N/C*) limekuja na mpango la kuhakikisha kwamba linaanzisha Bima ya Kilimo. Kwa hivyo, kwa kutumia dirisha hili la Bima ya Kilimo kutoka *N/C* na kwa kutumia mpango wetu wa ushirika kwa vikundi vyta wakulima, naomba mimi na Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum mama yangu Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu na Wabunge wengine wakulima wa mwani tuwahamasishe wakulima wetu wa mwani kule vijijini wajunge katika ushirika na hatimaye tuwaunganishe na Shirika letu la Bima ili kuweza kupata nafuu hii endapo litatokea lolote la kutokea.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ameniuliza juu ya viwanda vidogovidogo. Ni kweli kwamba tunahitaji

kutengeneza viwanda vidogovidogo. Changamoto kubwa inayoonekana hivi sasa pamoja naye kusema kwamba uzalishaji ni mkubwa lakini kwa soko la kimataifa bado tunayo changamoto kubwa ya uzalishaji mdogo lakini na ubora wenyewe wa lile zao letu. Ndiyo maana tumeweke mkakati wa kuhakikisha tunazalisha zaidi na pili tunazalisha kilicho bora.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa viwanda vidogovidogo tumekuwa tukivisaidia sana pale Bagamoyo maeneo ya Mlingotini ni eneo mojawapo ambalo Wizara yangu inasaidia vidogovidogo. Kipo kiwanda kidogo ambacho kinafanya uchakataji na *ku-pack* mazao yanayotokana na zao hili la mwani. Sisi Serikalini tupo tayari kuhakikisha kwamba tunaendelea kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vidogovidogo na kuwapa *support* wakulima wetu.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri ametupa habari mpya, *very interesting*, kwamba kule Bagamoyo eneo la Mlingotini sasa kuna viwanda pia, tunashukuru kusikia hivyo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Dkt. Sware, nilikuona.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Spika, wakulima wa mwani sasa hivi wanapata shida kutokana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi kwa sababu ya ule mfumo wa ukulima unafanyika katika maji mafupi, mazao yale ya mwani mengi yamekuwa yakifa kwa sababu ya joto la maji na mchanga. Napenda kujua nini mkakati wa Serikali kuwawezesha wakulima hawa ambao wengi wao ni wanawake waweze kufanikiwa katika kilimo hiki ukiangalia sasa hivi wanapata tatizo la mabadiliko ya tabianchi uzalishaji wa mazao yao unashuka chini?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo kwa kifupi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mwalimu wangu Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kutokana na mabadiliko ya tabianchi kilimo cha mwani ambacho kilikuwa kikifanyika katika maji mafupi sasa kinawalazimisha wakulima wa mwani wasogee na waende katika maji marefu. Je, mkakati wetu ni nini kuwasaidia akina mama hawa ambao wana vifaa duni vya kuwapeleka katika haya maji marefu. Mojawapo ya mkakati ni kusitiza na kupatikana kwa zile kamba, tunayo teknolojia ya kamba za kisasa za kufunga mwani ule ili uweze kuwa imara zaidi na upate ubora zaidi. Pilli, ni kuwapa vyombo kwa maana ya boti ama mashine za kuwasaidia kuweza kufika walau kina kirefu kidogo. Kwa hivyo, huu ndiyo mkakati wetu na tayari Serikali tunazo mashine za kukopesha vikundi vya wavuvi, ikiwemo wakulima wa mwani. Kwa hivyo, Wabunge wote tunayo kazi ya kuvileta Wizarani vile vikundi vyetu ili tuweze kuwakopesha kile tulichonacho ili waweze kusogea katika hayo maji marefu zaidi. Ahsante.

SPIKA: Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Prosper Mbena, uliza swali lako.

Na. 9

**Ujenzi wa Barabara ya Bigwa – Kisaki kwa
Kiwango cha Lami**

MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO (K.n.y. MHE. PROSPER J. MBENA) aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya kutoka Bigwa – Mvuha – Kisaki katika Wilaya ya Morogoro Vijijini kwa kiwango cha lami?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena, Mbunge wa Morogoro Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Bigwa – Mvuha – Kisaki (km 133.28) ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) Mkoa wa Morogoro. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuititia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) tayari imeanza maandalizi ya ujenzi wa kiwango cha lami kwa barabara hii ambapo kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa sehemu ya Bigwa – Mvuha (km 78) inayofanywa na Kampuni ya Mhandisi Mshauri M/S *Unitech Civil Consultants Limited* ya Dar es Salaam imekamilika. Serikali ipo kwenye hatua ya kutafuta fedha za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Bigwa – Mvuha – Kisaki (km 133.28) utatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, Serikali inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya aina mbalimbali kwa barabara hii ili iweze kuitika majira yote ya mwaka ambapo katika mwaka wa fedha wa 2018/2019 jumla ya shilingi milioni 1,822.550 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali inaendelea na ukarabati kwa kiwango cha changarawe katika sehemu ya Mvuha – Kisaki (km 65.29). Sehemu hiyo ni kipande cha barabara ya Ubena Zomozi – Ngerengere – Mvuha – Kisaki Stiegler's Gorge inayoelekea katika Mradi wa Kufua Umeme wa Mto Rufiji (*Rufiji Hydropower Project*). Kazi za ukarabati

wa barabara hiyo unaendelea na utekelezaji wake umefikia asilimia 50.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Songea Mjini, nilikuona uliza swalii lako.

MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, kutokana na umuhimu wa barabara hii ambao unatupeleka kwenye *Stiegler's Gorge* na kuunganisha Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Pwani katika maeneo ya Kibiti, je, ni lini barabara hiyo itakamilika kwa kiwango cha lami ili masuala ya kiuchumi ya *Stiegler's Gorge*, kilimo na utalii yaweze kunufaika?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kwa kuwa tatizo hilo linafanana na tatizo lililopo la kuunganisha kati ya Wilaya ya Malinyi Mkoa wa Morogoro na Namtumbo Mkoa wa Ruvuma. Je, ni lini barabara hiyo inayounganisha Malinyi, Kilosa Mpapo, Londo mpaka Lumecha itaweza kujengwa angalau ipitike kwa kiwango cha changarawe kwa sababu sasa hivi haipitiki kabisa? (*Makof!*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaona umuhimu wa kutengeneza barabara hizi ambazo zinaelekea eneo hili la *Stiegler's Gorge* kwa kutokea Kibiti hali kadhalika ile barabara inayotokea upande wa Morogoro kama nilivyojibu katika swalii la msingi. Mheshimiwa Mbunge atakumbuka pia katika mwaka wa fedha kuna kiasi cha shilingi bilioni 5 zilitengwa

na kupitishwa na Bunge kwa ajili ya kuboresha barabara hii kutoka Kibiti kuelekea sehemu ya *Stiegler's Gorge*.

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa niseme kama Serikali tumejipanga kwanza kuhakikisha barabara hii inapitika ili iweze kutoa huduma kwa shughuli ambazo zitakuwa zinaendelea kufanyika katika eneo hili. Ule utaratibu wa kujenga katika kiwango cha lami utafanyika katika siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalı lake la pili, barabara inayotoka upande wa Malinyi, Kilosa kwa Mpepo kwenda Lumecha kule Namtumbo ukitokea Ifakara (km 499) usanifu ulishakamilika, Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kujenga barabara hii. Kwa hiyo, nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge avute subira pindi fedha zitakapopatikana barabara hii muhimu itaanza kujengwa. Hata hivyo, kuhusu kuboresha barabara hii ipitike Mheshimiwa Mbunge anafahamu yako maeneo ambayo ni hatari, yana milima mikali, tunajipanga ili kuhakikisha kwamba tunafungua barabara hii ili iweze kupitika muda wote kabla hatujaijenga kwa kiwango cha lami.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Eng. Chiza. Mheshimiwa Chiza, tafadhalii wanakusikiliza. (*Makofii*)

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Spika, kwanza niruhusu niipongeze Serikali kwa siku za karibuni imeongeza kiwango cha usimamizi wa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara kutoka Nyakanazi kuelekea mpaka Kabingo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa barabara hiyo inajengwa na inaishia katika kijiji cha Kabingo; na kwa kuwa kipande cha kutoka Kabingo kwenda mpaka Kibondo, Kasulu hadi Kidahwe bado ni vumbi. Je, kwa muendelezo huohuo ambaa Serikali imetuonyesha, ina mpango gani sasa kipande cha kutoka Kabingo kwenda Kibondo, Kasulu mpaka Kidahwe kiweze kutekelezwa ili Mkoa wa Kigoma uweze kufunguka? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Selasini, mbona hupigi makofi?
(Kicheko)

Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Chiza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uniruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Chiza kwa kuchaguliwa na wananchi wa Buyungu kuwa Mbunge na Mwakilishi wao na namkaribisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utaratibu wa kujenga barabara katika Mkoa wa Kigoma. Nafahamu na Mheshimiwa Chiza anafahamu pia kwamba barabara ya kutoka Nyakanazi kuja eneo lake ujenzi unaendelea, lakini utaratibu ule wa manunuzi unafanyika na hivi karibuni kilomita karibu 87 hivi zitaanza kujengwa zikipita katika eneo hili la Kabingo kama alivyoletaja. Pia kilomita zote 300, Serikali iko katika hatua nzuri ya kujenga kwa maana ya kutoka sasa upande wa Kakonko, Kibondo kwenda Kasulu na viunga vyake vinavyoenda kuunganisha nchi ya Burundi kwa maana ya Manyovu na kipande kile cha Mabamba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hatua iliyofikiwa ni nzuri na kwa vile Mheshimiwa Mbunge yupo nafikiri itakuwa ni vizuri sasa tuzungumze ili angalau nikupe picha ili uweze kuona na kutimiza wajibu wako kama Mbunge wakati ukiwawakilisha wananchi wako kwamba Serikali imejipanga vizuri kujenga barabara hizi.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, swalii la Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay Mbunge wa Mbulu Mjini.

Na. 10

Hitaji la Baraza la Ardhi Wilaya ya Mbulu

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY aliuliza:-

Mwaka 2016 Serikali kuititia Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi aliahidi kuipatia Wilaya ya Mbulu Baraza la Ardhi la Wilaya:-

(a) Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa na hatimaye Wilaya ya Mbulu kuwa na Baraza la Ardhi la Wilaya?

(b) Je, ni kwa nini Serikali isipime ardhi ya wananchi wa Wilaya ya Mbulu na kuwapatia hati ili kuondoa migogoro ya ardhi?

SPIKA: Majibu ya swalii hilo, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi, tafadhali.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mwishoni mwa Julai, 2018 Wizara kuititia Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma

imetangaza nafasi za ajira kwa ajili ya kupata Wenyeviti 20 wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Wenyeviti hawa ni kwa ajili ya Mabaraza 17 ambayo hayana Wenyeviti. Vilevile Wenyeviti wawili ni kwa ajili ya kuongeza nguvu kwenye Mabaraza katika Mikoa ambayo imeelemewa na mashauri mengi na ina Mwenyekiti mmoja kama Dar es Salaam na Mwenyekiti mmoja ni kwa ajili ya Baraza la Mbulu ambalo litafunguliwa na kuanza kufanya kazi punde taratibu za kupata watumishi wengine zitakapokamilika. Kwa ushauri wa Mkoa na Wilaya Baraza hili litakuwa Makao Makuu ya Wilaya ya Mbulu.

(b) Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ni kuhakikisha kuwa kila kipande cha ardhi nchini kinapimwa. Azma hii inatekelezwa kwa kupeleka huduma zote za sekta ya ardhi ikiwemo huduma za upimaji katika Ofisi za Ardhi za Kanda na Wapima wa Wilaya. Aidha, Wizara imekalimisha taratibu za kupeleka vifaa vyaa kisasa ambavyo vitasaidia zoezi hili la upimaji na TEHAMA katika ngazi za Kanda vyenye thamani ya shilingi bilioni 4.3 ambavyo zimekabidhiwa kwa viongozi wa Kanda wiki hii ambavyo vitasaidia sana katika kurahakisha zoezi hili la upimaji katika Wilaya zetu katika Kanda husika.

Mheshimiwa Spika, napenda kukumbusha kuwa jukumu la upimaji ni la Mamlaka ya Upangaji, hivyo, Halmashauri zote zinatakiwa kushirikiana na Wizara kuitia Afisa Ardhi, Ofisi za Ardhi za Kanda, kuhakikisha kuwa azma ya kupima kila kipande cha ardhi nchini inafikiwa.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Mbulu Mjini.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeze Serikali kuitia Waziri wa Ardhi kwa kazi kubwa inayofanya Wizara hii. Pili niulize maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza, kwa kuwa tatizo kubwa linalowakabili akina mama wajane, watoto, ambao wamepoteza wapendwa wazazi wao ni katika tatizo hili la kesi na mashtaka ya ardhi; na kwa kuwa familia nyingi zinazopata matatizo hayo hazina uwezo wa kifedha kuweka wanasheria. Je, ni kwa namna gani sasa Serikali itatafuta msaada wa kisheria kwa akina mama wajane na watoto warithi wa ardhi katika familia mbalimbali zinazopoteza wazazi wao? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, majibu ya Wizara yameniridhisha kwa kiasi kikubwa, je, ni kwa namna gani Wilaya ya Mbulu ambayo hivi sasa kesi nyingi zinazoendeshwa katika Baraza la Ardhi la Babati zinapata nafasi ya fursa ya kupimiwa ardhi kwa msaada wa Serikali, wananchi na wadau wengine ili tatizo hili la mashtaka mengi ya ardhi katika Baraza la Babati yapungue na hata kwa Mbulu kwa sababu hata tukipata Baraza bado tatizo litakuwa kubwa kwa mashtaka yatakayoendelea kutokana na hali hii ya kunyang'anyana ardhi kwa wale wenye uwezo na wasio na uwezo? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi, tafadhali.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge wa Mbulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali inao mkakati wa kutoa msaada wa kisheria kwa makundi kadhaa yenyе shida kama hizi, lakini kwanza kwa Mbulu tulifikiri kitu cha muhimu tusogeze huduma na kuanzisha Baraza la Ardhi kwa sababu tusingeweza kufikiria huduma za kisheria wakati huduma yenyewe haitolewi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge naomba

kwanza atuvumilie, mwaka huu Mungu akipenda lazima lile Baraza ambalo amelipigania kwa muda mrefu Mbulu Mjini litaanzishwa.

Mheshimiwa Spika, pia lile Baraza la Babati linaendelea kufanya kazi. Tutahakikisha kesi zote za Mbulu ambazo ni nyingi sana, tukishamuweka pale Mwenyekiti pale Mbulu kesi zote za Mbulu zitarudi Mbulu kutoka Babati ili angalau iwarahisishie hawa akina mama na watu wasio na uwezo waweze kupata hii huduma karibu na mahali wanakoishi. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Mbulu Vijijini, Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi, swali la nyongeza.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge wa Karatu siyo wa Mbulu Vijijini.

SPIKA: Samahani, Mbunge wa Karatu tafadhali.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, Mabaraza haya ya Ardhi hasa yale ya ngazi ya Kata yanafanya kazi kubwa sana kwa sababu yako karibu na wananchi lakini mabaraza haya yamekuwa na changamoto kubwa hususani eneo la maslahi yao kwa maana ya posho za usafiri na posho za vikao pamoja na vitendea kazi. Nini kauli ya Serikali juu ya kuhakikisha Mabaraza yale ya Kata yanawezeshwa ili yafanye kazi zao kwa ufanisi mkubwa?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu tafadhali.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika muundo huu wa Mabaraza tunaanza na Mabaraza hayo ya Kata na kwa muundo wake Wajumbe wengi wa Baraza lile ni wenyeji wa maeneo yale. Kazi hii kwa kweli ni ya kujitolea kwa sababu inarahisisha na inaondoa kero ya watu wao, hatuna mtumishi wa kudumu kwenye Baraza la Kata.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunatarajia wananchi wajue hilo na ikiwezekana Halmashauri za Vijiji vinavyozunguka Kata ile wafanye utaratibu wa kuchangia uendeshaji wa lile Baraza la Kata, kwa sababu Baraza lile la Kata linatakiwa kusimamia na kusuluuhisha migogoro kadhaa inayokuwepo katika maeneo yanayozunguka pale kwenye Kata. Baada ya hapo rufaa huwa zinaenda kwenye Baraza la Wilaya, kutoka kwenye Baraza la Wilaya rufaa zinakwenda Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, nataka nimuarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba hatuna posho kwenye Mabaraza ya Kata. Tunataraji kwamba viongozi wanaopendekezwa na wenzao kufanya kazi ile ni wale amba wana uwezo na wana uwezo wa kujitolea.

SPIKA: Tunaenda Wizara ya Nishati, swalii la Mheshimiwa Mbunge wa Ukerewe, Mheshimiwa Mkundi, kwa niaba yake Mheshimiwa Gekul.

Na.11

**Kupeleka Umeme katika Vijiji vya Kakerege na
Nkilizya - Nansio**

**MHE. PAULINE P. GEKUL (K.n.y. MHE. JOSEPH M.
MKUNDI)** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka umeme katika Vijiji vya Kakerege na Nkilizya vilivyopo Nansio Ukerewe?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Subira Mgusu, Naibu Waziri wa Nishati, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Nkilizya kina vitongoji saba (7) na kati ya vitongoji hivyo vitatu (3) vya Magereza, Kenonzo na Lwocho, vilipata umeme mwaka 2005 kuitia utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme Nansio Wilayani Ukerewe kutoka Wilaya ya Bunda ambapo wateja 60 waliunganishiwa umeme. Vitongoji viwili (2) vya Namalebe na Chamatuli vilipatiwa umeme mwaka 2012 kuitia ufadhili wa Benki ya Dunia na jumla ya wateja 47 wameunganishiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, vitongoji vingine viwili (2) vya Mumakeke na Bubange vya Kijiji cha Nkilizya visiviyokuwa na umeme, pamoja na Kijiji cha Kakerege vitapatiwa umeme kuitia Mradi wa *REA III*/mzunguko wa kwanza unaoendelea kutekelezwa kwa sasa. Kuitia utekelezaji wa mradi huu, jumla ya vijiji 35 katika Wilaya ya Ukerewe vitapatiwa umeme. Kampuni ya Nipo *Group Limited* aliyepewaa kazi za Mradi wa *REA III* katika Mkoa wa Mwanza anaendelea na utekelezaji mradi huo na mradi unatarajiwa kukamilika Juni, 2019.

Mheshimiwa Spika, kazi za Mradi wa *REA III* Ukerewe zinajumuisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 78.32; njia ya umeme wa msongo

wa kilovoti 0.4 yenyе urefu wa kilomita 156; ufungaji wa transfoma 78 za KVA 50 na 100; pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 2,640. Gharama ya mradi ni shilingi bilioni 9.28.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Babati Mjini, swali la nyongeza.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, maeneo mengi nguzo zimeshapelekwa katika vijiji hususani Mkao wangu wa Manyara, kinachokosekana ni zile *conductor* na nyaya kwa ajili ya kuunganisha zile nguzo na umeme uwake na Mkandarasi wetu wa Mkao wa Manyara ameagiza hizo *conductors* na nyaya muda mrefu viwandani na hili halijafanyika huenda hili tatizo lipo maeneo mengine. Naomba nifahamu ni lini sasa hizo *conductors* na nyaya zitatoka ili umeme uwake kwenye maeneo na vijiji vyetu ambavyo nguzo zimeshafikishwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, naomba nitambue jitihada kubwa ambazo zimefanywa na Wizara hii, wamelipa shilingi milioni 102 kwa fidia ya wananchi wa Haraa kwa ajili ya umeme huu wa *REA*, Naibu Waziri anafahamu tulilishughulikia kwa karibu sana. Nitambue jitihada za KV400 ambazo zimefanyika na hivi navyoongea katika Mkao wangu wa Manyara pale *TANESCO* Babati ...

SPIKA: Mheshimiwa Gekul, twende kwenye swali badala ya *story*.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshiwa Spika, ahsante. Jitihada hizi zinaendelea isipokuwa Mheshiwa Naibu Waziri kuna tatizo moja limejitokeza la *variation* kati ya Wizara ya

Fedha na Wizara ya Nishati kwa baadhi ya wananchi ambao wanadai fidia hii ya KV400. Naomba nifahamu, hili tatizo la *variation na reconciliation* kujua hawa wanastahili kiasi gani linamalizwa lini kabla hawajaondoka Babati waweze kupata fedha hizo?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, kwa kifupi Naibu Waziri, Mheshimiwa Subira Mgusu, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Pauline Gekul, Mbunge Babati Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa niaba ya Serikali tunapokea shukrani za Mheshimiwa Pauline kutokana na jitihada mbalimbali ambazo zimefanyika katika miradi hii ya REA. Amekiri na kutambua kwamba nguzo zimefika katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la vifaa vya *conductors* nyaya, nataka nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge ni kweli hivi vifaa kwa mfano *conductors* wanaagiza nje ya nchi, lakini kwa kuliona tatizo la ucheleweshaji ndiyo maana baadhi ya vifaa katika mradi huu tulitoa maelekezo viwanda vyetu vya ndani vizalishe na wakandarasi waagize. Kwa hiyo, suala hili la vifaa hususani nyaya, viwanda vinavyohusika ni ni *East African Cable* pamoja na *Kilimanjaro Cable*, jambo ambalo limejitokeza wakandarasi wengi wanapenda kuagiza kwa mtu mmoja.

Mheshimiwa Spika, tumetoa rai kwamba kwa kuwa Serikali ilivyotoa maagizo ya kuviezeshwa viwanda vya ndani kusambaza vifaa vya utekelezaji wa miradi hii, wakandarasi

wote waone namna gani ya *ku-order* hivi vifaa wasirundike *order* kwa mtu mmoja. Kwa hiyo, naomba nilichukue hili tuende tukashulighulikie kwa kuwa nguzo zimefika maeneo mengi, basi vifaa vilivyosalia vifike ili kazi ikamilike na wananchi wapate huduma ambayo imekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili nami nimshukuru kwa kufuatilia malipo ya fidia kwa wananchi wake na maeneo mbalimbali hususani katika mradi huu wa ujenzi wa njia ya umeme KV400 unaotoka Singida mpaka Namanga. Katika Wilaya yake kama alivyosema Serikali imeanza kulipa fidia, niishukuru sana Wizara ya Fedha kwa kutekeleza ahadi hiyo lakini amesema kuna *variation*. Naomba baada ya kikao hiki tukutane naye Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kushughulikia suala ambalo amelisema.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, swali la Mheshimiwa Bhagwanji.

Na.12

Hitaji la Gari na *Radio Call* – Kituo cha Polisi Chwaka na Jozani

MHE. BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka gari, *radio call* pamoja na vitendea kazi vingine katika Kituo cha Polisi cha Chwaka na Jozani?

SPIKA: Kwenye maonesho ya *TWPG* kule Mlimani City, Mheshimiwa Bhagwanji alitia fora sana kwa vazi maalum alilokuwa amevaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bhagwanji Maganlal Meisuria, Mbunge wa Chwaka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uhaba wa magari pamoja na vitendea kazi katika Vituo vya Polisi nchini kikiwemo Kituo cha Polisi Chwaka na Jozani. Hata hivyo, Jeshi la Polisi linaendelea na mchakato wa upatikanaji wa magari mapya yaliyonunuliwa na Serikali. Baada ya mchakato huu kukamilika, hatua za kuyagawa zitafuata kwa kuzingatia kiwango cha uhalifu katika maeneo husika, idadi ya watu na ukubwa wa eneo la doria.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi Chwaka kinatumia mawasiliano ya radio ya mezani kwa sababu umbali wa ilikofungwa mitambo ya mawasiliano ya radio za mkononi. Aidha, radio za mezani kwa ajili ya Kituo cha Polisi Jozani imekwishaplikana na mafundi wa Radio za Polisi wanamalizia ufungaji wake ili kurejesha mawasiliano ya uhakika katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, ni azma ya Serikali kuhakikisha kuwa inaboresha mawasiliano katika vituo vyote vya Polisi nchini kwa kutafuta *repeaters* (mitambo wa radio za mkononi) ambazo zitafungwa katika vituo visivyokuwa na mawasiliano ya radio za mkononi ikiwemo Chwaka na Jozani.

SPIKA: Mheshimiwa Bhagwanji Meisuria.

MHE. BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Naibu Waziri amesema maneno mazuri

naunga mkono. Hata hivyo, nataka nimwambie wananchi wa Jimbo langu la Chwaka wana matatizo vilevile. Wabakaji wengi na watu mbalimbali wanakuja kufanya uhaini katika Jimbo langu huko Chwaka na Jozani. Mimi mwenyewe nimeshachangia *computermoja* Jozani lakini nimeomba gari mbili angalau hata moja ipatikane kwa sababu hali ni ngumu na ni lazima tupate gari moja kwa heshima na taadhima.

Mheshimiwa Spika, ni hayo tu, naomba Serikali na Waziri wanipatie gari gari moja ya Polisi ili liweze kusaidia wananchi wa Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, gari moja linahitajika Chwaka, wabakaji wengi sana huko. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bhagwanji, Mbunge wa Chwaka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu swali la msingi kwamba mchakato utakapokamiliika wa upatikanaji wa magari kwa kuzingatia vigezo ambavyo nilivyovieleza tutaangalia kuona kama Chwaka inakidhi vigezo hivyo na idadi ya magari yaliyopo ili tupeleke. Nimuombe Mheshimiwa Mbunge avute subira mpaka magari hayo yatakapokuwa yamepatikana.

SPIKA: Tunahamia Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Leah Komanya, uliza swali lako tafadhalii.

Na.13

Kupeleka Fedha za Ruzuku katika Halmashauri kama Zilivyopitishwa na Bunge

MHE. LEAH J. KOMANYA aliuliza:-

Pamoja na nia nzuri ya Serikali kudhibiti ulimbikizaji wa madeni lakini kumekuwa na changamoto katika utekelezaji wa shughuli za kila siku katika Idara za Halmashauri za Wilaya zinazopokea ruzuku ya matumizi ya kawaida toka Serikalini:-

Je, ni lini Serikali itaanza kupeleka fedha za ruzuku katika Halmashauri za Wilaya kama zilivyopitishwa na Bunge?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Kijaji, tafadhalii majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, bajeti ni makadirio ya mapato na matumizi. Kinachoidhinishwa na Bunge lako Tukufu ni makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka husika. Pili, utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa sasa unafanyika kwa mfumo wa *cash budget*. Hivyo basi, ruzuku kutoka Serikali Kuu hupelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya kulingana na makusanyo halisi ya mapato ya mwezi husika. Serikali yetu kwa mtindo huo itaendelea kupeleka fedha za

ruzuku kwenye Halmashauri zetu kutokana na makusanyo halisi kutoka vyanzo mbalimbali via mapato.

SPIKA: Mheshimiwa Leah Komanya.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu.

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, kwa kuwa Serikali inapeleka fedha Halmashauri kulingana na makusanyo lakini kumekuwepo na malimbikizo ya madeni yanayotokana na stahiki za watumishi kama gharama za mazishi, matibabu yasiyo ya Bima za Afya, gharama za kufungasha mizigo kwa wastaafu, masomo na likizo. Je, ni lini Serikali italipa madeni ya mwaka 2016/2017 yallyohakikiwa na kuwasilishwa Januari, 2018? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kwa kuwa Serikali ilipunguza ruzuku ya matumizi ya kawaida kutoka asilimia 100 kwenda asilimia 40, mafungu niliyoyataja yanaonekana kuelemewa. Je, Serikali haioni ipo haja ya kufanya mapitio katika mafungu niliyoyataja na kuweza kuyaongezea bajeti?

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili muhimu, Naibu Waziri Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Leah Komanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalii lake la kwanza la kulipa madeni ambayo yameshahakikiwa, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali yetu imekuwa ikilipa madeni yote ambayo yamehakikiwa kwa ajili ya watumishi

wetu. Kama ambavyo nimekuwa nikiliarifu Bunge lako Tukufu ni mwezi Aprili tu Serikali yetu ililipa zaidi ya shilingi billioni 43 kwa ajili ya madai mbalimbali ya watumishi wetu katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuongezewa kwa bajeti katika mafungu aliyoyataja Mheshimiwa Leah Komanya, napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba katika mafungu ambayo tunayapa kipaumbele kuyapatia fedha za ruzuku ni Mafungu ya Utawala ambayo ndiyo yanashughulikia haya matatizo aliyoyasema kama gharama za mazishi na gharama za uhamisho. Kwa mfano, kwa mwaka huu 2017/2018 tuliomaliza tulikuwa na bajeti ya Sh.27,447,000,000. Kati ya hizi shilingi bilioni 27, Serikali yetu ilipeleka shilingi bilioni 22 kulingana na mahitaji yaliyoletwa kutoka kwenye Halmashauri zetu ambayo ni zaidi ya asilimla 90 ya bajeti ambayo ilikuwa imepangwa. Hili lilikuwa ni Fungu la Utawala ambalo ndilo linaloshughulika na madai mbalimbali aliyoyataja Mheshimiwa Leah Komanya.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo tunatoa kipaumbele kupeleka fedha za ruzuku ni katika Fungu la Elimu ambapo Serikali yetu imekuwa ikiajiri Walimu na tunahakikisha Walimu wetu wanalipwa pesa zao kabla hawajafika kwenye vituo vyao vya kazi au wanapofika tu kwenye vituo vyao vya kazi. Kwa mfano, kwa mwaka 2017/2018 tulipanga kupeleka shilingi bilioni 116 na tukapeleka zaidi ya shilingi bilioni 111 kulingana na mahitaji yaliyoletwa kutoka kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba tunajua umuhimu wa mafungu haya na tunayapa kipaumbele katika kuyapelekea fedha za ruzuku.

SPIKA: Swali la mwisho kwa siku ya leo kwa Mheshimiwa Mbunge Kasulu Mjini.

Mkoa wa Kigoma kuwa Miiongoni mwa Mikoa Maskini Nchini

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO aliuliza:-

Takwimu za Mpango wa Maendeleo 2016/2017 zimeonesha kuwa Mkoa wa Kigoma ni miiongoni mwa Mikoa mitano (5) iliyo maskini zaidi nchini:-

(a) Je, Serikali inafanya nini kuhakikisha Mikoa hiyo inapata rasilimali fedha na watu ili iweze kuondokana na hali hiyo ya umaskini?

(b) Je, nini kifanyike kwa Mkoa wa Kigoma ili kujenga ulinganifu katika maendeleo?

(c) Je, kwa nini Serikali isitenge shilingi bilioni 5 kwa kila mwaka kwa kila Mkoa ili kuondoa kitisho cha Mikoa hiyo kuachwa nyuma kimaendeleo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha na Mipango, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasuli Mjini, lenye vipengele (a), (b), (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali yetu huzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na mwaka mmoja mmoja pamoja na Mwongozo wa Bajeti kugawa rasilimali fedha na watu ili kukabiliana na changamoto za umaskini. Aidha, mgawanyo wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo huenda sambamba na mgawanyo wa rasilimali watu kwa ajili ya

utekelezaji, usimamizi, uperembaji na kutoa huduma kulingana na aina ya miradi.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kujenga ulinganifu wa maendeleo katika Mkoa wa Kigoma, Serikali imebainisha maeneo na miradi ya kimkakati kwa ajili ya utekelezaji ili kufungua fursa za kiuchumi. Miongoni mwa maeneo ya kimkakati yaliyobainishwa na kuanza kutekelezwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021 ni Mradi wa Upanuzi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kigoma; Mradi wa Uzalishaji wa Umeme wa Maji katika maporomoko ya Mto Malagarasi MW 44.7; kuanzisha na kuendeleza Eneo la Uwekezaji Kigoma (*Special Economic Zone*); Mradi wa Gridi ya Kaskazini Magharibi KV400; na ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa.

(c) Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa rasilimali fedha huainishwa kwenye Mwongozo wa Bajeti ya Serikali kwa kila mwaka ambao huandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano; Dira ya Taifa; na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala. Hoja ya kutenga shilingi bilioni 5 kwa kila Mkoa, kila mwaka ni lazima ifungamanishwe na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala. Hivyo basi, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa sasa Serikali haina Sera wala Mwongozo wa kutenga shilingi bilioni 5 kwa kila mwaka, kwa kila Mkoa ili kukabiliana na changamoto za umaskini.

SPIKA: Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Spika, naomba kwa ruhusa yako kabla sijauliza maswali yangu mawili madogo ya nyongeza, kwanza niwashukuru timu ya kampeni iliyotoka Kakonko, uniruhusu niwapongeze Wabunge wote wa CCM na Upinzani waliokuja Kakonko kwa kampeni. Tunasema tunashukuru sana kwa changamoto mlizotupa na tunaendelea kumpongeza Mheshimiwa Chiza kwa ushindi mnono alioupata. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno machache ya utangulizi, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, msingi wa swali langu ni mikoa ile mitano ambayo iko nyuma, ndiyo msingi wa hoja na si suala la llani ya Uchaguzi ya CCM, si suala la Mpango wa Miaka Mitano. Hoja ni mikoa mitano iliyoko nyuma ambayo inahitaji kupata *special attention*, inahitaji *equalization* ili iweze kulingana na mikoa mingine ndiyo msingi wa swali.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza la nyongeza ni kwamba miradi yote alioitaja ukiacha ujenzi wa reli ya katii, hiyo miradi hajatekelezwa na mingine ina miaka 20. Hiyo mikoa mitano iliyoko nyuma inahitaji kubebwa, kusaidiwa itoke katika maeneo yale ili iweze kuwa sawa sawa na mikoa mingine. Je, ni nini mkakati wa Serikali kwa mikoa hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili la nyongeza ni kwamba hiki kinachoitwa *North-West Grid*, ni mradi ambao una urefu wa kilometra 2,500 kutoka Tunduma – Nyakanazi kupitia Sumbawanga – Mpanda – Kigoma – Kasulu – Kibondo mpaka Nyakanazi. Je, mradi huu utakapoanza kutekelezwa kwa nini usiwe na wakandarasi zaidi ya watatu ili uishe kwa haraka ili wananchi tupate umeme katika maeneo haya? (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Majibu ya maswali hayo mawili, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza amesema msingi wa swali lake ni mikoa mitano maskini, lakini

alikwenda *specific* na kuutaja Mkoa wa Kigoma na ndiyo maana na mimi nilijibu *specifically* kwa Mkoa wa Kigoma, nini ambacho Serikali yetu inafanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba kupitia miradi ya maendeleo kama nilivyoitaja ndiyo fursa a kiuchumi hufunguliwa kwa ajili ya wananchi wetu kwenye mikoa husika. Kupitia Mpango wa Pili wa Maendeleo, mpango wa maendeleo wa mwaka mmoja mmoja, Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ndiko vipaumbele huwekwa kulingana na *geographical location* ya mikoa yetu na aina ya umaskini. Kwa hiyo, miradi hupangwa kulingana na miongozo hiyo niliyoitaja. Kwa hiyo, naomba tu Mheshimiwa Daniel akubaliane na jibu hili kwamba hatuwezi kupanga bajeti nje ya miongozo na mipango inayotuongozwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalı lake la pili ametoa pendekexo, tutakaa kama Serikali na Wizara ya Nishati kuona jinsi gani mradi huu wa *North – West Grid* utatekelezwa kwa haraka ili kurahisisha maendeleo ambayo tunayataka yafike kwa wananchi wetu.

SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Anna Lupembe, Mwenyekiti wa Ibada anawataarifu Wabunge wote kuhudhuria Ibada katika *chapel* ya Bunge leo saa saba mchana. Mheshimiwa Anna Lupembe anawaomba wanamaombi wenzake kushiriki ibada saa saba mchana leo.

Wageni 18 wa Mheshimiwa Eng. Christopher Chizza ambao ni familia yake, Waheshimiwa Madiwani na wapiga kura wake kutoka Kakonko Mkoani Kigoma wakiongozwa na mke wake Ndugu Elisafina Chizza. Karibuni sana, mama Chizza yuko wapi? Ahsante sana, karibu sana. (*Makofii*)

Wageni 25 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanamaombi kutoka Jiji la Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Nzuzu. Wanamaombi, karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni 36 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ambao ni kwaya ya Elishadi kutoka Chadulu Jijini Dodoma wakiongozwa na Ndugu Omega Mwaluko. Karibuni sana. (*Makofi*)

Katibu, tuendelee.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

NDG. RAMADHAN ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi wa Mwaka 2018 [The Dodoma Capital City (Declaration) Bill, 2018]

(*Kusomwa Mara ya Pili*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Jafo tafadhalii.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la mwaka 2016, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi wa Mwaka 2018 [*The Dodoma Capital City (Declaration) Bill, 2018*] kama ulivyochapishwa upya kwa mujibu wa Kanuni na maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Utawala na Serikali za Mitaa, sasa usomwe kwa mara ya pili na Bunge lako Tukufu ili lijadili na hatimaye lipitishe Muswada huu kuwa sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhamishia rasmi shughuli za Serikali katika Makao Makuu ya nchi Dodoma sambamba na uamuzi wa kuipandisha hadi Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma kuwa Halmashauri ya Jiji. Hatua hiyo inachochea ukuaji wa Mji wa Dodoma na maeneo yaliyozunguka Dodoma kiuchumi na kijamii. Aidha, kutungwa kwa Sheria ya Makao Makuu ya Nchi ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi CCM ya Mwaka 2015 kwa kuzingatia Sura ya 7, Ibara ya 151(a).

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo na uongozi wao imara uliowezesha kufanikisha kuandaa Muswada huu wa Sheria ya Kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi. Naomba kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika kwa uongozi wenu imara na madhubuti katika uendeshaji wa shughuli za Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa, naomba kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa chini ya uongozi wa Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu hiyo ya Bunge ambaye pia ni Mbunge wa Bukoba Vijiji na Mheshimiwa Mwanne Jumanne Mchemba, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, Mbunge wa Viti Maalum kwa maoni na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia na kuchambua muswada huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 31 Agosti, 2018, Kamati ilikamilisha kupitia na kuchambua Muswada wa Sheria ya Kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi wa Mwaka 2018 na kuridhia uendelee kwa hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na tatu katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge. Maoni ya Kamati yamesaidia kuboresha Muswada huu kupitia marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Adelardus Kilangi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Dkt. Everitus Lungova, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushauri na ushirikiano waliotupatia wakati wa kuandaa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Muswada. Muswada unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi [*The Dodoma Capital City (Declaration) Bill, 2018*] ili kutambua kisheria kuwa Dodoma ni Makao Makuu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la Muswada. Chimbuko la hoja ya kutunga sheria hii ni kukosekana kwa sheria inayotambua na kuweka msingi ya uendeshaji wa Makao Makuu ya nchi. Pamoja na jitihada zilizofanywa na Serikali katika kuendeleza Makao Makuu ya nchi, kukosekana kwa Sheria inayotambua Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi kulisababisha uendeshaji wa Makao Makuu ya nchi kutofikia malengo. Hivyo, msingi wa kutunga sheria hii ni kutambua kisheria Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu. Katika kutunga sheria hii jambo liliolizingatiwa ni kutambua na kulitangaza Jiji la Dodoma kisheria kuwa ni Makao Makuu ya nchi na kwamba wazo lolote la kubadilisha Makao Makuu ya nchi litahitaji ridhaa ya theluthi mbili ya Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mpangilio wa Muswada. Muswada huu umeanza na utangulizi unaoelezea chimbuko la Muswada. Kifungu cha 1 kinaweka masharti ya utangulizi yakiwemo jina la sheria inayopendekezwa.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 2 kinaweka masharti ya matumizi ya sheria hii kutumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 3 kinaweka tafsiri ya maneno yaliyotumika.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 4 cha Muswada kinahusu kutambulika kwa Dodoma kama Makao Makuu ya nchi na namna ambavyo Makao Makuu yanaweza kubadilishwa kupitia Bunge.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 5 kinaelekeza kwamba ustawishaji wa Makao Makuu utafanyika kupitia sheria mbalimbali zilizopo na zitakazotungwa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 6 kinazungumzia mipaka ya Makao Makuu ambayo itawekwa kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Baada ya maelezo haya, naomba Bunge lako Tukufu Ilijadili Muswada wa Sheria ya Kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi [*The Dodoma Capital City (Declaration) Act, 2018*] na kuridhia usomwe kwa mara ya pili na mara ya tatu na hatimaye kuwa sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Jafo.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

No.3

3rd September, 2018

SPECIAL BILL SUPPLEMENT

*to the special Gazette of the United Republic of Tanzania No.6. Vol.99 dated 3rd September, 2018
Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government*

THE DODOMA CAPITAL CITY (DECLARATION) ACT, 2018

ARRANGEMENT OF SECTIONS

<i>Section</i>	<i>Title</i>
1.	Short title.
2.	Application.
3.	Interpretation.
4.	Declaration of Capital City.
5.	Management of Capital City.
6.	Boundaries of Capital City.

NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly was published as a Special Bill Supplement No.1A of 7th June, 2018 and was First Read in the National Assembly on the 29th June, 2018. This Bill is now re-published for purposes of Second Reading and Third Reading.

Dar es Salaam,
31st August, 2018

JOHN W.H. KIJAZI
Secretary to the Cabinet

PREAMBLE

WHEREAS Dodoma is the City within Dodoma region which is strategically located in the centre of the United Republic of Tanzania and the location makes it easily accessible and potential for economic, political and social development;

WHEREAS considering this strategic location of Dodoma, in 1973 the then President of the United Republic of Tanzania and Founder of the Nation, His Excellency, **MWALIMU JULIUS KAMBARAGE NYERERE** preferred and declared Dodoma to be the Capital City of the United Republic of Tanzania;

WHEREAS following the declaration by His Excellency, **MWALIMU JULIUS KAMBARAGE NYERERE**, the Government had for quite a long time taken various initiatives to develop the City of Dodoma with the view to achieving the objective of making Dodoma the Capital City;

WHEREAS on the 26th April, 2018 His Excellency, **JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI**, the President of the United Republic of Tanzania officially declared Dodoma to become the City to be developed and administered by the Dodoma City Council;

AND WHEREAS consequent to the declaration of the City of Dodoma by His Excellency, **JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI**, the President of the United Republic of Tanzania, the Government has determined to establish and develop the City of Dodoma as the Capital City of the United Republic of Tanzania.

NOW THEREFORE, be it ENACTED by the Parliament of the United Republic of Tanzania as follows:

Short title	1. This Act may be cited as the Dodoma Capital City (Declaration) Act, 2018 and shall come into operation on such date as the Minister may, by order published in the <i>Gazette</i> , appoint.
Application	2. This Act shall apply to Mainland Tanzania as well as to Tanzania Zanzibar.
Interpretation	3. In this Act, unless the context otherwise requires- “Capital City” means the Dodoma Capital City as declared under this Act; “Minister” means the Minister responsible for local government.
Declaration of Capital City	4.- (1) The Dodoma City is hereby declared to be the Capital City of the United Republic of Tanzania. (2) The Parliament may enact a law for altering any provisions of this Act except that, any decision to alter declaration of the Capital City under this section shall be supported by the vote of not less than two thirds of all members of the Parliament. (3) The provisions of the Local Government (Urban Authorities) Act and other laws governing local government authorities shall, where appropriate, apply to the Capital City with necessary modifications.
Cap.288	5. Management, administration and other matters relating to the Capital City shall be expressly provided for in the law enacted by the Parliament.
Management of Capital City	6. The President may, by instrument published in the <i>Gazette</i> declare the boundaries of the Capital City.
Boundaries of Capital City	

OBJECT AND REASONS

This Bill proposes the enactment of the Capital City (Declaration) Act, 2018 with a view to declaring the City of Dodoma as the Capital City of the United Republic of Tanzania.

MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Tamko la Mji Mkuu ya mwaka 2018 kwa madhumuni ya kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Dodoma,
30 Agosti, 2018

SELEMAN S. JAFO
*Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na
Serikali za Mitaa*

SPIKA: Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati, anakuja Mwenyekiti mwenyewe. Karibu sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

MHE. JASSON S. RWEKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Muswada wa Sheria ya Tamko la Kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, utangulizi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Muswada wa Sheria ya Tamko la Kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza Serikali imewasilisha Bungeni Muswada unaokusudia kuwezesha kutungwa kwa Sheria ya Tamko la Makao Makuu ya nchi yetu, ambapo Jiji la Dodoma sasa litatangazwa kuititia sheria iliyotungwa na Bunge kuwa Makao Makuu. Hatua hii inakuja ikiwa ni takribani miaka 45 tangu muasisi wa Taifa hili, Hayati Mwalimu Nyerere alipotoa tamko la Serikali kuhamia Mjini Dodoma mnamo tarehe 1 Oktoba, 1973.

Mheshimiwa Spika, dhamira hiyo ya Serikali kuhamia Dodoma kutoka Dar es Salaam illendelea kuwepo katika awamu zote tatu za Serikali zilizofuatia na hatua kadhaa zilichukuliwa ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu ya Dodoma (*CDA*) na Wizara maalum ya Ustawishaji Makao Makuu kwa lengo la kuandaa mazingira wezeshi kwa Serikali kuhamia Dodoma. Hata hivyo, zoezi la kuhamia Dodoma halikutekelezwa kikamilifu kutokana na changamoto kadhaa ikiwamo vita vya Kagera mwaka 1978/1979, baa la njaa na kudorora kwa uchumi katika miaka ya 1980.

Mheshimiwa Spika, utashi wa kutekeleza dhamira ya kuhamia Dodoma umedhihirika katika Serikali ya Awamu ya Tano, kufuatia agizo alilolitoa Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli wakati wa maadhimisho ya kumbukumbu ya Mashujaa yaliyofanyika Kitaifa Mjini Dodoma tarehe 25 Julai, 2016 ambapo alisisitiza taasisi zote za Serikali kuhamia Dodoma kama ambavyo iliishatangazwa na Hayati Mwalimu Nyerere. Agizo la Mheshimiwa Rais na msisitizo wa mara kwa mara kutoka kwa Spika wa Bunge hili, Mheshimiwa Job Ndugai (Mb) kwamba sasa nchi yetu inahitaji Sheria ya Tamko la Makao Makuu vilisaidia kuwasilishwa Bungeni kwa Muswada wa Sheria ya Tamko la Kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Mwaka 2018, uliochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, Toleo Na. 2A, Juzu ya 99 la tarehe 7 Juni, 2018 na kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza tarehe 29 Juni, 2018 katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ikisomwa pamoja na Vifungu vya 6(4)(ii) na 7(1)(b), vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Muswada huu uliletwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa. Aidha, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati iliwaalika wadau mbalimbali ili waweze kufika mbele ya Kamati kwa lengo la kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu ili kuisaidia Kamati katika uchambuzi wake. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa wadau mbalimbali walifika mbele ya Kamati kwa nyakati tofauti na kuwasilisha maoni yao ambayo kwa sehemu kubwa yaliisaidia Kamati katika uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, mionganini mwa Wadau waliosasilisha maoni yao kwenye Kamati yetu ni hao wafuatao:-

(i) Chama cha Wanasheria Tanganyika (*Tanganyika Law Society*);

- (ii) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*Legal and Human Rights Centre*);
- (iii) Taasisi ya Twaweza;
- (iv) Chuo cha Mafunzo ya Serikali za Mitaa Hombolo; na
- (v) Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Spika, ili kufanya uchambuzi wenye tija na utakaowezesha kupatikana kwa mchango mzuri katika utungaji wa Sheria inayopendekezwa, Kamati ilifanya mapitio ya dhana kuu (*conceptual review*) katika sheria hiyo. Matokeo ya mapitio hayo yamedhihirisha kuwa dhana ya kutoa tamko rasmi kuhusu Makao Makuu au kuhamisha Makao Makuu si jambo geni duniani na Tanzania si nchi ya kwanza ambayo imefanya hivyo. Historia inaonesha kwamba katika karne ya 20 pekee zaidi ya nchi 10 zimehamisha Makao Makuu yake, ziliwamo, India (1991 – kutoka Kolkata kwenda New Delhi); Urusi (1918 – kutoka St. Petersburg kwenda Moscow); Malawi (1974 – kutoka Zomba kwenda Lilongwe); Nigeria (1991 – Lagos kwenda Abuja); na Brazil (1960 – kutoka Rio de Janeiro kwenda Brasilia).

Mheshimiwa Spika, Makao Makuu ya nchi ni muhimu sana kwa sababu ndiyo kielelezo na utambulisho mkuu wa Taifa lolote lile duniani. Mara nydingi mji yalipo Makao Makuu ndiyo kitovu cha shughuli za utawala, uchumi, historia na utamaduni wa nchi pamoja na elimu/taaluma. Ni kutokana na umuhimu wake huo pekee wakati mwengine vyombo ya habari vimekuwa vikitumia majina ya Makao Makuu kama mbadala wa majina ya nchi au mataifa husika. Kwa mfano, si jambo la ajabu kusikia vyombo vya habari vikisema, uhusiano baina ya Washington na Moscow vikimaanisha uhusiano baina ya Marekani na Urusi.

Mheshimiwa Spika, mfano tarehe 15 Januari, 2018 wakati akihojiwa na Shirika la BBC kuhusu iwapo uhusika wa Urusi katika vita vya Syria unaweza kuharibu mahusiano ya nchi hiyo na Marekani, Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Urusi, Maria Zakharovic alisikika akisema, na hapa ninanukuu, "... *Washington and Moscow could resolve their*

differences over Syria with better communication...”, akimaanisha kwamba, Marekani na Urusi zinaweza kutatua tofauti zao kuhusu Syria kwa kuwa na mawasiliano mazuri.

Mheshimiwa Spika, historia inaonesha kwamba, mionganoni mwa sababu zinazochangia kuhamisha Makao Makuu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine ni pamoja na sababu za kijiografia ambapo eneo la katikati ya nchi huzingatiwa. Nyingine ni kitovu cha shughuli za Serikali na kisiasa; shughuli za kidini; shughuli za kiuchumi; kitamaduni na kielimu. Aidha, Makao Makuu yanaweza kuhamishwa ili kuepuka msongamano (*overcrowding*) na kuleta muafaka baina ya miji inayogombea kuwa Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, ingawa suala la kutamka kuhusu Makao Makuu au kuhamisha Makao Makuu kutoka mji mmoja kwenda mwagine limeshuhudiwa katika nchi nyingi duniani, ni nchi chache sana ambazo zimetunga sheria ya tamko la kuhamisha Makao Makuu. Mfano ni nchi ya Nigeria, ambayo ina Sheria inayoitwa “*The Federal Territory Act, CAP.128 ya mwaka 1976*” ambayo inatamka kwamba, Abuja ndio Mji Mkuu wa Nigeria. Sheria hiyo mbali na kutamka Makao Makuu, ilianzisha Mamlaka ya Uendelezaji Makao Makuu. Nchi nyingine ni Malawi ambayo ilitunga Sheria Mwaka 1968 iliyoutambua Mji wa Lilongwe kuwa Makao Makuu ya Nchi ya Malawi na pia lilianzishwa Shirika la Uendelezaji Makao Makuu ya nchi.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika baadhi ya nchi hakukuwa na sheria inayotamka au kutambua Makao Makuu na badala yake viliundwa vyombo vya uendelezaji Makao Makuu kwa mujibu wa sheria za nchi husika. Mfano ni nchi ya Malaysia, ambayo iliunda Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu ilioitwa Putrajaya Corporation (PjC) chini ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kwa ajili ya uendelezaji wa eneo la Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, kwa historia hiyo, ni dhahiri Muswada wa Sheria ya Kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa

Mwaka 2018, uliletwa kwenye Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa ili kufanyiwa uchambuzi wa kitaalamu kwa lengo la kuuboresha na kutoa maoni yatakayosalidia Bunge kutunga Sheria ya Tamko la Makao Makuu inayokidhi viwango.

Mheshimiwa Spika, kusudio la pendekero la Serikali la kutungwa kwa Sheria ya Tamko la Kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaonekana katika madhumuni na sababu za Muswada huu, kwamba; ninanukuu:-

"Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Tamko la Makao Makuu ya Mwaka 2018 kwa madhumuni ya kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania". Mwisho wa nukuu.

Mheshimiwa Spika, kwa nukuu hiyo, kutungwa kwa sheria hii kumejikita katika kuwezesha kuwa na Tamko la kisheria kuhusu Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kitu ambacho kilikosekana kwa takribani miaka 45.

Mheshimiwa Spika, tarehe 21 Agosti, 2018, Kamati ilikutana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika Ukumbi wa Msekwa Duliopo Jengo la Msekwa kwa lengo la kupokea maelezo ya Serikali kuhusu Muswada husika. Aidha, tarehe 27 na 31 Agosti, 2018, Kamati ilikutana na Waziri kwa mara nyingine katika vikao vya mashauriano kuhusu hoja zilizoibuliwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Muswada. Kamati ilifanya uchambuzi wa Muswada ili kutoa maoni ambayo yanaweza kuzingatiwa kwa lengo la kuuboresha ili kuwezesha kutungwa kwa sheria bora inayopendekezwa. Muswada huu una Ibara Sita (6) ambazo zimefanuliwa kama ifuatavyo:-

(a) Ibara ya 1 inahusu jina la Muswada ambalo ni *"The Dodoma Capital City (Declaration) Act, 2018"* na tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hii ambayo ni ile

itakayotangazwa kwenye Gazeti la Serikali na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

(b) Ibara ya 2 inahusu matumizi ya sheria ambapo sheria hii itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

(c) Ibara ya 3 inaainisha tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Muswada.

(d) Ibara ya 4 inalitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Ibara ya 4(2) inaweka masharti ya kubadili tamko hili kwamba, ni lazima kuungwa mkono kwa kura za Wabunge wasiopungua theluthi mbili ($\frac{2}{3}$) ya Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano. Vilevile Ibara ya 4(3) inaainisha kwamba, utungaji wowote wa sheria zitakazotumika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa utazingatia sheria hii pamoja na marekebisho yatakayofanyika.

(e) Ibara ya 5 bila kuathiri Ibara ya 4 inaeleza kuwa uanzishwaji wa Makao Makuu unaweza kufanyika kwa mujibu wa Katiba na sheria nyingine za nchi.

(f) Ibara ya 6 inaeleza kuwa mipaka ya Makao Makuu itakuwa kama ilivyofafanuliwa katika sheria husika (*relevant laws*).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa Muswada huu kwa kuzingatia maelezo na hoja za Serikali zilizowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuhusu vifungu vya Muswada huu, hoja za wadau mbalimbali na kufanya tathmini ya uchambuzi, ili kuliwezesha Bunge kutunga sheria bora ya Tamko la Kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa Muswada huu yamebainisha mambo yafuatayo:-

(i) Sheria hii itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

(ii) Wadau wanaunga mkono kutungwa kwa sheria hii, hata hivyo baadhi wanafikiri sheria ingegusa na maeneo mengine kama vile mipaka na namna ya kuendeleza Makao Makuu.

(iii) Zilikuwepo Ibara za Muswada zilizohitaji kuandikwa upya ili kuleta maana na kuendana na dhamira nzuri ya sheria hii iliyopendekezwa. Baada ya mashauriano na Serikali na Mheshimiwa Waziri ibara hizi ziliandikwa upya, kama inavyoonekana katika Muswada uliochapichwa upya (*reprint*).

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matokeo hayo, Serikali ilikubali mapendekezo yote ya Kamati kuhusu Muswada huu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Baada ya maelezo hayo, naomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu, ambayo yanatokana na mapitio ya historia ya dhana ya Tamko la Makao Makuu na kuhamisha Makao Makuu, pamoja na uchambuzi wa vifungu vya Muswada kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipendekeza kwamba, neno "and" lililokuwepo baada ya maneno "*Mainland Tanzania*" na kabla ya neno "as" katika Ibara ya 1 lifutwe kwa sababu halikuwa na maana yoyote katika Ibara hiyo. Kufutwa kwa neno hili kumeifanya Ibara hiyo isomeke ifuatavyo: "*This Act shall apply in Mainland Tanzania as well as Tanzania Zanzibar*".

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 3 ya Muswada Kamati inapendekeza herufi za mwanzo za maneno "*capital city*" yaliyo katika alama za nukuu ziwe kubwa kwa sababu hayo ni majina.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 4(2) Kifungu kidogo cha (7) kinachorejewa hakikuwepo, hivyo Kamati ilishauri kwamba, kifungu hicho kifutwe na badala yake kiwekwe kifungu kidogo cha (1) ambacho kililetwa maana iliyokusudiwa. Kamati ilibaini kwamba, hayo yalikuwa ni makosa ya uchapaji na ambayo yalirekebishwa kama ilivyoshauriwa na ibara hii ikaleta maana nzuri.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipendekeza kuandikwa upya kwa Ibara ya 4(3) kwani ilikuwa haieleweki. Ibara hiyo ilikuwa inasomeka ifuatavyo:-

"Any enactment that applies to the Local Government Authorities shall, subject to the provisions of this Act and with the necessary modifications."

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipendekeza Ibara hiyo isomeke hivi:-

"The provisions of the Local Government Urban Authorities Act and other laws governing the local government authority shall, where appropriate, apply to the Capital City with necessary modifications."

Mheshimiwa Spika, pendekezo hilo lilizingatiwa kama inavyoonekena kwenye *reprints*.

Mheshimiwa Spika, majadiliano ya mwisho na Serikali yaliwezesha makubaliano kuhusu masuala mbalimbali yaliyoibuliwa na Kamati kuhusu Ibara husika hapo juu. Serikali ilikubaliana na maoni na mapendekezo ya Kamati, hivyo, kuja na Jedwali la Marekebisho kama liliivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ibara ya 1 ya Muswada inayohusu kuanza kutumika kwa sheria iliyopendekezwa, Kamati inashauri kuwa ni vema Waziri mwenye dhamana, akatangaza mapema iwezekanavyo kwenye Gazeti la Serikali, ili kuwezesha sheria hii kuanza kutumika haraka. Msingi wa maoni hayo ni kuwa pamoja na dhamira nzuri ya Serikali, mchakato huu umecheleweshwa kukamilika kwa takribani miaka 45, hivyo sasa ni wakati mwafaka wa sheria hiyo ya Tamko la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi ikaanza kutumika mapema.

Mheshimiwa Spika, mbali na maoni yaliyotolewa kuhusu Ibara za Muswada zilizotajwa, Kamati pia ina maoni na ushauri wa jumla. Jambo kubwa katika hili ni uzoefu kutoka nchi nyingine (*other jurisdictions*) uliojitekeza katika

mapitio na machapisho mbalimbali. Uzoefu huo umeonesha kwamba, nchi zilizotunga Sheria ya Tamko la Makao Makuu au Kuhamisha Makao Makuu zilifanikisha azma hiyo kwa kipindi kifupi zaidi ya kile kilichotengwa kwenye sheria, ikilinganishwa na nchi ambazo hazikutunga sheria kwanza. Mfano ni nchi ya Nigeria ambayo ilitekeleza uamuzi wa kuhamisha Makao Makuu kutoka Lagos kwenda Abuja ndani ya miaka 16 badala ya miaka 20 iliyokuwa kwenye sheria.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Kwa mara nyingine tena naomba kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati nikushukuru sana wewe mwenyewe binafsi kwanza, kwa msisitizo ulioutoa kwa Serikali kuhakikisha inawasilisha Bungeni Muswada wa Kutunga Sheria ya Tamko la Kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu, lakini pia kutoa kibali, ili Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, iweze kuushughullikia Muswada huu kwa kufanya uchambuzi wa kina na hatimaye kuwasilisha maoni yake mbele ya Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda niwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano wao mkubwa walionipatia wakati wote wa kushughulikia Muswada huu. Weledi na umahiri waliouonesha wakati wa uchambuzi ndiyo ilikuwa chachu ya kutoa mapendekezo haya ya msingi ya kuboresha Muswada huu. Wajumbe hawa na Bunge lako Tukufu kwa ujumla, tunaingia katika historia ya nchi yetu kwa kuwezesha kutungwa kwa Sheria ya Bunge ya Tamko la Makao Makuu ya Nchi yetu, jambo ambalo halikuweza kufanyika kwa kipindi cha zaidi ya miongo minne. Ni dhahiri shahiri kuwa kazi hii waliyoifanya Wajumbe wa Kamati na watakayofanya Wabunge wote itakuwa kumbukumbu isiyosahaulika kutoka kizazi hiki hadi kizazi kingine kwa kadri nchi yetu itakavyodumu katika ulmwengu huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutambua kwa majina ya Wajumbe kama ifuatavyo: Mhe. Jasson Samson Rweikiza - Mwenyekiti na Mhe. Mwanne Ismail Mchemba - Makamu Mwenyekiti. Wajumbe ni Mheshimiwa Angelina Adam

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Malembeka ; Mheshimiwa Anna Joram Gidarya; Mheshimiwa George Malima Lubeleje; Mheshimiwa Hamad Salim Maalim; Mheshimiwa Mhe.Jerome Dismas Bwanausi; Mheshimiwa Innocent Bilakwate; Mheshimiwa Martha Mosses Mlata; Mheshimiwa Margareth Simwanza Sitta; Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali; Mheshimiwa Mwantum Dau Haji; Mheshimiwa Philipo Augustino Mulugo; Mheshimiwa Saada Mkuya Salum; Mheshimiwa Venance Methusela Mwamoto; Mheshimiwa Khamis Salum Salim; Mheshimiwa Lucia Ursula Michael; Mheshimiwa Rehema Juma Migilla; Mheshimiwa Joseph Roman Selasini; Mheshimiwa Joel Mwaka Makanya; Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga; Mheshimiwa Khatib Said Haji; na Mheshimiwa Daniel Edward Mtuka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia, kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Selement Said Jafo, Wasaidizi wake, Naibu Mawaziri, Mheshimiwa George Joseph Kakunda na Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Watendaji wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maelezo na ufanuzi wa kina walioutoa mbele ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Tamko la Kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nawashukuru wadau mbalimbali ambao walitoa maoni yao katika uchambuzi wa Muswada huu, ambayo yamesaidia kwa kiasi kikubwa katika kuboresha Muswada huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai, kwa ushirikiano wake ulioiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. Vilevile namshukuru Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Angelina Sanga, Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Kamati, kwa usimamizi mzuri wa shughuli za Kamati. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu wake, nawatambua na kuwashukuru Makatibu wa Kamati Ndugu Chacha Timasi Nyakega, Ndugu Eunike Donati Shirima, Ndugu Victor Leonard Mhagama na Msaidizi wa Kamati

Ndugu Modesta Kipiko, kwa msaada mkubwa sana kwa Kamati katika kutekeleza majukumu yake ya taarifa hii. Aidha, nawashukuru Washauri wa Mambo ya Sheria wa Bunge, Ndugu Prudence Rweyongeza na Ndugu Hawa Manzurya kwa kuisaidia Kamati katika uchambuzi wa kisheria wa Muswada na Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge kwa kusaidia kuchapisha vitabu vya Taarifa hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. (*Makof*)

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA
UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU MUSWADA WA
SHERIA YA TAMKO LA JIJI LA DODOMA KUWA MAKAO
MAKUU YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WA
MWAKA 2018 (*THE DODOMA CAPITAL CITY (DECLARATION)
BILL, 2018*] – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu Muswada wa Sheria ya Tamko la Kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Mwaka 2018 [*The Dodoma Capital City (Declaration) Bill, 2018*].

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza Serikali imewasilisha Bungeni Muswada unaokusudia kuwezesha kutungwa kwa Sheria ya Tamko la Makao Makuu ya nchi yetu, ambapo Jiji la Dodoma sasa litatangazwa kupitia Sheria iliyotungwa na Bunge kuwa Makao Makuu. Hatua hii inakuja ikiwa ni takribani miaka 45 tangu Mwasisi wa Taifa letu, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipotoa tamko la Serikali kuhamia Mjini Dodoma mnamo tarehe 1 Oktoba, Mwaka 1973.

Dhamira hiyo ya Serikali kuhamia Dodoma kutoka Dar es Salaam iliendelea kuwepo katika Awamu zote tatu za Serikali zilizofuatia na hatua kadhaa zilichukuliwa ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu ya Dodoma (*Capital Development Authority - CDA*) mwaka 1973 na Wizara Maalum ya Ustawishaji Makao Makuu kwa lengo la kuandaa mazingira wezeshi kwa Serikali kuhamia Dodoma. Hata hivyo zoezi la kuhamia Dodoma halikutekelezeka kikamilifu kutohana na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na Vita ya Kagera mwaka 1978/1979, Baa la Njaa na kudorora kwa uchumi katika miaka ya 1980.

Mheshimiwa Spika, utashi wa kutekeleza dhamira ya kuhamia Dodoma umedhihirika katika Serikali ya Awamu ya Tano, kufuatia agizo alilolitoa Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli wakati wa Maadhimisho ya Kumbukumbu ya Mashujaa yaliyofanyika kitaifa MJINI Dodoma tarehe 25 Julai, 2016 ambapo alisisitiza Taasisi zote za Serikali kuhamia Dodoma kama ambavyo iliishatangazwa na Mwalimu J.K. Nyerere kuwa Dodoma ndiyo Makao Makuu ya Nchi.

Agizo la Mheshimiwa Rais, na msisitizo wa mara kwa mara kutoka kwa Spika wa Bunge hili, Mheshimiwa Job Ndugai (Mb) kwamba, sasa nchi yetu inahitaji Sheria ya Tamko la Makao Makuu vilisaidia kuwasilishwa Bungeni kwa Muswada wa Sheria ya Tamko la Kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Mwaka 2018, uliochapishwa kwenye Gazeti Maalum la Serikali, Toleo Na.2A, Juzu ya 99 la tarehe 7 Juni, 2018 na kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza tarehe 29 Juni, 2018 katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ikisomwa pamoja na Vifungu vya 6 (4) (ii) na 7(1) (b), vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Muswada huu uliletwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa. Aidha, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati iliwaalika

Wadau mbalimbali ili waweze kufika mbele ya Kamati kwa lengo la kutoa maoni kuhusu Muswada huu ili kuisaidia Kamati katika uchambuzi wake.

Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wadau mbalimbali walifika mbele ya Kamati kwa nyakati tofauti na kuwasilisha maoni yao ambayo kwa sehemu kubwa yaliisaidia Kamati katika uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, mionganini mwa Wadau waliowasilisha maoni yao kwenye Kamati kuhusu Muswada huu ni pamoja:-

- i) Chama cha Wanasheria Tanganyika (Tanganyika Law Society);
- ii) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (Legal and Human Rights Centre);
- iii) Taasisi ya Twaweza;
- iv) Chuo cha Mafunzo ya Serikali za Mitaa (LGTI) Hombolo; na
- v) Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Spika, ili kufanya uchambuzi wenyewe tija na utakaowezesha kupatikana kwa mchango mzuri katika utungaji wa Sheria inayopendekezwa, Kamati ilifanya mapitio ya Dhana Kuu (Conceptual Review) katika Sheria hiyo. Matokeo ya mapitio hayo yamedhihirisha kuwa dhana ya kutoa tamko rasmi kuhusu Makao Makuu au kuhamisha Makao Makuu siyo jambo geni duniani, na Tanzania siyo nchi pekee ambayo imefanya hivyo. Historia inaonesha kwamba katika karne ya 20 pekee zaidi ya nchi 10 zimehamisha Makao Makuu yake, zikiwamo:-

- i. India (1991 – kutoka Kalkata kwenda New Delhi);
- ii. Urusi (1918 – kutoka St. Petersburg kwenda Moscow);
- iii. Malawi (1974 – kutoka Zomba kwenda Lilongwe);
- iv. Nigeria (1991 – Lagos kwenda Abuja); na
- v. Brazil (1960 – kutoka Rio de Janeiro kwenda Brasilia).

Mheshimiwa Spika, Makao Makuu ya nchi ni muhimu sana kwa sababu ndiyo kielelezo au utambulisho mkuu wa taifa lolote lile duniani. Mara nyingi mji yalipo Makao Makuu ndiyo kitovu cha shughuli za utawala, uchumi, historia na utamaduni wa nchi pamoja na elimu/taaluma.

Ni kutokana na umuhimu wake huo wakati mwingine vyombo ya habari vimeduwa vikitumia majina ya Makao Makuu kama mbadala wa majina ya nchi au mataifa husika. Mfano, sijambo la ajabu kusikia vyombo vya habari vikisema, "uhusiano baina ya Washington na Moscow" vikimaanisha "uhusiano baina ya Marekani na Urusi".

Mfano tarehe 15 Januari, 2018 wakati akihojiwa na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) kuhusu iwapo uhusika wa Urusi katika vita inayoendelea nchini Syria unaweza kuharibu uhusiano wa nchi hiyo na Marekani, Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Urusi, Maria Zakharovic alisikika akisema na hapa ninanukuu "... *Washington and Moscow could resolve their differences over Syria with better communication...*", akimaanisha kwamba, Marekani na Urusi zinaweza kutatua tofauti zao kuhusu Syria kwa kuwa na mawasiliano mazuri.

Mheshimiwa Spika, historia inaonesha kwamba, mionganoni mwa sababu zinazochangia kuhamisha Makao Makuu kutoka sehemu moja kwenda nyingine ni pamoja sababu za kijirografia ambapo eneo la katikati ya nchi huzingatiwa. Nyingine ni kitovu cha shughuli za kiserikali na kisiasa, shughuli za kidini, shughuli za kiuchumi, kitamaduni na kielimu. Aidha, Makao Makuu yanaweza kuhamishwa ili kuepuka msongamano (*overcrowding*) na kuleta mwafaka baina ya miji inayogombea kuwa Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, ingawa suala la kutamka kuhusu Makao Makuu au kuhamisha Makao Makuu kutoka mji mmoja kwenda mwingine limeshuhudiwa katika nchi kadhaa duniani, ni nchi chache sana ndiyo zilitunga sheria ya tamko au kuhamisha Makao Makuu. Mfano ni nchi ya Nigeria, ambayo ina Sheria ya Mji "The Federal Territory Act,

CAP.128" ya mwaka 1976 ambayo inatamka kwamba, Abuja ndiyo Mji Mkuu wa Nigeria. Sheria hiyo mbali na kutamka Makao Makuu, ilianzisha Mamlaka ya Uendelezaji Makao Makuu.

Nchi nyingine ni Malawi ambayo ilitunga Sheria Mwaka 1968 iliyoutambua Mji wa Lilongwe kuwa Makao Makuu ya Nchi ya Malawi, na pia ilianzisha Shirika la Uendelezaji Makao Makuu ya Nchi.

Aidha, katika baadhi ya nchi hakukuwa na sheria inayotamka au kutambua Makao Makuu na badala yake viliundwa vyombo yya uendelezaji Makao Makuu kwa mujibu wa sheria za nchi husika. Mfano ni nchi ya Malaysia, ambayo iliunda Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu iliyoitwa Putrajaya Corporation (PjC) chini ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kwa ajili ya uendelezaji wa eneo la Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, kwa historia hiyo, ni dhahiri Muswada wa Sheria ya Kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Mwaka 2018, uliletwa kwenye Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa ili kufanyiwa uchambuzi wa kitaalamu kwa lengo la kuuboresha na kutoa maoni yatakayosalidia Bunge kutunga Sheria ya Tamko la Makao Makuu inayokidhi viwango.

Mheshimiwa Spika, kusudio la pendekeso la Serikali la kutungwa kwa Sheria ya Tamko la Kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, linaonekana katika madhumuni na sababu za Muswada huu kwamba:

Nukuu:" Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Tamko la Makao Makuu ya Mwaka 2018 kwa madhumuni ya kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania" ". **Mwisho wa nukuu.**

Kwa nukuu hiyo, kutungwa kwa sheria hii kumejikita katika kuwezesha kuwa na Tamko la kisheria kuhusu Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kitu ambacho kilikosekana kwa takribani miaka 45.

Mheshimiwa Spika, tarehe 21 Agosti, 2018 Kamati ilikutana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika Ukumbi wa Msekwa D uliopo Jengo la Msekwa kwa lengo la kupokea maelezo ya Serikali kuhusu Muswada husika. Aidha, tarehe 27 na 31 Agosti, 2018 Kamati ilikutana na Waziri kwa mara nyingine katika vikao vya mashauriano kuhusu hoja zilizoibuliwa na Kamati.

2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa Muswada ili kutoa maoni ambayo yanaweza kuzingatiwa kwa lengo la kuuboresha ili kuwezesha kutungwa kwa sheria bora inayopendekezwa. Muswada huu una Ibara Sita (6) ambazo zimefafanuliwa kama ifuatavyo:-

(a) Ibara ya kwanza (1) inahusu jina la Muswada ambalo ni "The Dodoma Capital City (Declaration) Act, 2018 na tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hii ambayo ni ile itakayotangazwa kwenye Gazeti la Serikali na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa;

(b) Ibara ya pili (2) inahusu matumizi ya sheria ambapo sheria hii itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar;

(c) Ibara ya Tatu (3) inaainisha tafsiri ya maneno mbalimbali yalijotumika katika Muswada;

(d) Ibara ya Nne (4) inalitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Ibara ya 4(2) inaweka masharti ya kubadili tamko hili kwamba, ni lazima kuungwa mkono kwa kura za Wabunge wasiopungua theluthi mbili (2/3) ya Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano. Vilevile Ibara ya 4(3) inaainisha kwamba, utungaji wowote wa sheria zitakazotumika katika mamlaka za Serikali za Mitaa utazingatia sheria hii pamoa na marekebisho yatakayofanyika;

(e) Ibara ya Tano (5) bila kuathiri Ibara ya Nne (4) inaeleza kuwa uanzishwaji wa Makao Makuu unaweza kufanyaika kwa mujibu wa Katiba na Sheria nyingine; na

(f) Ibara ya Sita (6) inaeleza kuwa mipaka ya Makao Makuu itakuwa kama ilivyofafanuliwa katika Sheria husika (relevant laws).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa Muswada huu kwa kuzingatia maelezo na hoja za Serikali zilizowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kuhusu vifungu vya Muswada huu, hoja za Wadau mbalimbali na kufanya tathmini ya uchambuzi ili kuliwezesha Bunge kutunga Sheria bora ya Tamko la Kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa Muswada huu yamebainisha mambo yafuatayo:-

- i) Sheria hii itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar;
- ii) Wadau wanaunga mkono kutungwa kwa Sheria hii, hata hivyo baadhi wanafikiri sheria ingegusa na maeneo mengine kama vile mipaka na namna ya kuendeleza Makao Makuu;
- iii) Kuna makosa ya kiuchapaji (typos); na
- iv) Zipo Ibara za Muswada zinahitaji kuandikwa upya ili kuleta maana na kuendana na dhamira nzuri ya Sheria hii inayopendekezwa.

Kwa kuzingatia matokeo hayo, Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Serikali na kukubaliana ambapo Serikali ilikubali mapendekezo yote ya Kamati kuhusu Muswada huu wa Sheria.

3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu, ambavyo vinatokana na mapitio ya historia ya dhana ya tamko la Makao Makuu na kuhamisha

Makao Makuu, pamoja na uchambuzi wa Vifungu vya Muswada kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwamba, neno “**and**” liliopo baada ya maneno “**Mainland Tanzania**” na kabla ya neno “**as**” katika Ibara ya Kwanza lifutwe kwa sababu halina maana yoyote katika Ibara hiyo.

Kufutwa kwa neno hilo kutaifanya Ibara hiyo kusomeka ifuatavyo:-

1. *“This Act shall apply in Mainland Tanzania as well as Tanzania Zanzibar”*

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya Tatu (3) ya Muswada Kamati inapendekeza herufi za mwanzo za maneno “**capital city**” yaliyo katika alama za nukuu ziwe kubwa kwa sababu hayo ni majina.

Katika Ibara ya 4(2) ***Kifungu kidogo cha*** (7) kinachorejewa hakipo hivyo, hivyo Kamati inashauri kwamba kifungu hicho kifutwe na badala yake kiwekwe ***kifungu kidogo cha*** (1) ambacho kitaleta maana inayokusudiwa. Kamati inadhani kwamba, hayo ni makosa ya kiuchapaji na ambayo yakirekebishwa kama ilivyoshauriwa ibara hii italeta maana.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kuandikwa upya kwa Ibara ya 4(3) kwani haieleweki. Ibara hiyo inasomeka ifuatavyo:-

“Any enactment that applies to the Local Government Authorities shall, subject to the provisions of this Act and with the necessary modifications.”

Mheshimiwa Spika, majadiliano ya mwisho na Serikali yaliwezesha makubaliano kuhusu masuala mbalimbali yaliyoibuliwa na Kamati kuhusu Ibara husika hapo juu. Serikali ilikubaliana na maoni na mapendekezo ya Kamati, hivyo,

kuja na Jedwali la marekebisho kama liliwyowasilishwa namtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ibara ya 1 ya Muswada inayohusu kuanza kutumika kwa Sheria inayopendekezwa, Kamati inashauri kuwa ni vema Waziri mwenye dhamana, akatangaza mapema iwezekanavyo katika Gazeti la Serikali, ili kuwezesha Sheria hii kuanza kutumika haraka. Msingi wa maoni hayo ni kuwa pamoja na dhamira nzuri ya Serikali, mchakato huu umechelewa kukamilika kwa takribani miaka arobaini na tano (45), hivyo sasa ni wakati mwafaka wa Sheria ya Tamko la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi ikaanza kutumika mapema.

Mheshimiwa Spika, mbali na maoni yaliyotolewa kuhusu Ibara za Muswada nilizozitaja, Kamati pia ina maoni na ushauri wa jumla. Jambo kubwa katika hili ni uzoefu kutoka nchi nyingine (*Other Jurisdictions*) ulojitokeza katika mapitio ya machapishombalimbali. Uzoefu huo umeonesha kwamba, nchi zilizotunga Sheria ya Tamko la Makao Makuu au Kuhamisha Makao Makuu zilifanikisha azma hiyo kwa kipindi kifupi zaidi ya kile kilichotengwa kwenye Sheria, ikilinganishwa na nchi ambazo hazikutunga sheria kwanza. Mfano ni nchi ya Nigeria ambayo ilitekeleza uamuzi wa kuhamisha Makao Makuu kutoka Lagos kwenda Abuja ndani ya miaka 16 badala ya miaka 20 iliyokuwa imetamkwa kwenye Sheria.

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena naomba kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati nikushukuru sana wewe binafsi kwanza, kwa msisisitizo ulioutoa kwa Serikali kuhakikisha inawasilisha Bungeni Muswada wa Kutunga Sheria ya Tamko la Kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu, lakini pia kutoa kibali ili Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, iweze kuushughulikia Muswada huu kwa kufanya uchambuzi wa kina na hatimaye kuwasilisha maoni yake mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa napenda niwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano wao mkubwa walionipatia wakati wote wa kushughulikia Muswada huu. Weledi na umahiri waliouonesha wakati wa uchambuzi ndiyo ilikuwa chachu ya kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha Muswada huu.

Wajumbe hawa na Bunge lako Tukufu kwa ujumla, tunaingia katika historia ya nchi yetu kwa kuwezesha kutungwa kwa Sheria ya Bunge ya Tamko la Makao Makuu ya nchi yetu, jambo ambalo halikuweza kufanyika kwa kipindi cha zaidi ya miongo minne. Ni dhahiri shahiri kuwa, kazi hii waliyoifanya Wajumbe wa Kamati na watakayoifanya Wabunge wote itakuwa kumbukumbu isiyosahaulika kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa kadri nchi yetu itakavyodumu kuwepo katika Ulimwengu huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutambua majina ya Wajumbe hao wa Kamati kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Jasson Samson Rweikiza, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Mwanne Ismail Mchemba, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Angelina Adam Malembeka, Mb- Mjumbe
4. Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb - Mjumbe
5. Mhe. George Malima Lubeleje, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Hamad Salim Maalim, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Jerome Dismas Bwanausi, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Innocent Sebba Bilakwate, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Martha Mosses Mlata, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Margareth Simwanza Sitta, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Hamidu Hassan Bobali, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Mwantum Dau Haji, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Saada Mkuya Salum, Mb – Mjumbe
15. Mhe. Venance Methusela Mwamoto, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Khamis Salum Salim, Mb – Mjumbe
17. Mhe. Lusia Ursula Michael, Mb – Mjumbe
18. Mhe. Rehema Juma Migilla, Mb – Mjumbe
19. Mhe. Joseph Roman Selasini, Mb – Mjumbe
20. Mhe. Joel Mwaka Makanya, Mb – Mjumbe

21. Mhe. Njalu Daudi Silanga, Mb –	Mjumbe
22. Mhe. Khatib Said Haji, Mb –	Mjumbe
23. Mhe. Daniel Edward Mtuka, Mb –	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Suleiman Said Jafo (Mb), Wasaidizi wake Mhe. George Joseph Kakunda (Mb) na Mhe. Josephat Sinkamba Kandege (Mb), Watendaji wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa maelezo na ufanuzi wa kina walioutoa mbele ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Tamko la Kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wa Mwaka 2018.

Aidha, nawashukuru Wadau mbalimbali ambao walitua maoni yao katika uchambuzi wa Muswada huu, ambayo yamesaidia kwa kiasi kikubwa katika kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, kwa ushirikiano wake ulioiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. Vilevile, namshukuru Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, na Ndg. Angelina Sanga, Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Kamati, kwa usimamizi mzuri wa shughuli za Kamati.

Mwisho lakini si kwa umuhimu wake, nawatambua na kuwashukuru Makatibu wa Kamati Ndg. Chacha Timasi Nyakega, Ndg. Eunike Donati Shirima, Ndg. Victor Leonard Mhagama na Msaidizi wa Kamati Ndg. Modesta Kipiko, kwa msaada mkubwa sana kwa Kamati katika kutekeleza shughuli zake hadi kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru Washauri wa Mambo ya Sheria wa Bunge, Ndg. Prudence Rweyongeza na Ndg. Hawa Manzurya kwa kuisaidia Kamati katika uchambuzi wa kisheria wa Muswada, na Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge kwa kusaidia kuchapisha vitabu vya Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Jasson S. Rweikiza (Mb)

MWENYEKITI

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA
NA SERIKALI ZA MITAA**

4 Septemba, 2018

SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa. Tunakushukuru sana. (*Makofii*)

Sasa nimuite Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu TAMISEMI. Ni muda mrefu hatujawahi kupata maoni ya Kambi ya Upinzani, ngoja tuone leo mwanzo unakwendaje. Karibu Mheshimiwa. (*Makofii*)

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu Muswada wa Sheria ya Kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa maoni hayo, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutujalia sote uhai, lakini zaidi sana kuendelea kutujalia moyo wa ujasiri na uvumilivu hasa sisi Wabunge wa Upinzani ambao kwa kipindi kirefu sana tumepitia majaribu makubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, si nia yangu kuelezea kwa undani hujuma zinazofanywa hivi sasa kwa wapinzani nchini, ila ni kusudio langu kutoa angalizo kwa Serikali iliyo kujua, kwamba tusifanye mzaha wala mchezo na amani tuliyonayo hivi sasa. Pengine hivi sasa hatuoni umuhimu wa amani

tuliyonayo, lakini baadaye tutakuja kujua ni jinsi gani hatukusimamia haki na kuleta vurugu katika taifa hili kwa kutokufuata mfumo wa sheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimelazimika kuanza kwa maneno haya kwa kuwa vitendo vya hila vinyavofanywa sasa hivi na kuwarubuni na kuwanunua viongozi wa vyama vya upinzani na kuuhadaa umma kwamba viongozi hao wanaunga juhudzi za Serikali ya Awamu ya Tano...

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA): Hii si sawa kwa sisi wapinzani.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Kuhusu Utaratibu.

SPIKA: Mheshimiwa naomba usimame kidogo, naomba ukae. Mheshimiwa Waziri wa Nchi nilikuona.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza labda nianze kwa kuishukuru Kambi ya Upinzani kwa sababu sasa hivi wameendelea kufuata utaratibu kwa kutoa hotuba zao mapema na sisi tunapata nafasi ya kuzisoma na kujua kama zimefuata muktadha wa Kanuni zinazoendesha Bunge.

Mheshimiwa Spika, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(1) ya Kuhusu Utaratibu na utaratibu nitakaouzungumza unatokana na Kanuni ya 64(1)(a),(b) na (c). Kifungu (a) kinazungumzia utaratibu wa kusema ukweli Bungeni. Kifungu cha (b) kinazungumzia kutokujadili ndani ya Bunge suala ambalo halijawekwa Mezani kama ndiyo suala la mjadala

wa leo na kifungu cha (c) kinazungumzia jambo ambalo lilikwisha kuamuliwa na mikutano iliyopita. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema msingi wa hoja yangu ya utaratibu, sasa nakwenda kwenye maeneo ambayo mzungumzaji wa Kambi ya Upinzani, nakuomba unisaidie utaratibu huo kama unavunjwa ni jambo gani linaweza likafanywa. Katika kifungu hicho ambacho ameanza kukisema akiituhumu Serikali na viongozi mbalimbali kwamba wamekuwa wakifanya biashara ya kununua viongozi wa vyama nya upinzani lakini jambo hilo linajirudia tena kwenye *paragraph* ya tatu kwenye *page* hiyo ya pili na linajirudia pia kwenye *paragraph* ya kwanza kwenye *page* ya tatu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nianze na hilo. Katika mtizamo na uelewa wangu na uelewa mpana wa Serikali toka chaguzi hizi ndogo zimeanza si msomaji wa taarifa wala chama chake wala mtu ye yeyote aliyewahi kufungua shitaka lolote katika Mahakama yoyote akimtuhumu kiongozi yoyote aliyeondoka kwenye chama cha upinzani kwa sababu amenunuliwa. Kwa hiyo, kama jambo hili halijathibitika kulileta hapa ndani ya Bunge ni kukiuka Kanuni yetu ya 64(1). Jambo hili ni uwongo uliokithiri na ambao hauwezi kuvumilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili nilisema kanuni ndogo ile ya (b) inasema ni lazima jambo linaloendelea Bungeni liwe linahusu mjadala uliopo. Mjadala huu ni Sheria inayohusu Tamko la Makao Makuu ya Nchi na si shughuli za uchaguzi zinazoendelea ndani ya nchi yetu, kwa hiyo huko ni kukiuka kanuni. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini Kanuni ya (c) inasema, kama jambo lilikwishakutolewa uamuza, jambo hili limeshazungumzwa sana ndani ya Bunge hili na lilikwisha kutolewa uamuza kwa hiyo, linakiuka utaratibu wa kikanuni.

Mheshimiwa Spika, pia ukienda pia kwenye ukurasa wa hotuba hii, nisipoteze tu muda wa Bunge lako, ukurasa wa nne ziko pia tu huma zinazoeleza kwamba, Serikali

ilipotamka Dodoma kuwa Jiji ilivunja sheria. Naomba nirudi pale pale kwenye msingi wa Kanuni ya 64(b), hoja hii inayozungumzwa hapa mbele ni ya Tamko la Makao Makuu ya Nchi na sio Tamko la Dodoma kuwa Jiji.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Kwa hiyo, hii pia ni uvunjifu wa kanuni.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu. Usichambue hotuba wengine hatujaisikiliza bwana.

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Spika, lakini pia Kanuni ndogo ya 64(c), jambo hili la Dodoma kuwa Jiji lilishatolewa maelezo ndani ya Bunge hili kwenye Mkutano uliopita na lilishafanyiwa maamuzi. Kwa hiyo, kulirudisha kwenye hoja hii leo ni ukiukwaji wa kanuni.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa
Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Spika, naomba kuweka utaratibu huu mbele ya Kiti chako ili tuweze kujua kama hoja hii na hotuba hii katika vifungu hivi vina haki ya kuendelea ama havina haki ya kuendelea kusomwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Sophia ningeomba uanze kwa kujaribu ku-react na uliyoambiwa, nafikiri umesikia yote uliyoelezwa, unasemaje kuhusu hayo uliyoambiwa, karibu hapa mbele.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO A NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Spika, hotuba hii ni Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani na si hotuba ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikijiendeleza kujikita na kuendelea na hotuba yetu ya Kambi Rasmi ya Upinzani, si kila jambo...

SPIKA: Mheshimiwa Sophia...

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO A NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Spika, ndio.

SPIKA: Hii hotuba ni ya Msemaji Mkuu na kwa maana hiyo Msemaji Mkuu ni wewe, sio ya Kambi ni ya Msemaji Mkuu. Sasa mambo yaliyozungumzwa hapa ni mambo ya msingi hatuvezi kuyadharau, inatakiwa kwa kweli tujielekeze kwa kilicho Mezani. Kilichoko Mezani si uchaguzi unaoendelea, kilichoko mezani si nani kanunuliwa sijui kamnunua nani, vitu ambavyo tukisema twende maadili huko uende ukathibitishie nani alipewa shilingi ngapi, wapi na kadhalika itakuwa hatujitendei haki. Kwa hiyo, mtaona mmefungua *pandora* na kuanza kwenda kwenye *unchanted waters* ambazo yaani ni vigumu ku-*substantiate*. Hii hotuba ilivyo, hata ukiitazama huku mbele sijui utasoma kitu gani ambacho kitapita salama, yaani sioni, labda twende kidogo ili uweze kujithibitishia mwenywewe.

Mheshimiwa Spika, twende, lakini nakuomba mambo ambayo yanaenda kinyume na kanuni ujaribu kuyaruka. Habari ya nani kamununua nani, *unless* una ushahidi endelea nayo na mimi baada ya kumaliza hii shughuli tutakupeleka kwa wenzako kule upeleke ushahidi wako. Hatupendi sana mambo ya kuzushazusha hivi, karibu. (*Makofii*)

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Huo ulikuwa ni utangulizi wangu kama vile ambavyo wengine wanamshukuru Mheshimiwa Chiza kuchaguliwa leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, si kila jambo linalofanywa na Serikali hii ya Awamu ya Tano ni baya ila tatizo ni kwamba hata yale mambo mazuri yanafanywa bila utaratibu ndiyo maana yanaishia kuwa ya hovyo. Kwa kusudio la kufanya Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi, enzi za Mwalimu alikuwa na kusudio la kufanya Dodoma kuwa Makao Makuu. Hivyo basi, si kwamba Serikali za awamu zilizopita zilishindwa kutangaza Manispaa ya Dodoma kuwa Jiji kama hoja ni kutangaza tu. Umuhimu wa kutambua kwamba utaratibu wa kutangaza Jiji upo kisheria na una vigezo vyake.

Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya sana sana tunaletewa Muswada huu wa kuipandisha Manispaa ya Dodoma kuwa Jiji hatimaye kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu...

SPIKA: Sasa hapo Sophia...

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA): ...ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania...

SPIKA: Hapo Sophia ndiyo yale niliyokuwa nakwambia kwamba Muswada uliopo hapa ni kuifanya Dodoma kuwa Mji Mkuu na siyo kufanya Dodoma kuwa Jiji. Endelea tu (*Makofi*)

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Jedwali la Tano la Sheria ya Mipango Miji ya mwaka 2007 likisomwa pamoja na kifungu cha 7(2) cha sheria

hiyo, ni kwamba mamlaka ya kupandisha hadhi Manispaa kuwa Jiji itakuwa kwa Bunge. *The power to bestow a municipality the status of a city shall be vested in the National Assembly.* Licha ya takwa hili la kisheria, Serikali imepoka madaraka ya Bunge na kuchukua jukumu la kutangaza Manispaa ya Dodoma kuwa Jiji wakati haina mamlaka hayo kisheria... (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Sophia bado upo nje ya uwanja, yaani inaelekea hamuelewi hasa kitu gani kimekuja hapa mbele. Kilichokuja hapa si kutangaza Dodoma kuwa Jiji na Muswada huu ni wa kurasa mbili tu wala hauna kurasa nyingi. Tunatakiwa tujielekeze kwenye jambo ambalo lipo mezani. Jitahidi uruke hayo mengine, hayana maana.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Spika, ukiachilia mbali ni nani mwenye mamlaka ya kuipandisha hadhi Manispaa kuwa Jiji, Jedwali la Tano la Sheria hiyo hiyo ya Mipango Miji imeweka orodha ya sifa au vigezo ambavyo Manispaa inatakiwa kuwa navyo ndipo iweze kutangazwa kuwa Jiji. Sifa hizo ni pamoja na Manispaa husika kuwa na idadi ya watu wasiopungua 500,000; uwezo wa kujidesha kibajeti kwa kutumia mapato ya ndani kwa zaidi ya asilimia 95; kuwa na vitu vyenye utambulisho wa kipekee kama vile maeneo ya kihistoria; maeneo yenyе umaarufu wa kiutamaduni kama vile vituo vikubwa vya utalii...

SPIKA: Mheshimiwa Sophia si nia yangu kukukata lakini inaonyesha kabisa jinsi ambavyo kambi ilikuwa *very unprepared* kuleta maoni. (*Makofii/Kicheko*)

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Spika, unafahamu jana kama Kambi Rasmi ya Upinzani tumekulalamikia na hii tumefanya kama Wabunge kwa utashi na uelewa wetu kwa sababu mmetuondolea wafanyakazi wanaotufanya tafiti, naomba kuendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana Manispaa ya Dodoma haikidhi kigezo hata kimoja kilichotajwa na sheria hiyo.

SPIKA: Mheshimiwa Sophia sasa unabishana na Kiti na unafahamu kabisa nachokuelekeza ni kitu cha msingi sana kwamba jielekeze kwenye sheria iliyopo hapa, sheria hii haizungumzii habari ya Manispaa ya Dodoma kuwa Jiji. Mchungaji Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, samahani labda tupate maelekezo. Hii sheria tulioletewa hapa inasema *The Dodoma Capital City (Declaration) Act, 2018; Arrangement of section, section 1 - Short title; application; interpretation, declaration of Capital City*, inazungumzia *management of Capital City*. Sasa napata tabu kwamba tunawezaje kukwepa haya mambo yote tunapojadili kwenye kuwa *Capital City* hapa, labda tungepata ufanuzi katika hilo.

SPIKA: Mheshimiwa Msigwa *Capital City* na *City* ni vitu viwili tofauti. Arusha *is a City*, Arusha *is not a Capital City*, Mwanza *is a City*, Mwanza *is not a Capital City*. We are talking about a Capital City here, mbona ni straight forward wala haina shida. Kama umemaliza Sophia basi, tunazungumza habari ya Mji Mkuu siyo Jiji, Majiji yapo mengi tu. (*Makof*)

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Spika, mara nydingi tukileta maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kumekuwa na utaratibu wa kutuzuia. Kwa maana hiyo, naomba niikabidhi ripoti yetu na iingie kwenye *Hansard* kama ilivyo ili tuweze kuonyesha kwamba tuliweza kutoa maoni yetu kama Kambi Rasmi ya Upinzani na Serikali itachukua yale inayoona yanafaa lakini bado sisi ni muhimu kufanya kazi yetu kama wapinzani kuielekeza Serikali kufanya yale mambo yanayostahili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa kwa ustaarabu uliouounesha. Kwa kweli hatuzuui mtu yejote kusikika, lakini tukiwa tunafanya kwamba ajenda inakuja inahusu jambo fulani halafu mtu anakuja na ajenda zake mwenyewe na kuanza kuzungumza mambo ambayo wala hayapo inatupa shida kidogo. Hata hivyo, ukiwa na ushahidi nayo unaruhusiwa tu, taratibu zetu za Bunge hazina tatizo kama kuna watu wanunuliwa unaruhusiwa tu, lakini baadaye kidogo ukibanza usiseme kwamba umeonewa kwa sababu ni mpinzani na kadhalika. Hilo tu ndiyo tunasisitiza na kukumbushana kwa sababu muda mrefu mlikuwa hamjaandika hotuba sasa sikushangaa sana lakini huko mbele tunapoenda natumaini tutajikita zaidi kwenye *subject matter* iliyopo mezani.

**MAONI YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI KATIKA OFISI YA RAIS – TAMISEMI, MHESHIMIWA
JAPHARY MICHAEL (MB), KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA
KUTANGAZA JIJI LA DODOMA KUWA MAKAO MAKUU YA
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA YA MWAKA 2018
(THE DODOMA CAPITAL CITY (DECLARATION) ACT, 2018) –
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu Muswada wa Sheria ya Kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa maoni hayo, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutujalia sote uhai, lakini zaidi sana kwa kuendelea kutujalia moyo wa ujasiri na uvumilivu hasa sisi wabunge wa vyama vya upinzani ambao kwa kipindi hiki tunapita kwenye majaribu makubwa.

[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

2. MUSWADA WA SHERIA YA KUTANGAZA JIJI LA DODOMA KUWA MAKAO MAKUU YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Mheshimiwa Spika, si kila jambo linalofanywa na Serikali hii ya awamu ya tano ni baya; ila tatizo ni kwamba hata yale mambo mazuri yanafanywa bila utaratibu ndiyo maana yanaishia kuwa ya hovyo. Kusudio la kuufanya Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi tangu enzi za Mwalimu lilikuwa jema; na kusudio hilo lilikuwa likitekelezwa kwa awamu kulingana na vigezo na mahitaji ya wakati husika. Si kweli kwamba Serikali za awamu zilizopita zilishidwa kutangaza Manispaa ya Dodoma kuwa jiji kama hoja ni kutangaza tu! Muhimu la kutambua ni kwamba utaratibu wa kutangaza Jiji upo kisheria na una vigezo vyake.

Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya sana tunaletewa Muswada huu wa Kuipandisha Manispaa ya Dodoma kuwa Jiji na hatimaye kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati zoezi hilo lilishafanyika nje ya utaratibu wa kisheria. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili; hivi Bunge linatunga sheria kuweka utaratibu wa kuanzisha kitu au linatunga sheria kubariki kitu kilichoanzishwa nje ya utaratibu?

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Jedwali la tano la sheria ya Mipango Miji ya mwaka 2007 likisomwa pamoja na kifungu cha 7(2) cha Sheria hiyo, ni kwamba mamlaka ya kupandisha hadhi Manispaa kuwa Jiji itakuwa kwa Bunge. *"The power to bestow a municipality the status of a city shall be vested in the National Assembly"* Licha ya takwa hili la kisheria, Serikali imepoka madaraka ya Bunge na kuchukua jukumu la kuitangaza Manispaa ya Dodoma kuwa Jiji wakati haina mamlaka hayo kisheria. Hii ni dharau kubwa sana kwa Bunge, na ni mwendelezo wa tabia ileile ya Serikali hii ya CCM kulidhibiti na kulinyamazisha Bunge. Jambo hili halikubaliki na safari hii lazima Bunge lisimame litetee kwa wivu mkubwa mamlaka yake.

Mheshimiwa Spika, ukiachilia mbali ni nani mwenye mamlaka ya kuipandisha hadhi manispaa kuwa Jiji; jedwali la tano la sheria hiyo ya Mipango Miji imeweka orodha ya sifa au vigezo ambavyo manispaa inatakiwa kuwa navyo ndipo iweze kutangazwa kuwa jiji. Vigezo hivyo ni pamoja na Manispaa husika kuwa na idadi ya watu wasiopungua laki tano (500,000); Uwezo wa kujidoresha kibajeti kwa kutumia mapato ya ndani kwa zaidi ya asilimia 95; kuwa na vitu vyenye utambulisho wa pekee kama vile maeneo ya kihistoria; maeneo yenye umaarufu wa kitamaduni kama vile kituo kikubwa cha utalii; kuwe na makao ya shughuli za kimataifa nk.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana Manispaa ya Dodoma haijakidhi kigezo hata kimoja kilichotajwa na sheria hiyo. Kuhusu kigezo cha idadi ya watu, sensa ya 2012 inaonyesha kwamba idadi ya watu katika manispaa ya Dodoma ni takriban laki nne (400,000); na hata maoteo (projections) ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu yanaonyesha kuwa Manispaa ya Dodoma ilitarajiwa kuwa na watu lakin nne na hamsini na sita (456,000) kufikia mwaka 2017. Kwa hiyo, kwa kigezo cha idadi ya watu, Manispaa ya Dodoma haina sifa za kuwa Jiji

Mheshimiwa Spika, kigezo kingine muhimu cha Manispaa kuweza kuwa jiji ni kujitosheleza kibajeti kwa kutumia mapato ya ndani kwa zaidi ya asilimia 95. Ukweli ni kwamba Manispaa ya Dodoma haijawahi kufikia kigezo hicho. Hii ni kwa sababu miradi mingi ya maendeleo chini ya Capital Development Grant imekwama kutokana na kukosa fedha kutoka Serikali Kuu. Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ingekuwa inajitosheleza kibajeti ingeweza kutumia fedha zake kukamilisha miradi hiyo. Lakini bado Halmashauri inategemea fedha kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya miradi yake ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vigezo vin gine vya kuwa na vitu vyenye utambulisho wa pekee na maeneo ya kihistoria pamoja na kuwa na makao kwa ajili ya shughuli za kimataifa bado Dodoma haijakidhi vigezo hivyo. Hakuna eneo la utalii

wa kitamaduni Dodoma, hakuna vitu vyenye utambulisho wa pekee au maeneo ya kihistoria; hakuna shughuli za kimataifa zinazofanyika Dodoma ukiachilia mbali tangazo la Serikali la kuwataka mabalozi waje kununua viwanja vyatujenga balozi zao. Kwa kifupi sifa hizo za kisheria hazijafikiwa na Manispaa ya Dodoma.

Mheshimiwa Spika, masharti mengine ya kutangaza jiji ni yale yaliyoainishwa katika Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 kwamba katika upanuzi wa mijii Serikali kuzingatia mahitaji na ulazima wa kupanua mijii na kwa kuzishirikisha mamlaka zinazohusika na umegaji au umegwaji wa maeneo yao. Aidha katika kufanya hivyo, Serikali inatakiwa kuhakikisha kwamba maeneo ya vijiji yanakoma kuwa vijiji. Aidha, tangazo la kuifanya Manispaa ya Dodoma kuwa Jiji lilitakiwa liende sambamba na kutangaza eneo (ukubwa) na mipaka ya Jiji hilo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utaratibu huo wa kisera, Hakuna kikao chochote cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma kilichokutana na kuazimia kupandisha hadhi Manispaa ya Dodoma kuwa Jiji. Aidha, jiji hilo tajwa eneo lake na mipaka yake hajatangazwa na bado kuna maeneo mengi ya vijiji katika Jiji hilo tajwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi kitendo cha kutangaza Manispaa ya Dodoma kuwa Jiji kimefanyika kinyume na Sheria; na hata bunge hili kukaa kutunga sheria ya kitu ambacho kimeshaanzishwa tayari nako ni kwenda kinyume na sheria. Inafahamika kuwa siku zote sheria hutungwa kwa mambo mapya siyo yaliyopita; lakini kwa mshangao mkubwa sheria hii inatungwa kuhalalisha mambo yaliyopita (retrospective).

Mheshimiwa Spika, kifungu cha pili cha muswada huu kinaeleza kwamba sheria inayopendekezwa itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Kwa mujibu wa ibara ya 98(1)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sheria ya namna hiyo inatakiwa kuitishwa na theluthi mbili ya wabunge wote. Theluthi mbili ya wabunge itapatikana

kwa kupiga kura ya wazi kwa kila mbunge kuitwa jina na kusema ndiyo kama anaikubali au hapana kama anaikataa. Nimetoa angalizo hili kabla ili tusije tukapitisha sheria ya namna hii kwa kuhojiwa (acclamation) na kujibu kwa ujumla wetu kwani kwa kufanya hivyo itakuwa vigumu kupata theluthi mbili ya watu waliotamka kwa pamoja. Ni vema kuzingatia jambo hili ili kuwa na kauli moja ya bunge katika kuipitisha sheria hii iwe tumeikubali au tumeikataa.

3. HITIMISHO

Napenda kumalizia hotuba yangu kwa kutoa rai kwa Serikali kuzingatia sana utaratibu wa kisheria inapotekeleza majukumu yake. Sheria ndiyo msingi wa utekelezaji makini wa shughuli za Serikali. Sheria ndiyo inayoelekeza kazi zifanyike namna gani na sio kazi ziielekeze sheria cha kufanya. Kutangaza Jiji la Dodoma nje ya utaratibu wa sheria na baadaye kuja kutunga sheria kuhalalisha tangazo hilo ni sawa na kujenga nyumba bila msingi na baadaye kuja kujenga msingi. Kwa vyovyyote vile msingi huo hauwezi kuwa imara.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Japhary Michael (Mb)
**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI
KATIKA OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
4 Septemba, 2018

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, leo uchangiaji wetu ni wa dakika 15 kwa kila Mbunge lakini tukifanya hivyo watachangia Wabunge wachache mno. Kwa hiyo, nilikuwa nataka bila kumtaka Waziri wa Nchi kutengua Kanuni nitumie tu mamlaka yangu ya uendeshaji bora wa shughuli za Bunge mnikubalie mnaochangia mjikite kwenye dakika 10, kitu chenyewe kipo *straight forward* hiki. Kwa maana hiyo mtapata nafasi watu wengi zaidi kuweza kuchangia. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, nafikiri sasa tuendelee, Mheshimiwa Ally Saleh uanze.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kusema ukweli hii ni sheria muhimu kwa maana ya *progress* ya nchi na ni sheria ambayo pengine wengine wanaweza wakasema kwamba ingepaswa ije kabla ya hapa lakini mtu anaweza akajiuliza kwa nini imechelewa muda wote kutangaza Makao Makuu ya nchi. Kwa sababu hii si dhana ngeni imewahi kutokea sehemu nyingi kama ilivyosema hotuba ya Kamati na hata ndani ya Afrika kumekuwa na nchi ambazo zimekuwa zikiamua kubadilisha Makao Makuu yao.

Mheshimiwa Spika, kubadilisha Makao Makuu kunategemea sababu nyingi, inawezekana ya kiusalama, kibashara au mkakati mwingine wa kuleta maendeleo karibu na watu. Kwa mfano, zipo nchi ambazo kwa kuanzia ziliikuwa na mipaka yake karibu na nchi nyingine, wameondosha Makao Makuu kupeleka sehemu nyingine ili kuondoa uwezekano wa matatizo inatokea dharura katika nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, hakuna maelezo ya kina hasa kwa nini tumehamisha kwa maana ya kuja katikati ya nchi lakini tuna-*assume* kuna sababu ambazo zimeelekeea kufanya hivyo. Sehemu kubwa tumejikita katika Tamko la Mwalimu Nyerere la mwaka 1973 kwamba angependa kuona Makao Makuu ya Chama chake cha *TANU* wakati huo yanakuwa Dodoma na halikadhalika na Makao Makuu ya Nchi yanakuwa Dodoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tukumbuke wakati anasema hivyo kulikuwa na Chama cha *ASP* cha Zanzibar kwa sababu tuliunganisha vyama mwaka 1977 kwa maana ya *TANU* na *ASP*. Kwa hivyo, dhana ambayo mimi naweza kuipata ni dhana ya Mwalimu kwa chama chake na siyo dhana ya Tanzania nzima. Kwa maana hiyo, wakati huo alipaswa au

ilitakiwa tuoneshwe tamko ambalo alizungumza kwenda zaidi ya pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, alikuwa anakisemea chama chake.sasa hivi kushikilia hoja hiyo kwamba ndiyo hoja madhubuti ya kwamba tunahamisha Makao Makuu ya nchi kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma kwa sababu ya kauli kama hiyo inaleta utata kidogo kwa sababu wakati ule Mwalimu alitia na suala la chama chake cha *TANU*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile...

TAARIFA

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Ally Saleh upokee taarifa, Mheshimiwa Peter Serukamba.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nataka kumpa taarifa mzungumzaji kaka yangu Mheshimiwa Ally Saleh kwamba mwaka 1973 nchi hii ilikuwa na chama kimoja tu. (*Makofi*)

SPIKA: Unaipokea taarifa hiyo Mheshimiwa Ally Saleh.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Spika, namshangaa swahiba yangu kwamba hajui kwamba mwaka 1973 kulikuwa na Chama cha *Afro Shiraz Party - Zanzibar* na kulikuwa na Chama cha *TANU - Bara*. Ndiyo maana nikatangulia kusema kwamba 1977 vyama hivi vikaungana *ASP*na *TANU*ikazaliwa CCM na mimi nilikuwepo Zanzibar wakati ule na udogo wangu nilikwenda Uwanja wa Amani kushuhudia. Kwa hivyo, taarifa hiyo siipokei na nakusamehe kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kuhamisha Makao Makuu ya nchi ungetarajia kungekuwa na kitu cha kuuliza wananchi wanasemaje juu ya kuhamishwa Makao Makuu ya nchi kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Siku za nyumba haikuwahi kufanya lakini ningetarajia sasa hivi kutokana na kupanuka kwa demokrasia na vitu mbalimbali kungekuwa na *White Paper* Wazanzibar kama walivyoulizwa kuunganisha vyama, wangeulizwa juu ya kuhamishwa mji kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nikasema tangu mwanzo, dhana ya kuhamisha siyo *problem*, kwa sababu kunaweza kuwa na sababu nyingi za kimsingi za kuhamisha lakini hizi ni pande mbili za Muungano. Unapohamisha Makao Makuu ya nchi kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine, ilipaswa pande mbili zishiriki kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, taarifa niliyonayo, sina uhakika, sitaki nijinukuu lakini katika *corridors* tunaambiwa Serikali ya Zanzibar katika hili haikushiriki. Tunaambiwa na watu wetu waliopo katika Kamati walimuuliza Mheshimiwa Waziri anayehusika na jambo hili, vipi kuhusu hili hakuna jawabu la uhakika lilitotoka kwamba Zanzibar ilishiriki. Sasa unahamishaje Makao Makuu ya nchi ya pande mbili bila ya *popular will* ya pande zote mbili zinazohusika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa tatizo liko wapi? Ni katika mfumo mzima wa sheria wa Tanzania. Serikali ya Muungano inaweza ikaamua chochote kuhusu Muungano, hapa tunaambiwa itapigwa kura kwa maana ya Bunge zima na ni sawa kwa maana ya Bunge zima tupate *two third* lakini mara nyingi sheria ikishapitishwa hapa inatakiwa iende kuwa *tabled* katika Baraza la Wawakilishi, unajiliza tutasema mara ngapi kama nchi kwamba kuna matatizo katika kutunga sheria lakini ikienda kule inaenda kukataliwa, hii ni moja katika sheria ambayo inaweza kukataliwa Zanzibar labda itumike *whip* ya chama lakini njia rahisi ingekuwa ni kuishirikisha Serikali ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ipo mifano mingi ambapo sheria iliyotungwa huku bila kushirikishwa Zanzibar kule zimekataliwa, mojawapo ilikuwa ni ya *Deep Sea*. Sheria ile ilipitishwa kwa magube hapa kwa sababu ya huu utaratibu kwamba Serikali ya Muungano inaweza ikafanya lolote lile kisheria hailazimiki kuishirikisha Zanzibar, hilo ni kosa kubwa la kikatiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nasema binafsi naafiki suala la kuhamisha lakini ninavyoona mimi taratibu hazijatimia, mojawapo ni kujaribu kuwaliza wananchi kwamba wanataka Makao Makuu ya nchi yao yahamishwe yaje Dodoma? Upande wa Zanzibar hatukuwahi kuona kwa maana ya kura ya maoni au njia yoyote ile ya kuwashirikisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ally Saleh. Ninyi kama Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo mnafanya kazi hii kwa niaba ya wananchi kwa hiyo Tanzania yote ipo humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa atafuatiwa na Mheshimiwa Boniface Simbachawene.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru na mimi kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, nianze kama alivyosema Mheshimiwa Saleh, dhana nzima ya kuifanya Dodoma iwe Makao Makuu ni nzuri na hatuwezi kusema ni jambo baya. Hata hivyo, kuna tofauti kubwa sana kati ya kufanya jambo zuri na jambo sahihi. Linaweza likawa ni jambo zuri lakini lisiwe jambo sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wabunge hapa kazi yetu kubwa ni kusimamia kodi za wananchi. Kwa hiyo, masuala

mengi ambayo Serikali inatuletea mezani ni wajibu wetu kutafakari kwa pamoja kama Taifa kwamba hili suala tunalokwenda kulifanya *is it economical?* Ni suala la kiuchumi, lina tija gani kwa wananchi wetu, ni *priority*, liliwa limepangwa? Sasa tunaangalia kile ambacho tunacho kwenye hazina kama Taifa, tunaangalia vipaumbele vyetu ni *vipi*, vitaleta tija gani, sisi kama Wabunge ni wajibu wetu kuchekecha.

Mheshimiwa Spika, tukiwa wakweli na tukijitathmini kiundani kweli kweli, amezungumza Mheshimiwa Saleh hapa wengi wanakuja na hoja kwamba Mwalimu Nyerere alishasema, Mwalimu Nyerere kasema mambo mengi sana, alishawahihata kusema kwamba chama kinachofaa kutawala baada ya CCM ni CHADEMA, hilo mbona hamelitekelezi? Hatuwezi tukasema mambo yote aliyosema Mwalimu Nyerere lazima tuyatekeleze hapa lakini mnachukua yale machache aliyosema Nyerere mnapindisha msumeno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachotaka kusema wajibu wetu ni kutunza kodi ya wananchi. Nchi hii ina matatizo mengi na makubwa sana. Ukiangalia kwa mfano kwenye masuala ya afya kuna matatizo makubwa sana, *policy* ya nchi yenu imezungumza mambo mengi sana kuhusu kuboresha afya ya mama na mtoto, tuna matatizo ya maji na kuna mambo makubwa ya msingi. Sasa tukipima kama Wabunge tukitafakari hapa wote tukiwa na *sober mind*, tuna-reason, tunakuja na *evidence* kwa sababu *argument* hapa ni kuhamia Dodoma kama tuna *reasoning* ukipima mizani *is this our priority?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulipoingia Bunge hili, suala hili halikuwa kwenye Mpango wa nchi wa Miaka Mitano, *it was unplanned*; halikuwa kwenye mpango wa mwaka mmoja, *it was unbudgeted*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa leo tunakuja na...

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Msigwa pokea taarifa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Spika, naomba tu kumpa tarifa Mchungaji Msigwa kwa mujibu wa Kanuni ya 68(8) kwamba Ibara ya 151 ya llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 imeeleza wazi mkakati na mpango wa Serikali kuhamishia Makao Makuu hapa Dodoma. Kwa hiyo, kila jambo litakalotekelezwa na Serikali yetu kwa miaka hii mitano ni lazima linatokana pia na mapendekezo ya llani ya Uchaguzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namuomba Mchungaji Msigwa ajue kwamba haya tunayoyatekeleza, tunatekeleza llani yetu ya Uchaguzi; tunatekeleza afya, maji, barabara na tuatekeleza na mambo mengine. (*Makofii*)

SPIKA: Mchungaji pokea taarifa hiyo.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nimeomba haya masuala tuyajadili tukiwa na *sober mind*. *It's not about* Chama cha Mapinduzi au CHADEMA, tunazungumzia kuhusu masuala ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, labda nikurudishe kidogo; *simple understanding*, mkiwa na *argument* yoyote kuna mambo matatu ya kuzingatia ambayo ni *premises*, *inference* na *conclusion*. *Premises* tuliyojenga hapa tunazungumzia kuhamia Dodoma lakini kwenye *inference* tulete hoja, tuwe na *argument* za hoja, tuwe na mifano, kwa nini tunahamia Dodoma na kwa nini tusihamie Dodoma?

Mheshimiwa Spika, mimi najenga hoja, ukiniambia hapa llani ya Chama cha Mapinduzi, hatutekelezi llani ya Chama cha Mapinduzi hapa, tunatekeleza Mpango wa Taifa. Tukishamaliza uchaguzi na kuja humu ndani tunaubadilisha unakuwa Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano na inakuwa Mpango wa Taifa wa mwaka mmoja mmoja; sasa Chama cha Mapinduzi kinatoka wapi hapa, vinginevyo si mngejadili kwenye *caucus* muamue wenyewe? Mimi nazungumzia Mpango wa Miaka Mitano wa Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa nimezungumza tuwe na *sober mind*, tuangalie *is this our priority?* Siku moja niliwahi kusema hapa, Botha kwenye hotuba yake maarufu aliwahi kusema, *an African person can only plan for one year.* Nimezungumza hiki kitu, tumekuja hapa *it was unplanned; ilikuwa-plannedwapi*, kwenye Mpango wa Miaka Mitano iko wapi?

SPIKA: Kwa hiyo, Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, unakubaliana na Kaburu Botha kuhusu mtu mweusi?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, kama tunafanya mambo bila kupanga tutakuwa tuna-*prove*. Kwa sababu kama hatupangi, yaani tunaamka asubuhi leo twende Dodoma, hakuna bajeti, hela ziko wapi, hatuna *priorities*, sasa tunamkosoaje Kaburu? Kaburi siyo rangi hata mtu mweusi anaweza kuwa Kaburu tu kama Mwalimu alivyosema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi / am not against...

SPIKA: Yaani Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, kweli unaunga mkono P.W. Botha?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, usi-*spin*. Sijasema namuunga mkono Botha lakini nasema anaweza akatu-*prove right* kama tunafanya makosa yale

yale. Kwa sababu hii nchi haijapata uhuru jana ndugu zangu, hii siyo Sudan ya Kusini ambayo wanahangaika kutafuta majengo. Leo hata wewe mwenyewe Mheshimiwa Jenista ofisi yako ni mgogoro hapa Dodoma. Ofisi zote hapa ni mgogoro, ukienda kwa mfano Zimamoto kwa Wizara ya Mambo ya Ndani kuna majengo makubwa tulikuwa tume-plan kule Dar es Salaam, yalikuwa yanainuka, sasa hivi tumesimamisha tunakuja hapa Dodoma. Narudia kusema, *it was unplanned, unprepared, unbudgeted, uneconomical.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumekuja hapa tunataka ku-popularize tu, tunatafuta *political mileages* kuleta hapa lakini haya mambo tukikaa chini, nimezungumza tuna matatizo makubwa sana ya vituo vya afya, vifo vya akina mama na watoto, hatujayaweka mbele; magonjwa mengi yanayosababishwa na...

TAARIFA

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Mlinga nimekusikia, taarifa.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, tatizo la Kambi Rasmi ya Upinzani huwa hawahudhuriil Vikao vya Bunge. Bajeti iliyoisha tumejenga vituo 205 vya afya nchi nzima. Mwaka huu kwenye bajeti tumetoa pesa kwa ajili ya kujenga hospitali 64 za wilaya; hiyo siyo kipaumbele? Muwe mnahudhuria vikao vya Bunge. (*Makofi*)

SPIKA: Hiyo umepigwa kwa *data*. (*Kicheko*)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, haya ni matatizo ya kukimbia shule. Nimezungumza mambo ya *inference*, nadhani haelewi hata ninaposema *inference* ni nini. Anazungumzia vituo 200, nchi hii tunahitaji vituo 4,600 wewe

unazungumzia vituo 200. Hizo *data* gani amazoniambia? (*Makofi*)

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, nina elimu ya *masters...*

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Sasa linakuwa Bunge gani hili? Tunapewa nafasi na Spika bwana.

SPIKA: Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, pokea taarifa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, tunahitaji vituo 4,600 na magonjwa mengi tunatumia pesa nyingi kwenye dawa yako *related*na maji, watu wanakunywa maji machafu. Dodoma hii inaongoza kwa kutokuwa na maji, sasa *priority*ni kuhamia Dodoma, tuseme tu tumehamia Dodoma au tunapanga hela zetu chache tulizonazo tuangalie *priority* yetu ni ipi, tufanye nini? Watoto hawana vifaa madarasani, hawana madarasa; *is it our priority?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali hajatuambia hapa *how much money you are using moving from Dar es Salaam to here*, halafu tunakuja hapa tushangilie tu. Huu si wajibu wa Bunge, Bunge siyo *rubber stamp, we are here to reason*, tuje na *evidence*. Njooni na hoja zenu kwamba faida ya kuhamia Dodoma ni hii, tukikaa Dar es Salaam ni hii, tusipokwenda Dodoma tutapata hasara moja, mbili, tatu nne, tukikaa Dar es Salaam tutapata hasara moja, mbili, tatu nne. Mnakuja hapa na siasa mnatuambia llani ya Chama cha Mapinduzi, *who cares?* Inatusaidia nini hapa? *We are all in the same boat*. Chama cha Mapinduzi kikiwa dhaifu wote tunakuwa dhaifu hapa, mnahitaji *strong political party* ili muwe na nguvu, sasa mnakaa mnajilegeza hapa mnapiga makofi tu, mnataka tusi-reason? Mahali hapa ni pa ku-reason. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya duniani kote, ndiyo maana mihimili mitatu ilianzishwa. Mtawala, Serikali

yoyote huwa inataka Bunge liwe *rubber stamping*, lisijadili, watu wapige makofi, kwa sababu mtawala yeote duniani anataka mambo yake yawe mteremko. Bunge lipo kwa ajili ya ku-*balance* na tuko hapa kusema Serikali mmeleta mpango huu, huu mpango unatia hasara kwa Taifa, haya lazima tujadiliane hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa tunakuja hapa mnaanza kusema Serikali, llani ukurasa, mimi *I haven't even read your llani*. Tulikuja tukajadili kama Wabunge hapa tumeondoka na Mpango wa Miaka Mitano wa nchi, hiyo ndiyo dira ya nchi yetu. Hivi vitu havikuwa *planned*, havipo, tukiwaambia mnashindwa kutekeleza hayo mambo mnaanza kusema tunahama hoja. (*Makofi*)

TAARIFA

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Ndugu zangu, haya ni mambo ya kujadiliana wote kwa pamoja...

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Hela tuliyonayo tupime...

SPIKA: Taarifa, tafadhali.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Spika, mchangiaji anayechangia anaonesha jinsi gani ambavyo yeye mwenyewe ni mshiriki wa vikao vya Bajeti vya Bunge, ni mshiriki wa vikao vya bajeti vya hal mashauri na katika maandalizi ya bajeti tunaangalia maeneo mengi na si eneo moja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kimsingi suala la kuweka gharama za kuhamia Dodoma ni moja ya mwendelezo wa mikakati ya kuendeleza nchi na Serikali iko makini ndiyo maana tunatekeleza. Yeye katika halmashauri anafanya mipangilio ya bajeti ya miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida, kwa hiyo na kile kinachofanyika kwenye vikao vyta halmashauri ambavyo anahudhuria basi anatuonesha jinsi gani ambavyo hayuko makini kwa masuala ambayo yanafanyika katika halmashauri yake.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, binafsi hata sjamuelewa. Nachowenza kusema kwa kifupi kwa sababu mmekuwa mnani-*interrupt* sana, *it is very dangerous to do a good thing at the expense of the right thing*. Kama ninyi mnaona kuhamia Dodoma ina tija zaidi kuliko kuboresha vituo vyta afya, kuliko kuwa na maji ya kutosha katika nchi hii ili tupunguze magonjwa, wananchi watatu-*Judge* na historia itakuja kuzungumza. Nimesema kuja Dodoma ni jambo zuri lakini *it was unplanned, it is not economical, we were not prepared, it is unbudgeted.* (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, nakushukuru sana. Hata hivyo, ni vizuri hata ukiwa mpinzani, *principles* kuzibakiza kuwa *principles*. Hakuna wananchi wa Tanzania waliopigia kura Mpango wa Taifa unaouzungumza, wananchi walipigia kura llani, *whether you like it or not*. Kwa hiyo, iwe ni mpango gani lazima uanze kwenye llani iliyochaguliwa na wananchi. Kwa hiyo, *whether you like it or you don't like the llani that's the common denominator*, kwa hiyo, hilo tukubaliane. Kwani Makao Makuu yalivyokuwa Dar es Salaam hivyo vituo vyta afya vilimalizika kujengwa? (*Makofi/Kicheko*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Simbachawene, atafuata Mheshimiwa Joel Makanyaaga.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kabisa kwa kuunga mkono hoja iliyoko mbele yetu. Kusema kweli, kama mtu wa Dodoma aliyeko nje ya Bunge amesikiliza hotuba ya mzungumzaji aliyeppita, ndugu yangu Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, Msigwa anajitafutia chuki isiyokuwa na sababu na watu wa Dodoma.

WABUNGE FULANI: Aaaaa.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, kwa sababu kwanza Mheshimiwa Mchungaji Msigwa anafahamu wazi kabisa na Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania wanafahamu kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekamilisha mpango wa kuhamia Dodoma, iko kwenye asilimia 99, yaani zoezi limekwisha. Serikali imehamia Dodoma, Wizara zote ziko Dodoma, Waziri Mkuu yuko Dodoma, Makamu wa Rais yuko Dodoma amebakia Rais tu yaani biashara hii imekwisha. Jambo likiwa limekwisha mimi nadhani njia nzuri ya mtu mstaarabu ni kupongeza tu kwamba kazi imefanyika vizuri na mambo yote yanaendelea vizuri na hakuna ambalo limeshindwa kufanyika. (*Makofii*)

T A A R I F A

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika...

SPIKA: Naomba iwe taarifa ya kweli.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, ndiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa msemaji anayeongea sasa hivi kwa ajili ya kuweka hali ya hewa sawa. Kama ambavyo yeye anafikiri Mheshimiwa Mchungaji Msingwa anawakosea watu wa Dodoma ukiangalia na mchango aliokuwa ametoa Mheshimiwa Ally Saleh ni

sawasawa na ambavyo Chama cha Mapinduzi kinazidi kujichimbia kaburi upande wa Zanzibar kwa maana ya Muungano. Kwa sababu nako hawajashirikishwa kwenye zoezi hili la kutaka kufanya Dodoma iwe ndiyo Makao Makuu ya nchi yetu, kwa hiyo, nayo aichukue. (*Makofii*)

SPIKA: Hiyo ni kupanda chuki tu.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa
Wabunge waliongea bila mpangilio)*

SPIKA: Maana siku hizi mmekaa Zanzibar, Zanzibar, mmekuwa wapenzi wa Zanzibar tangu lini?

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa
Wabunge waliongea bila mpangilio)*

SPIKA: Mheshimiwa Simbachawene, endelea.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, taarifa yake siipokei, kwa sababu uamuzi wa kuhamia Dodoma kwa mara ya kwanza ulifanywa na Serikali ya kikoloni mwaka 1959, na kwa mara ya pili ukafanywa mwaka 1973 na Serikali ya Awamu ya Kwanza na sababu ni hizi zilizopo kwenye *preamble* kwenye Muswada huu. Sababu hizi za kwenye *preamble* zimejitosheleza na zinaonesha ukubwa na uzito wa uamuzi huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa faida kubwa kwa Watanzania sababu ni kwamba Dodoma ni katikati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuweka Makao Makuu ya nchi Dodoma ni kutafuta urahisi wa kuwashudumia Watanzania. Ni rahisi kwa Watanzania kutoka katika kila pembe ya nchi yetu kuja Dodoma na kurudi kwa ghamama nafuu lakini pia ni rahisi kwa Serikali *ku-monitor* maendeleo na matatizo ya wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoa...

TAARIFA

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Unajua tukiyaendekeza haya mambo huu mjadala utakuwa mgumu sana.

WABUNGE FULANI: Aaaaa.

SPIKA: Kwa sababu taarifa mnazozitoa wala siyo taarifa, hebu itoe hiyo taarifa tuisikie.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nataka tu nimpe taarifa Mheshimiwa Simbachawene, sasa hivi teknolojia imebadilika mno, ukatikati hauna maana yoyote kwa sababu mtu anaweza kutuma karatasi dakika moja kutoka kijiji chochote ikaja hapa, tofauti na kipindi cha miaka ya sabini.

SPIKA: Sasa hiyo ndiyo taarifa kweli?

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

SPIKA: Tena taarifa hiyo imetolewa na mtu wa Tarime anayeona kutoka Tarime kwenda Dar es Salaam *is cheaper than* Tarime *to Dodoma*, hiyo hesabu sijui ya *kindergarten*, sijui ya shule gani. Mheshimiwa Simbachawene, endelea.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, tatizo langu wanaonipa taarifa wote ni marafiki zangu, sasa inakuwa shida.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kwamba sababu hizi zitabakia kuwa *valid*kwa namna yoyote ile. Mimi nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa uamuvi wake wa dhati wa kuamua kwamba sasa kweli tunahamia Dodoma. Wala hakuja na jambo jipya, hili jambo

amelikuta lakini ye ye ame amua kuli fanya kwa vitendo na ndiyo maana tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu hata katika llani zetu zote hakuna llani ambayo imewahi kuacha kusema tutaendelea kutekeleza mpango wa Serikali wa kuhamishia Makao Makuu ya Serikali Dodoma, hakuna llani imewahi kuacha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, binafsi nikupongeze wewe, Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na historia itakukumbuka katika jambo hili kwa kusimama kidete na kusema lazima ije sheria inayotaka uamuzi wa kuhamishia Makao Makuu Dodoma isiwe tena inawekwa kwenye kanuni bali kwenye sheria iliyotungwa na Bunge. Hakika sisi Wana-Dodoma na wananchi wa Dodoma tunakupongeza sana kwa kusimamia jambo hili kwa nguvu zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara ya TAMISEMI pamoja na wadau wote walioshiriki kutengeneza Muswada huu wa sheria hii ambayo tunaipitisha hapa inayo-*declare* kwamba Dodoma ndiyo Makao Makuu. Ni sheria fupi, ina kurasa mbili, lakini iko *loaded*, huwezi ukachezea tena habari ya Makao Makuu Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kifungu kile cha 4 inazungumza ugumu wa kubadili tena mawazo haya, yaani hata angekuja nani hawezi kubadili mpaka mabadiliko yale yaweze kuitishwa na theluthi mbili ya Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungani wa Tanzania. Hii maana yake nini? Maana yake ni kwamba Serikali imeona ilipe uzito jambo hili kama inavyotoa uzito kwenye vifungu vyta Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii ni heshima kwa uamuzi huu na uamuzi huu kwa kweli umewekewa misingi mizito na mikubwa sana. Tunashukuru sana TAMISEMI kwa kusimamia na kuleta *declaration* hii ambayo ina uzito unaostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kifungu hichohicho cha 4(3), kinasema kwamba sheria nyingine zinazoendesha Mamlaka

za Serikali za Mitaa zitapaswa zizingatie uzito wa Makao Makuu na kwa hiyo Makao Makuu haya haitaendeshwa kwa sheria hizi zilizokuwepo na hivyo ni lazima zitungwe sheria nyingine ili ziweze kufanya Makao Makuu itambulike na kuwa na hadhi yanayostahili, hili ni jambo jema. Kwa sababu hii ilikuwa ni *declaration* basi ifanyike haraka hizi sheria nyingine zinazozungumzwa ziweze kutungwa zinazoendana na uzito wa Makao Makuu maana kwa sheria zilizopo hatuwezi tukaendesha Makao Makuu kwa ufanisi kama ambavyo tunatarajia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nirudie tena kusema, duniani moja kati ya mikakati na kitu cha kujivunia cha kila nchi katika maamuzi ya mambo yao huwa ni uzito na asili na historia ya nchi hiyo. Kwa sisi Tanzania kulitekeleza jambo hili ambalo liliaisisiwa na Baba wa Taifa letu la Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kwetu sisi hii ni ibada na tutatoka tunajivunia. Leo au kesho sheria hii ikipitishwa tutakuwa tumefanya ibada kubwa na sifa hizi ziende kwa Watanzania wote, kwa viongozi wetu wa Chama cha Mapinduzi na wazee wetu, waasisi wa Taifa letu ambao ni wengi kwa kweli na wengine wako hai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, yejote anayebeza mpango huu anaibeza historia ya nchi yetu. Maamuzi haya yalifanywa kwa uzito maana hata nchi kubwa kama China waliamua kuhamisha Makao Makuu kwa gharama kubwa. Nchi kama Nigeria wameamua kufanya hivyo. Ni kwa sababu wanataka kutekeleza mambo yanayolenga maslahi yao, historia na utamaduni wao. Kwa hiyo, sisi kufanya haya leo kwa gharama ndogo kama ilivyotokea, kwa kweli tumejitoa na tumetoa mchango mkubwa na niipongeze sana Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa George Simbachawene kwa *argument* nzuri.

Niwataarifu tu Waheshimiwa Wabunge kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko ziara China na kwa upande wa uongozi wa shughuli za Serikali Bungeni, shughuli hizo anazo Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi. Kwa hiyo, *in case of consultation*, yuko pale tafadhali. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Joel Makanyaaga.

MHE. JOEL M. MAKANYAGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi leo niweze kuwa mmoja kati ya wachangiaji watakaoingia kwenye historia ya Wabunge waliochangia Muswada huu wa kuitangaza Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nimpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, kwa uamuzi wake wa dhati wa kuamua kuyatekeleza kwa vitendo maamuzi yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Kwanza chini ya uongozi wa Rais, Baba wa Taifa, Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mwaka 1973. Leo tukiwa tunayazungumzia ni miaka 45 tangu hayo yametendeka na sasa tunaona yanakwenda kutekelezeka kwa ukweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, si kwamba siku za nyuma hayakuwa yanatekelezeka. Tunachokifanya hapa sasa ni kuweka sheria itakayofanya jambo la kuchezza Dodoma kuwa Makao Makuu lisiwepo tena. Maana tumeona siku za nyuma wakijaribu kwenye awamu mbalimbali zilizopita, kila Rais aliyekuja; Awamu ya Pili, ya Tatu, ya Nne, hakuna ambaye alilipinga jambo hili, lakini kila kulipokuwa kunatokea *move* ya kuja Dodoma ulikuwa unaona inakwenda kwa muda mfupi na baadaye watu wanarudi Dar es Salaam. Kwa umakini kabisa Rais huyu ameona kwamba tatizo liliopo hakuna sheria na sisi tunampongeza sana kwa hili. Sasa tunatunga sheria ifanye iwe vigumu kabisa kwa mtu ye yeyote kuja kujaribu kusema Makao Makuu ya nchi yahamie sehemu nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haya yanayozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge humu ndani ni kweli, kwamba ni gharama kuhamishia Makao Makuu sehemu nyingine. Sasa kama alivyosema msemaji aliyepita Makao Makuu ya nchi yako Dodoma, tukubali tusikubali yako Dodoma hapa leo; Waziri Mkuu yuko Dodoma, Mawaziri wote wako Dodoma, ofisi zote kubwa za Serikali ziko Dodoma, aliyebakia ni Rais peke yake. Kwa hiyo, tukiliacha hili akaja mwingine kusipokuwa na sheria akasema tunahamishia Makao Makuu Mwanza, itakwenda, akipata *consensus* ya Wabunge wengi humu ndani, *two-third* ya Wabunge lakini gharama hii itaendelea kumuumiza Mtanzania. Sasa sisi tunaona ni vyema kwamba gharama hii iishie hapa kuja Dodoma, ndiyo maana tunampongeza sana Rais kwa kuhamia Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme tu haya aliyozungumza mwenzangu, Dodoma ni katikati ya nchi, Dodoma ndipo zinakutana njia nne zote kutoka Kusini hadi Kaskazini kwa maana ya kutoka Johannesburg hadi Cairo Misri. Ukitoka Mashariki unatoboza baharini huko hadi Magharibi, hapa ni katikati. Ni kweli ufikaji wa hapa Dodoma kutoka Mwanza ni rahisi, ufikaji wa hapa Dodoma ukitoka Kaskazini huko Kilimanjaro ni rahisi, ufikaji wa Dodoma toka kona zote ni rahisi kwa sababu ya ukatikati wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kusema teknolojia imekuwa lakini bado viko vitu vinahitaji *presence* ya watu, si kila kitu makaratsi. Rais akitaka kukutana na viongozi mbalimbali wa nchi hii hawatatumwa vikaratasi, watasafiri *physical/waje* hapa, gharama hizi ambazo tunaziona ndogo ndogo ndani ya muda mrefu ni gharama kubwa. Ndiyo gharama ambazo zinaweza kusaidia katika kuleta maendeleo ya nchi hii kwenye sekta nyingine hizo kama afya, elimu na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa na taadhima, mimi nitamke kuunga mkono asilimia 100 Muswada huu wa Shelia Kuifanya Dodoma itamkwe kuwa Makao Makuu ya Nchi. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatuma Toufiq.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu na nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kimsingi kabisa Muswada huu ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Kama walivyotangulia kusema na taarifa ya Kamati imezungumza hapa kwamba nchi nydingi sana zimeweza kuhamisha Makao Makuu ya Serikali kwa sababu ya mambo mbalimbali na sisi Tanzania *base* yetu ni pale Mwalimu Nyerere alivyo-*declare* kwamba angeona na angetamani kwamba Makao Makuu yahamie Dodoma ambako ni katikati ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hapa kuna mambo mawili, nilikuwa nasikiliza Wabunge wenzangu hapa, nimeona majibu ya upande wa Serikali wakati mwingine kuna kujichanganya kidogo. Kwenye *preamble* ukisoma kipengele cha mwisho kinaeleza kwamba:-

"WHEREAS on the 26th April, 2018 His Excellency JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI, the President of United Republic of Tanzania officially declared Dodoma to become the City to become developed and administered by the Dodoma City Council".

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jambo la kwanza hapa ni Dodoma kutangwaza kuwa Jiji na ilitangazwa na Mheshimiwa Rais tarehe 26 Aprili, 2018 pale Uwanja wa Jamhuri. Alitangaza kwamba Dodoma sasa ni *City* kwa mamlaka aliyopewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili inasema, naomba kunukuu:-

"AND WHEREAS consequent to the declaration of the City of Dodoma by His Excellency JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI, the President of the United Republic of Tanzania, the Government has determined to establish and develop the City of Dodoma as the Capital City of the United Republic of Tanzania". (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapa kuna mambo mawili, kuna suala la kutangazwa Mji huu wa Dodoma kuwa Jiji na kuna suala la kuhamia Makao Makuu ya Serikali. Kwa hiyo, hatuwezi kukwepa kuzungumzia vinasaba mbalimbali vinavyofanya Makao Makuu ya Serikali kama Jiji viweze kutekelezwa sawasawa na kweli dunia iweze kufahamu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sambamba na kutangazwa kuwa Jiji na Makao Makuu ya Serikali na kama nilivyosema kwamba, naunga mkono hii hoja kwa sababu ya mambo kadhaa. Jambo la kwanza tunafanya *decentralization of economy* kwa sababu pale Dar es Salaam pamekuwa na maendeleo makubwa kwa sababu Ofisi zote za Serikali ziliikuwa pale Dar es Salam. Pia kulikuwa na suala la msongamano mkubwa sana wa magari Dar es Salam, leo hii tunavyoleta huu Muswada na kuunda hii sheria, mimi naamini kwamba sasa msongamano ule wa Dar es Salaam ambako Ofisi zote za Serikali, magari ya wafanyakazi na watumishi wa Serikali yalikuwa yako pale Dar es Salaam sasa hivi yatakuwa Dodoma, tutapunguza msongamano pale Dar es Salam, ni jambo jema sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine naomba nizungumze kidogo kwamba tunavyokwenda sasa kuhamia hapa Dodoma rasmi na kwamba tayari imeshatangwaza kuwa ni Jiji kama nilivyosema na kama taarifa hii ilivyoeleza basi tuboreshe miundombinu ya Dodoma. Leo hii ukitembea hapa hapa Dodoma mitaa hii ya *Medeli East*, Chaduru na sisi kwa sababu Wabunge ni wakazi wa Dodoma kwa muda wa miezi saba kwa mwaka, tunaifahamu hii Dodoma, kwa hiyo, tunaomba Serikali sasa sambamba na kuleta huu

Muswada waboreshe miundombinu ya Dodoma. Maeneo ya Chaduru mvua zikinyesha yaani mtu hapiti, gari yake haifiki kule mtaani ni katikati ya mji kabisa. Pia ukija kwenye maeneo yale mengine maeneo ya hapa chini kidogo tu; Waheshimiwa Wabunge wakati ule wa masika gari zao wanaacha karibu mita 200 *then* wanatembea kwenye maji wanaenda majumbani kwao; ni hapa hapa chini tu hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana kwamba hii sheria ikipita tuboreshe miundombinu ya Dodoma kwa sababu kuna wageni wengi sana. Mimi naamini kwamba sasa Makao Makuu ya Serikali yanavyohamia hapa Dodoma sasa hata Mabalozi wote watahamia Dodoma, ni imani yangu hiyo. Nilishasikia humu ndani ya Bunge kwamba wametengewa maeneo ya kujenga Ofisi za Kibalozi, kwa hiyo, tunaamini kwamba kutakuwa na wageni wengi sana. Kwa hiyo, miundombinu yetu sasa ioneshe kwamba kweli ni Jiji lakini Dodoma ni Makao Makuu ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine naomba nichangie kidogo ni suala hili la Wagogo wanaishi Dodoma hapa. Wakazi wengi wa Mji wa Dodoma ni Wagogo lakini hawa Wagogo wakati mwингine wamekuwa, sijui nitumie lugha gani hapa kuzungumza, wanavyopita barabarani, wewe ukiwa unaendesha gari, Wagogo wanataka kukatiza kwenye zile zebra, wanatembea kama hawataki. Sasa hili ni Jambo la hatari sana kwamba hawa Wagogo kwa sababu tunahamishia Makao Makuu ya Serikali hapa Dodoma wapewe elimu. (*Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Nachuma, ni vizuri ukafahamu kwamba Spika naye ni Mgogo pia. (*Kicheko*)

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshmiwa Spika, ahsante. Nilikuwa nazungumza hili maana nina ushahidi sana. Tunaendesha gari sisi Wabunge tukiwa hapa, ukikaribia zile zebra, watu wanakatiza pale zebra wanatembea kama wanaingia ndani. Sasa haina maana kwamba kwa sababu ni zebra basi watu watembee kilonyalonya. Inapofika

kwamba Dodoma inakuwa Makao Makuu ya Serikali, Serikali itoe elimu kwa Wagogo kwamba wahakikishe wanakimbia wanavyokatiza maeneo ya zebra. Pia kwa mujibu wa Sheria za Usalama Barabarani zebra mwisho 12 ikifika usiku watu wanatakiwa wakimbie zebra ili kuepuka kugongwagongwa ovyo.

Mheshimiwa Spika, wapo pia waendesha baiskeli hawajali magari, watembea kwa miguu hawajali magari, tunaomba sana Wizara inayohusika, kwa sababu sasa hivi Dodoma ni Makao Makuu ya Serikali basi elimu iweze kutolewa hawa Wagogo ili wasiweze kugongwagongwa. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo nilikuwa naomba kumalizia katika kuchangia Muswada huu, kwa sababu Dodoma sasa itakuwa Makao Makuu ya Serikali lakini pia ni Jiji basi tunaomba Idara ile ya Ardhi pale *City Council* kama Muswada huu unavyosema ichangamke, kwa sababu hawachangamki. Ukipeleka kuitisha ramani kutaka kujenga nyumba kunakuwa na mlolongo mkubwa na urasimu mkubwa. Mimi naamini ni kwa sababu tu pia hata watendaji wenyewe wale wa Idara ile ya Ardhi na Mipango Miji Dodoma wako wachache, waongezewe kwa sababu sasa wajenzi watakuwa ni wengi Mji wa Dodoma na watu wanahitaji kujenga Dodoma, watu wanahitaji kuitisha ramani zao basi kuwe na kuchangamka, waweze kuongezewa vitendea kazi na *personnel*/iweze kuongezeka ili sasa mambo yaende sawasawa kama ilivyokuwa Mji wa Dar es Salam ambako Serikali inahama kuhamia Dodoma.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makof*)

SPIKA: Shekhe alikuwa anaenda kwenye *border line* namna hii, kidogo tu angeteleza, nakushukuru umeenda vizuri. Mheshimiwa Fatuma Toufiq nilishakutaja na Mheshimiwa Bura atafuata.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa na mimi kuchangia hoja iliyo mbele yetu ya Muswada wa Sheria wa kilitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya mwaka 2018 [*The Dodoma Capital City (Declaration) Bill of 2018*].

Mheshimiwa Spika, kwanza mimi naomba niseme kwa unyenyekevu mkubwa sana kwamba nampongeza sana Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuona umuhimu wa kuleta Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, mimi wakati Dodoma inatangazwa kuwa Makao Makuu, nilikuwa ni mtoto mdogo bado nikisoma shule ya msingi na niliweza kwenda kucheza pale kwenye lile jengo la CCM wakati ule lilikuwa linaitwa jengo la TANU. Leo kwa kweli nina faraja kubwa sana nimesimama hapa nikiwa nina umri wa zaidi ya miaka 55 tunapitisha Muswada huu. Nashukuru sana na nimefarijika sana kwamba leo ninaandika historia kwamba nilipokuwa mtoto mdogo lilitangazwa tangazo hili la kuhamia Dodoma na sasa leo mimi ni mmojawapo wa watunga sheria ambaye nasimamia Muswada huu ili uweze kupitishwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wenzangu wengi wamezungumza kwa kweli upitishwaji au uletwaji wa sheria hii ambayo tutaipisha leo hii utaleta tija kubwa sana katika Mji wetu huu wa Dodoma ambao tunaamini kabisa kwa sasa hivi ndiyo Makao Makuu ya nchi yetu. Ni ukweli usiopingika kwamba Dodoma, kama wenzangu walivyosema, ni mji ambao uko katikati lakini sambamba na hilo Dodoma ni mji ambao mpaka sasa hivi haujawa *polluted* hasa kwenye suala la ardhi kwani maeneo mengi sana yamepimwa, kwa hiyo, hatutegemei *squatters* kama ilivyokuwa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naamni kabisa sheria hii itasaidia zaidi kuendeleza na kuweka yale maeneo yote ya miundombinu ili kusudi Dodoma iwe ina sura tofauti. Naamni kabisa kwa sheria hii itasaidia kuifanya Dodoma

yetu kuwa na sura tofauti kulinganisha na Makao Makuu ya Mji mingine yote duniani. Naamini kabisa kwamba upitishwaji wa sheria hii, wawekezaji wengi sana watakuja kuwekeza hapa Dodoma, kwa hiyo, fursa nyingi zitapatikana, akina mama, vijana watafanya kazi mbalimbali. Kwa hiyo, naomba niungane na wenzangu wote kusema kwamba sheria hii itasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo naomba tu nitoe ushauri, kwamba sheria hii ikipitishwa Serikali itabidi ione ile mipango kabambe ya uendelezaji wa Mji Mkuu wa Dodoma isiwe tena ya miaka mitano, mitano au kumi au 25. Itabidi tuiangalie Dodoma ya miaka 100 inayokuja ili kusudi sasa ile miundombinu itakayowekwa kadri watu wataendelea kuongezeka basi ile miundombinu iwe inatosheleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kulzungumzia katika kuperitishwa kwa sheria hii ni kwamba, tunajua kabisa kuna ule mpango kabambe wa kuikijanisha Dodoma, yaani Dodoma iwe kijani. Kwa hiyo, kutokana na sheria hii, naamini kabisa ile mipango tuliyonayo pamoja na ule mpango wa Ofisi ya Makamu wa Rais wa kuikijanisha Dodoma tukiweka mkakati kabambe wa kuhakikisha kwamba zile Wilaya zote ambazo ziko ndani ya Makao Makuu ya Mji wa Dodoma nazo zikajitahidi kupanda miti kwa jinsi itavyoweza ili kuikijanisha Dodoma itakuwa bora zaidi. Ikiwezekana sasa ule upandaji wa miti kwa mfano wa malengo wa kupanda miti 1,500 ikapandwa lakini uwepo ufuutiliaji wa kuhakikisha kwamba ile miti 1500 yote inamea na inaendelea, hivyo tutawenza kuikijanisha Dodoma. Tukipanda miti ile tufanye ufuutiliaji na kufanya tathimini. Kwa hiyo, naendelea kuipongeza sana Serikali kwa kuweza kuleta Muswada huu hapa leo hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, jambo lingine ambalo nilikuwa naomba Serikali ni kwamba, sheria hii ikipitishwa, kwa kuwa tunataka sasa Makao Makuu yaweze kuendelea kwa haraka Serikali ione namna ya kupunguza bei ya vifaa vyatya ujenzi ili kusudi sasa wale wawekezaji ambaao

wanakuja kuwekeza hapa waweze kujenga majengo mbambali. Si kwa wawekezaji tu bali hata wale wananchi ambao watakuwa na nia ya kuja kuendeleza Dodoma kwa kuweka miundombinu mbalimbali basi Serikali ione jinsi gani itakavyoweza kupunguza bei ya vifaa mbalimbali nya ujenzi ili kusudi wananchi waweze kuendeleza huu Mji wa Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hakika naomba niendelee tena kukushukuru sana kwa kunipa fursa lakini mimi ya kwangu yalikuwa ni hayo, naendelea kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Fatuma Toufiq. Mheshimiwa Halima Mdee, atafuatiwa na Mheshimiwa Felister Bura.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza na mimi naungana na hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani na niseme kwamba na kwenye hotuba yetu tumeandika, hakuna mtu anayepinga kuhamia Dodoma, hakuna mtu anayepinga Dodoma kuwa Jiji. Hoja zetu hapa ni utaratibu wa kisheria, hoja zetu hapa ni mipango ya Taifa kupangwa na itekelezwe kwa mujibu wa Katiba na kwa mujibu wa Mpango ya Miaka Mitano na mwaka mmoja mmoja, hizo ndiyo hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, isije ikajengwa propaganda hapa kwamba kuna mtu ye yeyote anapinga. Kwa sababu sasa hivi siasa zetu zimetoka kwenye hoja zimeenda kwenye vihoja yaani watu wakizungumza hoja inafanyiwa *spin* na kupotosha watu bila sababu za msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru Mbunge wa Mtwara amezungumza huu Muswada hapa una mambo mawili na yamechomekewa *strategically* na nitarudia kusoma. Kwenye *preamble* hapa kuna maneno yafuatayo:-

"WHEREAS on the 26 April, 2018 His excellence JOHN POMBE MAGUFULI, the President of the United Republic of

Tanzania officially declared Dodoma to become the City to be developed and administered by the Dodoma City Council".

Mheshimiwa Spika, hiyo ya kwanza, ya pili, inasema, nanukuu:-

"AND WHEREAS consequent to the declaration of the City of Dodoma by His Excellency JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI, the President of the United Republic of Tanzania, the Government has determined to establish and develop the City of Dodoma as the Capital City of the United Republic of Tanzania".

Mheshimiwa Spika, hii sheria inazungumzia vitu viwili, inazungumzia Makao Makuu na inazungumzia Jiji. Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, sijui mlikuwa mmejlipanga, naona mkawa mna m-crush pale kumchanganya, hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani imesema hivi, hii *document* kuna Jiji hapa na kuna Makao Makuu. Imesema Rais wakati anatangaza Jiji ambalo mmelichomekea hapa kwenye sheria hakuzingatia matakwa ya kisheria, *that was our basic question*. Sasa nyie badala mjadili hoja mmeingia kwenye kichororo cha Makao Makuu, mmekuja mmehalisha Bunge kunyang'anywa mamlaka yake ya kisheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, *it's so unfortunate*, mimi ni Mbunge wa Awamu ya Tatu, Viti Maalum, Jimbo, Jimbo; sijawahi kuona *I am sorry to say that*, Bunge ambalo linapelekwa pelekwa na Serikali kama Bunge hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nina Sheria ya Mipango Miji ya 2007, Sheria Na.8 inasema vigezo vya Jiji, *minimum population 500,000, self sustenance at least 95 per cent of annual budget halafu kuna kipengele cha mwisho kinasema the power to bestow a municipality the status of a City shall be vested in the National Assembly, and this is the National Assembly*. Sasa mtuambie ni lini Bunge hili lilitewa lilitewa Muswada ukainyanya Dodoma...

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, taarifa!

SPIKA: Hebu nikuombe muache kwanza ajikanyage aingie kwenye 18...

MHE. HALIMA J. MDEE: Sawa.

SPIKA: Halafu atajibiwa tu...

MHE. HALIMA J. MDEE: Sawa.

SPIKA: Endelea Mheshimiwa Halima.

MHE. HALIMA J. MDEE: Sawa. Ni lini Bunge hili lilifanya kazi yake kwa mujibu wa Sheria?

Mheshimiwa Spika, nina taaarifa hapa; nyaraka ya Serikali ambao walitoa taarifa kwa umma baada ya hoja kutolewa kwamba jamani, tunakubali kwamba Dodoma ina haki ya kila kitu lakini taratibu zimefuatwa? Wakajibu hapa ukurasa wa pili, kwamba; baada ya maombi haya kuwasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Rais ambaye pia ndiye Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa alitafakari na kujiridhisha kwamba Manispaa ya Dodoma imekidhi vigezo vya kupandishwa hadhi kuwa Jiji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Rais hana Mamlaka *automatic* ya ku-declare kwa sababu *declaration* ni kitu kingine, kuipa *legal status* ni kitu kingine. Rais anaweza akasema, lakini Mamlaka ya Bunge sasa kuipa uhalali lazima itekelezwe. Sasa nilitarajia kwa nia njema kabisa angekuja Waziri hapa na Muswada wake, angesema jamani, tuna-declare Makao Makuu, ndani ya Sheria hii tumechomekea Jiji kuna vigezo moja, mbili, tatu, nne, tano vimefikiwa, hakuna! *We just do politics.* Hapa kwenye maandishi hapa ya Serikali yanaeleza wazi kabisa kwamba ni kweli Rais amesema lakini tutaleta Bungeni, waliileta lini? Haya ndiyo majibu tunayotaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni wajibu wako wewe kulinda heshima na hadhi ya Bunge lako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli hili jambo la Makao Mkuu siyo jipya, amezungumza hapa Mheshimiwa Msigwa mipango. Wakati tarehe Mosi Oktoba, 1973 baada ya referendum kufanyika nchi nzima na kuamua kwamba Makao Makuu ya Serikali yawe Dodoma kulikuwa kuna bajeti kwamba itatugharimu paundi milioni 186 na itachukua miaka 10, mwaka 1973 wakati huo shilingi moja dola ni 0.5

SPIKA: Umesema kitu muhimu sana Halima ambacho Mheshimiwa Msigwa hajui kwamba *there was a referendum*, hajui hilo, endelea. (*Kicheko*)

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, nasema hivi, nchi haiwezi kuendeshwa bila mipango. Mwaka 1973 kulikuwa kuna mpango wa miaka 10, kuna fedha ambayo ilikuwa iko *allocated*, sasa tunataka watuambie wakati wanajibu hapa; hii kuhamisha Dar es Salaam kuja Dodoma namsikia eti Waziri anasema kuna Ofisi, kuna Ofisi wakati wanaweka Ofisi zenu kule *UDOM!!* Sasa hivi watoto wetu watapata mimba, watapata maradhi kwa sababu kuna mchanganyiko wa watu wazima na watoto, hizo ndizo ofisi hizo? *We have to be serious* kuweka mipango ya nchi. Sasa hivi...

SPIKA: Yaani Halima unataka kusema wanafunzi wa Chuo Kikuu ni watoto?

MHE. HALIMA J. MDEE: Kwa hiyo, maana yake unavyosema hivyo unahalalaisha sisi watu wazima kutembea na watoto, siyo? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ninachosema ni hivi, naomba ninukuliwe vizuri, kwamba mipango ya nchi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Tayari Mheshimiwa Halima muda hauko upande wako. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali *at this juncture*, sijui kama una cha kusema?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, ninacho cha kusema. Mwanasheria Mkuu hawezi kuishiwa vya kusema.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi waliotha mchango na kusema kwamba Mheshimiwa Rais alikosea kultamka Manispaa ya Dodoma kuwa Jiji wametumia Sheria ya “*The Urban planning Act of 2007*”.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii siyo sahihi. Nitakwenda tu kwenye utangulizi wa Sheria hiyo ilikusudiwa kwa kazi gani. “*This is an Act to provide for the orderly and sustainable development of land in urban areas*” Hii ni kwa ajili tu ya kuweka mipango na mpangilio mzuri wa matumizi ya ardhi katika maeneo ya mjini.

Mheshimiwa Spika, Sheria sahihi ni “*The Local Government Urban Authority Act*”. Sheria hiyo uende Kifungu cha 5(3) ndiyo kinaeleza Mamlaka hayo yako kwa nani, naomba niisome hii yote; “*Where the purpose sought to be achieved by the order under sub-section (1) is only to confer on an existing Municipality the status of the City that order shall be made by the President*” (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

SPIKA: Ndiyo maana nikamwambia Mheshimiwa Mlinga muache Mheshimiwa Halima Mdee aingie kwenye 18, hoja zake nyepesi sana. Mheshimiwa Bura. Pole sana Mheshimiwa Halima leo maana umeamka vibaya leo. (*Kicheko*)

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bunge hili na namshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema ambayo amenipatia.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana viongozi wa Kitaifa, Mheshimiwa Makamu wa Rais, dada yangu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuhamia Dodoma, nampongeza pia Waziri Mkuu kwa kuhamia Dodoma, lakini nawapongeza Mawaziri wote na Manaibu na Makatibu Wakuu na viongozi wote wa Serikali kwa kuhamia Dodoma. Dodoma ni salama, Dodoma ni kwema, Dodoma ni pazuri na wanafanya kazi katika hali ya hewa nzuri, vyakula *fresh* na hata ukiwaona afya zao zimebadilika kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Rais, Hayati Baba wa Taifa alipotamka kwamba Dodoma ni Makao Makuu tangu mwaka 1973, tamko hili hakulifanya peke yake. Suala hili lilitoka Bungeni na Wabunge waliokuwepo kipindi hicho walikubaliana kwamba Makao Makuu yaye Dodoma na matokeo yake mwaka 1974 wakaanzisha Shirika la Uendelezaji Makao Makuu yaani *CDA*.

Mheshimiwa Spika, Marais wetu waliopita wa Awamu zote walifanya kazi ya kufanya maandalizi ya Serikali kuhamia Dodoma na ndiyo maana hata Awamu ya Nne wakajenga Ukumbi huu kwa maandalizi ya Serikali kuhamia Dodoma. Huwezi kusema kwamba kulikuwa hakuna mipango ya Serikali kuhamia Dodoma, kulikuwepo na mipango na ndiyo maana Serikali ikajenga ukumbi huu wa Bunge na kuhamishia shughuli zote za Bunge Mkoani Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sioni sababu ya kusema kwamba hakuna mipango iliyokuwepo ya Serikali ya Awamu zote kuhamia Dodoma. Mipango illikuwepo na ndiyo maana tukajenga na Ikulu-Chamwino Dodoma na ndiyo maana *CDA* ilikuwa inafanya kila linalowezekana kwa uendelezaji wa Makao Makuu Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kama kulikuwa na shida, tangu mwaka 1973 Watanzania walikuwepo angetokea mmoja akaleta Muswada binafsi kwamba hili la Dodoma sasa haliwezekani lakini Watanzania wote waliunga mkono ndiyo maana tangu mwaka 1973 Watanzania wanasubiri Serikali

ihamie Dodoma. Serikali imehamia Dodoma tuwashukuru na kuwapongeza kwamba maamuzi yaliyosubiriwa kwa muda mrefu sasa yamefanyika.

Mheshimiwa Spika, tunao Wabunge ambao wana Awamu Nne humu ndani, wengine wana Awamu Tatu, wangeweza kuleta Muswada wa kupinga kwamba Makao Makuu imesubiriwa muda mrefu sasa hakuna haja ya kuja Dodoma, lakini wamefurahia ndiyo maana tunajumuika pamoja kushangilia.

Mheshimiwa Spika, niwape taarifa nzuri kwamba Dodoma itajengeka kwa mpangilio mzuri ajabu na wengi ambao wanaona siyo sawa, watakuja na najua nina orodha yao maana mimi ni Diwani. Wameomba viwanja kama hawataki kujenga Dodoma kwa nini wameomba viwanja? Nawakaribisha wajenge Dodoma na ambao wamekwishajenga nyumba zao ziko salama, mali zao ziko salama, kila walichonacho kiko salama.

Mheshimiwa Spika, Dodoma tuna *master plan* nzuri ambayo Dodoma utakuwa Mji mzuri Afrika Mashariki na kati na inawezekana Afrika nzima Mji wa Dodoma utakuwa ni mzuri. *Master plan* iliyokuwepo ikajengwa Abuja imetengenezwa upya na kila siku inafanyiwa marekebisho ili Mji wa Dodoma uwe Mji tofauti. Anayetaka kuwekeza kwa ajili ya viwanda aje tumetenga maeneo kwa ajili ya viwanda, anayetaka kujenga Chuo Kikuu aje, tuna maeneo tumetenga kwa ajili ya Vyuo vikuu, anayetaka kujenga hospitali nzuri za rufaa aje tuna nafasi tumemwekea. Kwa hiyo, msongamano huu wanauona ni wa muda tu, Mji wa Dodoma kutakuwa hakuna msongamano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naipongeza Serikali kwamba wazazi waliokuwa wanafanya kazi Dar es Salaam, wanaondoka saa 11 alfajiri wanarudi saa tano usiku watoto wameshalala, siku hizi familia zao zinawajua kwa sababu Dodoma hakuna foleni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika,...

TAARIFA

MHE. COSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. FELISTER A. BURA: ...Dodoma tunajenga soko la Kimataifa...

MHE. COSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Bura kuna taarifa. Mheshimiwa tafadhalii.

MHE. COSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Spika, ukienda leo Dar es Salaam ukawatafuta Wazaramo huwapati, sasa nataka nishauri tu kwa sababu *speed hili* ya Dodoma inatisha ni vizuri kakatengwa kaeneo kakuwaweka Wagogo wasije wakatoweka kabisa.

SPIKA: *Hansard* futa kabisa hiyo. Mheshimiwa Bura. (*Kicheko*)

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa Mbunge aliyesema kwamba nyumba ambazo zipo na ambazo zime wahifadhi wageni waliofika robo tatu ni nyumba za Wagogo, kwa hiyo hatuna wasiwasi, tuko vizuri.

Mheshimiwa Spika, nimeshangaa na hotuba ya Kambi ya Upinzani ukurasa wa nane, wanasesma; "Halmashauri ya Dodoma hakuna kikao cha Halmashauri ya Dodoma kilichokutana kuazimia kupandisha hadhi Manispaa ya Dodoma"

Mheshimiwa Spika, mimi ni Diwani wa Jiji hili na Baraza la Madiwani liliopita la Serikali ya Awamu ya Nne tuliomba Dodoma kuwa Jiji na ukitafuta taarifa hizo utazipata kwamba tulikwishakuomba na tukapitia hatua zote, tukaenda *DCC* na tukaenda *RCC* na tukapeleka

ALAT Taifa na tukapeleka TAMISEMI kuomba Dodoma kuwa Jiji. Watu wetu siyo hivyo mnavyofikiria, tulikidhi vigezo vyote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wanaposema, waseme kitu ambacho wana uhakika nacho. Mimi ni Diwani wa Jiji hili, najua kilichosemwa na najua tulichokiomba sisi tuliokuwa Madiwani. Kwa hiyo, siyo kwamba Rais amekurupuka tu, lilikuwa ombi toka Awamu ya Nne kwamba Manispaa ya Dodoma tunaomba iwe Jiji.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, taarifa nyingine wanasema kwamba hatujitoshelezi kimapato; kwa taarifa, Rais mwenyewe alisema kwamba Dodoma ndiyo Jiji la kwanza kwa ukusanyaji wa mapato kwa mwaka huu wa fedha uliopita. Kama unabisha tafuta taarifa kwa vyombo vya habari utapata. Dodoma ndiyo Jiji la kwa makusanyo ya mapato, shangilia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunafanya tunachokielewa na tuko tayari kupokea Jiji kwa kufanyakazi, siyo lele mama na niwaambie wananchi wa Dodoma sasa hivi wanafanya kazi kwa...

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, niwatoe hofu wanaohamia Dodoma, waje Makao Makuu kuna neema.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, kuna neema na mwaka huu tunajenga barabara zaidi ya kilomita 100 ndani ya Jiji hili...

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. FELISTER A. BURA: ...tunaboresha miundombinu.

SPIKA: Mheshimiwa...

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, tunajenga Stendi kuu...

SPIKA: Mheshimiwa Bura pokea taarifa.

MHE. FELISTER A. BURA: ...ya kuchukua mabasi 600 kwa mara moja.

SPIKA: Mheshimiwa Bura pokea taarifa.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bura ni Mkristo mwenzangu, tunasali *fellowship* moja, tunaabudu pamoja, kuongea uwongo ni ubaya. Anafahamu fika ni lazima atetee Dodoma lakini aangalie kinywa chake kisijinajisi, kuongea uongo kwa maana kwamba Dodoma ina mapato makubwa kuliko Jiji lolote katika nchi hii ya Tanzania.

SPIKA: Sasa Mheshimiwa Mwakagenda si ungetaja Jiji lenye mapato makubwa kuliko Dodoma!! Lile Jiji la akina Halima Mdee? Hamna kitu. Mheshimiwa Bura endelea. (*Kicheko*)

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, Mwakagenda asiniapishe kwa mambo ambayo hana uhakika nayo na nitamletea taarifa kwa sababu lilizungumzwa na Mkuu wa Nchi siyo leo, nitamwambia. Naomba niendelee kwa sabbau anachosema wala hana habari nacho.

Mheshimiwa Spika, nikwambie kwa Serikali kujiardaa vizuri kwamba tunapokea Makao Makuu...

SPIKA: Hakuna Jiji lenye Meya wa CHADEMA ambalo linaongoza kwa mapato, hakuna. Haya Mheshimiwa Bura endelea.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Niwaambie tu kwamba hatuna shida ya maji, tumejiandaa vizuri na niwaambie magari yote tunajenga *ring roads* ambazo magari hayataingia mjini kwa wale ambao hawataki kuingia mjini, kwa hiyo tumejiandaa vizuri na Serikali imejiandaa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kwamba Dodoma iwe Makao Makuu, tumesubiri kwa muda mrefu, miaka 45 siyo muda mfupi. Miaka 45 ni mtu mwenye watoto kama ni mtu wa kijijini ana wajukuu. Kwa hiyo, Serikali imetimiza yale ambayo Watanzania wote tulitamani yatimizwe. Zamani wanafunzi wakifanya mitihani wakiulizwa Makao Makuu ya Tanzania ni wapi? Wengine wanaandika Dar es Salaam, wengine aanandika Dodoma sasa hivi wataandika jibu sahihi, Makao Makuu ni Dodoma kwa sababu walikuwa hawajui, je, ni Dar es salaam au Dodoma? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mambo mengine kwamba Majengo hayatoshelezi, kwani Wizara wanafanya kazi chini ya mti? Wanafanya kazi kwenye majengo ya Serikali wala siyo ya kukodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwamba Muswada huu umekuja kwa wakati na unafaa na Watanzania wote wanafurahi sasa kwamba anapotoka Arusha anakwenda Mbeya ni siku moja kutoka Arusha kwenda Mbeya kwa sababu barabara zipo za lami na akipenda kulala Makao Makuu, saa nane waliotoka Mbeya wako Dodoma, waliotoka Mwanza saa nane yuko Dodoma na sasa hivi tunejengewa reli ya *standard gauge* watakuwa wanatembea masaa matatu, mawili wamefika Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Muswada huu. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, sana. Mheshimiwa Allan Kiula atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Mtuka.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika Muswada huu. Nami nilipigwa bumbuwazi kidogo, unajua Singida ni kilomita 240 tu mpaka kufika Dodoma sasa nikawa nafikiria kwenda kufuata huduma Dar es Salaam ambako nakwenda kilomita 720 sasa nikaona hilo ni jambo la kushangaza kidogo.

Mheshimiwa Spika, niseme uongozi ni kuonyesha njia na uongozi ni kuishi kwa maneno yako na kwa matendo hilo ni jambo muhimu sana. Sasa Serikali zote zilizopita suala la kuhamia Dodoma lilishapitishwa na uamuzi huo ulikwishapitishwa. Kwa hiyo, ilikuwa ni suala la kufanya maandalizi na muda muafaka ukifika ndipo jambo hilo litekelezwe. Sasa Awamu ya Tano ndiyo muda muafaka umefika, kwa hiyo, hilo nimpongeze Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kulivalia njuga suala hili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hivyo, hata wewe mwenyewe ulisema "Mkutano huu hautakuwepo, nikunukuu mwenyewe "Kama Muswada huu hauataletwa". Kwa hiyo, nikupongeze na wewe pia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ulisema kwa nia njema kwa maana ya Tanzania kwa ujumla wake. Ukiangalia sababu zilizotolewa kuhamia Dodoma jambo moja kubwa ilikuwa ni katikati ya Nchi, sasa sababu hiyo haijabadilika, ipo na itaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, Iakini pia tulitaka huduma, wananchi wapate huduma karibu, tusogeze huduma kwa wananchi. Jambo hilo pia linaendelea kubaki na watu watapata huduma kama kawaida lakini lilikuwa ni so *divested* kwamba Dar es salaam ni Mji wa kibiashara na iko Miji mingi ya kibiashara Arusha, Mbeya, Mwanza ni Miji ya kibiashara sasa tuwe na Mji wa Serikali. Pia usalama wa nchi kwa hiyo, imeonekana Dodoma iko katikati na Serikali itakuwa salama ikikaa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, yako mambo mengi ambayo yamekwishafanyika. Bunge hapa tuko tumeona Bunge

tumekuwa na makao yetu makuu hapa, tunaendelea. Waziri Mkuu alishahamia, Ikulu ilikwishajengwa, Makamu wa Rais yupo, kwa hiyo, suala la *white paper* linakuwa ni suala ambalo halina tija na limepitwa na wakati kwa sababu uko uwekezaji ambao tayari umekwisha fanyika.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunasisitiza sisi ifanye *white paper*, lakini sisi Wabunge tuko mia tatu tisini na ngapi ndio tunaosema *white paper* lakini wananchi ndio shida yao hiyo *white paper*? Wananchi jambo hili wanasubiri utekelezaji wake tu kwa sababu lilishatolea uamuzi. Pia tumeona nchi nyingi zimechukua uamuzi wa kuwa na makao makuu ya Serikali wakahama kwenye miji ile ya zamani. Afrika ya Kusini tumeona, Abuja tumeona, China tumeona. Pia kwa kumbukumbu nzuri ni kwamba, hata Nigeria walikuja kujifunza hapa kabla ya kujenga Abuja, kwa hiyo, hilo lilikuwa ni wazo nzuri ambalo lillonekana kwamba, ni jambo muhimu kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa nikirejea kwenye uwasilisho MUswada, *intent* ya Muswada ni nini? Muswada huu, Muswada unapendekeza kutungwa, nanukuu "kutungwa kwa sheria na kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi". Sasa hilo ni jambo muhimu sana na sisi Wabunge tumekasimiwa nafasi hiyo na madaraka hayo. Kwa hiyo, ni muda muafaka wa kuweza kuunga mkono Muswada huu, tuupitishe na Dodoma iwe Sheria, sheria iwepo na Dodoma iwe Makao Makuu.

Waheshimiwa Wabunge kwa heshima na taadhima kubwa nasema jambo hili, nilifikiri mjalada utakuwa ni mwepesi sana kwa sababu ni jambo ambalo lipo na linaloendelea. Kwa hiyo, ilikuwa ni sisi kukamilisha tu, lakini inatokea kama sintofahamu, sasa sintofahamu isisababishe tukalitia Taifa hili hasara kwa sababu uamuzi ni kwamba Dodoma iwe ni Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa tuliopo humu ndani tumeona Serikali imeweza kuhamia, sasa wakati mwingine uongozi lazima ufanye maamuzi magumu, ni magumu lakini

yanatekelezeka. Kama huko nyuma tulilegalega, sasa yametolewa maamuzi magumu na uamuzi umetekelvezeka, Wizara zote zimekwishahamia hapa, bado Rais tu ambaye na yeze tunamtarajia Mwenyezi Mungu akijalia mwaka huu na yeze aweze kuhamia Dodoma. Kwa hiyo, kumbe basi hata siku za nyuma tungekuwa tumechukua uamuzi mgumu huu tayari Dodoma ingekuwa imeshakuwa na sura nyingine kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Serikali kuhamia Dodoma maana yake sio kwamba Jiji la Dar es Salaam, maana tunapozungumza kuhamia Jiji la Dar es Salaam ndio Makao Makuu yalikuwepo, sio kwamba litadumaa linaendelea na shughuli zake ndio maana mnaona maendeleo ya Dar es Salaam yako pale pale. Bandari inapanuliwa, *flyovers* na barabara zinatengenezwa kama kawaida. Kwa hiyo, Tanzania yetu na yenyewe sasa inanufaika na Serikali kuhamia hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi ni jukumu letu sisi kuweza kutambua ukweli, ukweli ni nini? Ukweli ni kwamba uamuzi wa kuhamia Dodoma ulikwishafanyika, sasa sisi tukamilishe tu hilo jambo, lakini kwa manufaa yetu sisi Watanzania wa sasa hivi na wa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na naomba Wabunge wenzangu tuweze kuunga hoja hii, ili Dodoma iwe Makao Makuu kikamilifu kwa sheria. Naomba kuwasilisha. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Daniel Mtuka

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii angalau nitoe mchango wangu mfupi, mengi yameshazungumzwa na wenzangu sitataka kuyarudia sana. Niseme tu nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa maamuzi haya sasa ya kutushauri Wabunge kwa maana ya kuleta sheria hii sasa ya kubariki jambo hili sasa liwe rasmi maana limeanza tangu mwaka 1973.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo niseme tu kwa ufupi kwamba, naunga mkono hoja hii, mjadala ulioko wa kubariki hii *declarationsasa* ya kulitangaza jiji hili sasa kuwa Makao Makuu ya nchi. Kwa sababu zifuatazo chache tu wenzangu wamezigusia, niseme tu kwamba ndugu zangu, niwaombe na Watanzania wote, kwanza wamekuwa wakisubiri kwa hamu sana ujio wa jiji hili sasa kisheria. Tujiandae kisaikolojia, sasa Dodoma itakuwa makao makuu, najua Sheria hii inapita.

Mheshimiwa Spika, tunatamani sana Jiji hili kama ambavyo amesema dada yangu Mheshimiwa Bura, Jiji hili sasa tujiandae kisaikolojia kwamba tunataka tuandae jiji ambalo kwa kweli liwe mionganini ya majiji katika dunia hii ya kutolea mfano. Ibara ya tano (5) ya Muswada huu inasema kutakuwa na sheria itatungwa rasmi itakayoongoza namna ya kuendesha jiji hili. Naomba sana Sheria hii ikishapita hii isichelewe kutungwa kwa maana ya *ku-manage* namna ya kuliendeleza jiji. Sisi watu wa Mipango Miji tunatamani sana sheria ije hii jiji hili liandaliwe katika utaratibu unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, tumezungumzia, zipo sheria za mipango miji sawa zitatumika katika kuliendeleza jiji hili, ningetamani sana, kwa mfano *master plan* iliyopo au mpango kabambe wa kuendeleza jiji hili upo lakini ungehuishwa pia kidogo. Likae jopo la watalaanam, watalaanam wa Mipango miji na watalaanam wa ardhi kwa pamoja wajadili na waweke utaratibu mzuri sasa wa kuhuisha mpango huu, uwe mzuri zaidi wauboreshes zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumeona maeneo mengine ya nchi nyingine duniani, kwa kweli wana mipango mizuri sana ya uendelezaji wa majiji kama haya. Tunatamani sasa kwa mfano maeneo ya makazi yaye ya makazi, lakini tunatamani maeneo ya kibiashara yaye ya biashara, tunatamani maeneo ya maofisi yaye ya maofisi, kuwe na mji wa viwanda. Mimi nilikuwa Rwanda juzi, nashukuru tulikuwa tumeenda kujifunza kule kwa wenzetu.

Mheshimiwa Spika, umetembezwa ule mji, kuna mtaa kabisa wa viwanda, unatembea huwezi kuona maeneo mengine, ni mji ule tu ndio viwanda. Kwa hiyo, natamani sana Dodoma tutengewe eneo kabisa sasa unaenda kutembea viwandani kule, hatutaki kuona mchanganyiko huo mara maji machafu hapa, harufu sijui nini, hapana tunataka tuwe na vitu hivi vitengwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tunatamani kuwe na eneo la masoko mazuri, tunatamani tuwe na eneo la maegesho la magari makubwa na madogo, tunatamani tuwe na stendi kubwa imeshaanza kujengwa, stendi ndogo ya magari madogo, bandari kavu iwepo, tunatamani *airport* kubwa iwepo. Mji wa kielemu kwa mfano kama ambavyo tayari maeneo yameshapangwa uwepo, maeneo ya starehe, tuwe na bustani nzuri kama wenzetu walizonazo.

Mheshimiwa Spika, kwenye huduma za barabara tuwe na *high ways, ring roads*, tuwe na *by pass*, hatutaki magari makubwa hapa katikati ya mji. Tunataka mji ambaao umetulia uko vizuri. Tuwe na *flyovers*, baadaye tuandae na zile *provision za fly over*, mji huu unakuwa. Tusianze tena baadaye kubomolea watu tunataka *flyovers* hapana ule mpango uonyeshe. Pia huduma tuwe nazo madhubuti, tuwe na vyanzo vya uhakika vya maji kwa mfano Mzakwe ile itazidiwa, Farukwa lile bwawa lile liharakishwe kujengwa ili tuwe na huduma nzuri ya kutosha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini tuwe na huduma ya umeme ambaao ni wa uhakika, *stable and reliance power*, lakini tuwe na utaratibu mzuri wa *waste management*, takataka zinasumbua sana kwenye miji lakini kwenye *plan ile* ionyeshe *s,torms water management* tuwe na Dodoma hii ni *plain area* hii, ni bonde la ufa hili tuwe na utaratibu mzuri wa *manage* maji haya ya mvua yanasumbua kwenye mvua kubwa mafuriko Dar es Salaam imekuwa imetufundisha sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini natamani pia Dodoma tuwe na kasi ya upimaji wa viwanja na ugawaji wa viwanja hasa

site and services. Pima kiwanja, peleka maji, peleka umeme, peleka huduma zote gawa kiwanja, watu wajenge. Vilevile Waziri wa Ardhi atusaidie sana na wote wanaosimamia mambo ya sheria, *land speculation* inatusumbua sana mtu ananunua kiwanja kwa ajili ya mjukuu?. Kinabaki kichaka katikati ya mji, hapana watu wajenge kwa muda unaotakiwa, tunataka jiji hili liwe limejengwa vizuri. Pia Dodoma tukubali kwamba ni eneo la mkondo wa matetemeko. Watalaaam watushauri na wala sijengi hofu lakini tuwe na tahadhari hiyo kwamba, tuwe na nyumba za ghorofa zisiwe ndefu sana, ziwe *standard*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia ningependa mfano wa majengo kwenye majengo ya makazi, tunataka kwa mfano kama *block* nzima hivi iwe na ghorofa tatu iwe na rangi labda bati rangi nyekundu ziwe nyekundu, kama rangi nyeupe ziwe nyeupe na urefu uko sawa sawa, maeneo kama hayo, yaani ule mfanano wa uzuri ule inaleta pitcha nzuri ya mji.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho niseme tu kwamba wakazi wa Dodoma na Watanzania kwa ujumla wanaojenga hapa tuijandae kisaikolojia kwamba, sasa tukubali huu ni mji sasa mambo ya kufuga sijui ng'ombe katikati ya mji sijui, usafi wa mazingira yaani tuijandae. Dada yangu Mheshimiwa Bura amesema kupanda miti, tupande miti tupendezeshe jiji letu hili tuijandae kisaikolojia kwamba sasa ni Jiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia maeneo ya jirani na Dodoma tuijandae pia, kwa mfano Manyoni pale mimi ni karibu. Manyoni na Bahi ni karibu lakini Manyoni ni nzuri zaidi kwa sisi kujandaa zaidi kwa sababu Bahi kidogo haiko sawasawa, sisi pale tunalima, pamenyanyuka pale tunaweza tukapima pale watu wanakuja kupumzika pale. Manyoni ni juu ya Bonde la Ufa.

Mheshimiwa Spika, ukijenga hoteli pale juu ya bonde la ufa pale juu, unaliangalia bonde la ufa chini, watu wanaweza kuja kupata mahali pazuri sana pa kupumzika. Tuna eneo kwa mfano pale Kilimatinde, ukipanda pale

Kilimatinde kuna sehemu inaitwa ukanda wa juu. Ukipiga mahoteli pale, ukiangalia lile bonde yaani mpaka maisha unaona yanaongezeka unapata burudani kilionna bonde, uwanda ule safi. Kwa hiyo, Manyoni tujiandae sisi pia maeneo ya karibu karibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii hoja, huu kwamba sasa tunataka kuufanya *declaration* naiunga mkono sana. Naiunga mkono na kwa kweli na kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene amesema kwamba, ni baraka na ni ibada kubwa sana kubariki juhudzi za Mwalimu Nyerere ambazo alizianzisha kwa kweli tunapata thawabu kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, naomba tu tuunge mkono Muswada huu Wabunge wote jambo hili ni jema, yametokea mambo, sisi sio malaika lakini jambo hili ni nzuri, hilo ndilo jambo la msingi. Hoja ya kusema Zanzibar haikushiriki tuna kamati, Kamati za Bunge za Kudumu tunao Wazanzibari, tumejadili kwenye kama lakini hapa Bungeni tuna Wazanzibari wenzetu...

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, ni kengele ya pili

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Spika, sawa namalizia, tunao Wazanzibari wenzetu wameshiriki kwenye jambo hili. Kwa hiyo sio kwamba Wazanzibari hawakushirikishwa. Sisi ni watungaji wa sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba sana kuunga mkono hoja. Nashukuru kwa nafasi hii. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Omary Badwel, Mbunge wa Bahi

MHE. OMARY A. BADWEL: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nichangie japo kidogo katika Muswada huu wa kutambua rasmi kwamba Dodoma sasa ni Makao Makuu. Kwanza nichukue nafasi kama walivyotangulia Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuamua sasa kutekeleza rasmi jambo

letu ambalo limekuwa kwa miaka mingi halijatekelezwa na sasa Serikali yote imeshahamia rasmi hapa Dodoma na yeye mwenyewe ameahidi kuja hapa Dodoma hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza sana Wizara kwa kuleta Muswada huu mzuri ambao kwa kweli umekuwa ukisubiriwa kwa muda mrefu na hatimaye leo umeingia hapa Bungeni naamini baada ya hapa sasa Dodoma ni rasmi kwamba, ni Makao Makuu ya Nchi yetu na hakutokuwa na kitu tena cha kuyumbisha makao makuu haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia ya kutoa ushauri kidogo kwa sababu napongeza hatua Dodoma sasa kuwa jiji na Mheshimiwa Rais ametangaza na sisi watu wa Dodoma tumepokea na tumefurahi sana. Hata hivyo, nataka nishauri tu kwamba, tukiangalia katika haya majiji liko Jiji la Dar es Salaam lina Manispaa tano sasa, nadhani kama hivyo, lakini kuna Jiji la Arusha lina Manispaa moja, Jiji la Tanga Manispaa moja, Mwanza Manispaa mbili, lakini Dodoma sasa inaonekana bado kuna manispaa moja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya kupitia sheria hii ya Dodoma sasa kuwa makao makuu, tunataka kujua nini kitafuata? Tunaweza kuwa Halmashauri zaidi ya moja kwa maana ya Manispaa. Hii nadhani itasaidia sana kuleta maendeleo kwa haraka, kwa sababu leo ukienda pale ofisi ya ardhi Dodoma hata hospitali sidhani kama kuna watu wengi kama pale. Maana watu wameamka, watu wameamua kujenga hapa Dodoma lakini inaonekana ofisi zile zinalemewa lakini naamini kama tukiwa na Manispaa mbili zikagawanyika.

Mheshimiwa Spika, kwanza zitasaidia urasimu kupungua lakini hata usimamizi wa ujenzi wa miundombinu na mipango kwa upande mmoja utakuwa unapanga mipango yake na upande wa pili unapanga mipango yake, Dodoma itaendelea kwa kasi sana. Nadhani tuangalie pia mfumo huu wa Jiji moja na kuwa na Manispaa moja huko mbele tuone vizuri kama tunaweza kuwa na manispaa zaidi ya moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, najua tunapitia upya *master plan* yetu ya Mji wa Dodoma na ni vizuri kweli kuipitia kwa sababu jambo la miaka 45 iliyopita huwezi kulinganisha na leo. Nataka niseme tunashukuru sana kwamba jambo hili limechelewa, ukiangalia kama jambo hili tungekuwa tumelipitisha mwaka huo sabini na kitu leo tungekuwa na mbanano mkubwa wa Dodoma hapa lakini, kwa sababu wakati ule mwamko wa kimaendeleo watu wengi walikuwa bado hawajui nini kitatokea.

Mheshimiwa Spika, mfano, leo kuna barabara ya sita, barabara ya saba, ya nane, ya tisa mpaka barabara ya kumi na mbili tumeamua sasa zigeuzwe iwe barabara za njia moja, kwa sababu zilikuwa *planned* zamani na watu walikuwa hawafikiri kwamba labda kutakuwa na magari mengi kama sasa. Hata hivyo, leo hii kwa uelewa mkubwa tulionao na watalaan wetu wapo, najua wameiweka Dodoma sasa miaka 1000 ijayo, kwa maana kwamba watai-*plan* Dodoma sasa hata kama sisi tumeondoka miaka 50, miaka 100, miaka 200 watu wasitulaani sisi kwamba, hawa nao walio-*plan* wali-*plan* vibaya leo tumebanana.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia wenzetu kwenye hii Master *Plan* waipitie lakini wa-*plan* vizuri, hata kama hatuwezi kujenga barabara za njia sita kwa maana ya tatu huko, tatu huku lakini tuweke eneo ambalo linakubali huo ujenzi baadaye, hata kama leo tutajenga barabara moja, lakini kesho ikitakiwa mahitaji ya barabara mbili liwe eneo lile lile, barabara tatu eneo hilo hilo, kwa sababu itusaidia sana kupunguza msongamano lakini pia kujenga mji wenye ramani ya kutosha wakati huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia tunataraja Dodoma kuwa mji wa kisasa, mzuri utakaopendeza, kwa hiyo tunawapa kazi hiyo watalaan wetu kutembelea hata miji mbalimbali kujifunza kuona wenzetu wamefanya nini, walikumbana na changamoto gani, wamefanikiwa wapi ili haya yote mazuri wayalete hapa Dodoma na zile changamoto waweze kuziepuka mapema ili kwa kweli Jiji la Dodoma liwe zuri na liwe endelevu ambapo ukitaka kufanya jambo lolote

unaendeleza kutokea pale ulipokuwa, unasonga mbele kuliko kufikiri kuanza kulipa fidia na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nikiangalia hapa Dodoma leo tunaitangaza kuwa Makao Makuu lakini Ikulu iko Chamwino. Sasa nataka nipate pia maelezo kwa sababu Ikulu iko Wilaya ya Chamwino sasa Makao Makuu haya Ikulu iko pembedi labda tuambiwe na yenye, Chamwino kipande kile kinakuja huku Dodoma au kitabaki kule kule ili tuweze kujua sasa Mheshimiwa Rais tunakaa naye hapa Makao Makuu au tunakaa naye wapi?

Mheshimiwa Spika, vile vile nafikiri hata eneo la Mabalozi liko huko Dodoma, liko eneo la Dodoma lakini eneo la Ikulu liko Chamwino. Kwa hiyo, nadhani na hilli nalo pia tupewe maelekezo yake kwamba, sasa Chamwino inabaki kuwa Ikulu kule kule Chamwino au Chamwino inarudi kuwa Dodoma kwa maana ya marekebisho ya mipaka kwa eneo hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hapa sasa watakuja watu wengi sana kwa maana ya uwekezaji, lakini ukiangalia katika eneo la uwekezaji bado tuna urasimu mwangi sana. Tunakutana na wawekezaji wengi sana wanalalamika hapa, wanalalamika pale mambo yanachukua muda mrefu na wengi wanapenda kujenga Dodoma. Kwa mfano juzi tu tulikuwa tunakagua viwanda, wale wenye viwanda wengi wanasema sisi tunataka kuja kujenga Dodoma lakini bado tunasumbuliwa eneo, bado hatujapata.

Mheshimiwa Spika, tukashangaa sana kama tumeshatangaza Dodoma ni Makao Makuu na wako watu wanataka kuja kuwekeza Dodoma hususan viwanda na kadhalika lakini bado wanalalamika urasimu uliopo hapa. Nilidhani Serikali ingeliangalia hili jambo kwa upekee sana. Kama kweli tunataka Dodoma ikue haraka tutafute mbinu nzuri ya kuwafanya wawekezaji na watu wengine wanaotaka kuja kuwekeza Dodoma maeneo mbalimbali waweze kupata maeneo kwa urahisi, muda mfupi na kwa kweli tuwasaidie kuhakikisha wanafikia malengo yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tukiwa na makao makuu ambayo hayana hata maeneo ya utalii, maeneo ya burudani itakuwa ni ajabu sana, kwa sababu mji huu sasa utapokea watu wa nchini mwetu, utapokea watu wa kimataifa, watapenda kuja kuona vitu mbalimbali. Sisi Wagogo tuna tamaduni zetu nadhani tutafute mahali ambapo pia tutaweka utamaduni wetu wa kabilia la Wagogo ili watu waweze kuja kujifunza kwa sababu Dodoma ndio makao makuu. Hata kama hawa watani zetu wanatutaniatania lakini tunawaambia sisi tutabaki hapa hapa, hatupotei na tuweke utamaduni wetu hapa katikakati ya mji ili mtu akija aone kwamba, Dodoma Wagogo wapo na wanaendelea kufanya kazi zao kama Wagogo, najua hili utaniunga mkono vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maeneo ya utalii pia, tuna mbuga zipo jirani jirani katika Wilaya ya Kondoa na Wilaya zingine hapa zilmashirwe hata kama zitakuwa ni mbuga za kutengenezwa kwa kuangalia hali ya hewa na kuhamishia wanyama ambao wako kwenye maeneo mengine ambayo wanaweza kukubali hali ya hewa hapa Dodoma, ni vizuri kwa kweli Serikali ikaone utaratibu wa kuhamishia hao wanyama. Kwa sababu tutakuwa na Mabalozi na wageni wa nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, nina hakika wageni hawa wote wangependa kuona wanyama wetu, wangependa kuona tamaduni zetu na Dodoma itapendeza kwa kweli ikiwa na vitu mbalimbali mchanganyiko, sio tu Makao Makuu ya Serikali na sisi kuhutubia, lakini pia kuwe na vitu ambavyo tukishawahutubia wanakwenda pia baadaye kuangalia mambo mbalimbali ambayo yatawaliwaza na yatawafanya waendelee kuipenda Dodoma.

Mheshimiwa Spika, lakini mahotelii vile vile makubwa na ya kisasa, tutafute namna ya kutenga maeneo mazuri na kuwashawishi wenzetu ambao wanaweza kujenga mahotelii mazuri, yuko mtu anaweza akaja Dodoma hapa akasema mimi hapa hata hotel moja silali. Anataka hotelii ya nyota tano, nyota ngapi, kwa hiyo lazima haya mambo yote tuyaangalie sana sasa ili tuweze kushawishi watu.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia mpango wa kujenga *airport* yetu. Sasa Mheshimiwa Rais akihamia hapa na Marais wengi watakuja, wengine wanakuja ndege zao kubwa hawawezi kutua hapa Dodoma, sasa sijui itatakiwa Mheshimiwa Rais akawapokee tena Dar es Salaam. Kwa hiyo, na hili jambo pia la uwanja nalo lipewe kipaumbele, ikiwezekana Mungu akipenda bajeti tunayokuja kupitisha mwakani kwa mwaka wa fedha unaokuja, tuone pia mipango ya ujenzi wa kiwanja kikubwa na cha kisasa cha ndege hapa Dodoma ili wageni wetu mbalimbali wanaokuja, mashirika mbalimbali ya kimataifa yaweze kuvutiwa pia kwamba sasa yanakwenda Dodoma lakini yatapata mahali pa kutua na sio waje Dar es Salaam wabadili ndege na mambo kama hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naunga mkono hoja hii, naunga mkono Waheshimiwa Wabunge wote, lakini nataka nimwambie Mheshimiwa Mtuka Bahi ipo karibu zaidi kuliko Manyoni. Maana yake alipokuwa anasema hapa Bahi haijakaakaa vizuri, namwambia Bahi pamekaa kaa vizuri na Bahi ndio itakuwa sehemu ya kupumulia mji huu utapokuwa umejaa, kwa sababu Bahi na Mjini hapa ni karibu sana, kwa hiyo Mheshimiwa Mtuka angoje kwanza Bahi ikamilike halafu tutakuja Manyoni, lakini kwanza ukitaka kwenda Manyoni lazima upite Bahi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tutaendelea jioni na mjadala wetu, lakini kwa sababu sitakuwepo hapa nichukue nafasi hii, kuipongeza sana Serikali kwa kuleta jambo hili ambalo tumelilia kwa muda mrefu sana sana sana, *at last* jambo hili linafanyika. Kwa kweli katika *legacy* na *land marks* ambazo Mheshimiwa Rais wetu Dkt.John Pombe Joseph Magufuli ambazo ataziacha mojawapo ni jambo hili. (*Makofi*)

Wako waliofafuta sababu za msingi, za kuhamia Dodoma na kadhalika na zimetajwa nydingi, lakini iko moja ambayo hatui-re-emphasize nayo ni ya sababu za kiulinzi na

kiusalama. Dodoma inavyozidi kujengwa *deployment* ya kiulinzi na kiusalama iko sawa sawa, itoshe tu kusema hivyo. Lakini kama nchi hapa sasa tuko sawa sawa, kule tulikuwa sebuleni sana. (*Makofi*)

Kwa hiyo tunamshukuru sana sana Mheshimiwa Rais, tunamwombea kwamba kabla ya mwaka huu kwisha na yeze aweze kuhamia hapa Dodoma, sote tuweze kuwa hapa Dodoma na kwa uamuzi huu shughuli za Bunge zitabadiika, huko tunakoenda. Hata taratibu zetu zitabadiika, kwa sababu Bunge liko Dodoma na Serikali iko Dodoma si lazima tena tuendelee na taratibu ambazo tulikuwa nazo hizi za kuja na kuondoka, kuja na kuondoka labda tutaingia utaratibu wa kuwepo Bungeni muda wote kama wenzetu.

Tukawa tunaenda likizo kama wafanyakazi wengine kwa hiyo ikabidi Waheshimiwa Wabunge mnapokuja Dodoma mhamie pamoja na paka wenu na mbwa maana yake mtakaa muda mrefu sana. Kwa hiyo, tunaishukuru mno Serikali, tunaishukuru sana kwa jambo hili, natumaini tutaunga mkono kwa kiasi kikubwa sana.

Kwa hatua hiyo basi naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja leo jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilitishwa hadi saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia)

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alkalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na wachangiaji wetu tuanze na Mheshimiwa Saada Mkuya.

MHE. SAADA S. MKUYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata fursa hii ya kuchangia Muswada huu ulioko mbele yetu na nachukua fursa hii kuipongeza sana

Serikali kwa kuleta Muswada huu hapa Bungeni na mimi nikiwa mmoja wa Wajumbe wa Kamati hii. Huu ni Muswada ambao comprehensively tumeu-*discuss* na kutoa maoni yetu na tuko *proud* kwamba maoni yetu mengi yemechukuliwa na Serikali na yamepelekea kutengenezwa ama kuchapishwa upya kwa Muswada huu wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mawili makubwa, kwanza kuhusiana na wadau ambao wametakiwa kutoa maoni yao katika Muswada huu wa sheria. Nadhani muda ufike sasa tuone umuhimu wa ushirikishwaji wa wadau wengine mbali ya Serikali ambao wanatoka katika upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mfano katika Muswada huu wa sheria umejadiliwa kwa kina vilevile na wadau ambao sio Serikali kwa mfano TAMWA, Tanganyika *Law Society* na wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa upande mwininge kwa Zanzibar na hao wadau vilevile wana *exist* tuna Zanzibar *Law Society* na wengine ambao pengine wangeweza na wao kutoa maoni yao ili kuona Muswada huu unaboreshw zaidi. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo lazima sasa tufike tuone kuna umuhimu wake wa kushirikishwa wadau wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, Muswada huu kwa sababu ni Muswada ama sheria hii sasa ni sheria ambayo inakwenda vile vite kutengenezwa muunganiko wa kazi mbalimbali za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakuna namna nyininge isipokuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au kazi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar vilevile mara nyangi ziwe wana-*coordinate* na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii iende sambamba na uboreshwaji wa miundombinu iliyopo hususanii usafiri, kwa upande wa Zanzibar kuja Dodoma ukitaka kumtuma Afisa kwa mfano aje Dodoma labda ku-*attend* kikao cha masaa mawili au matatu ni lazima apate *per diem* ya siku tano, kwa sababu anapoondoka Zanzibar anaondoka leo, yaani tukitaka kufanya kikao leo ina maana Mjumbe kutoka

Zanzibar aondoke Zanzibar kama juzi ili alale Dar es Salaam halafu achukue basi aje Dodoma, kesho yake ndio ashiriki kikao halafu alale pengine Dodoma na baadaye aende Dar es Salaam, akiwahi boti sawa, hakuwahi inabidi alale Dar es Salaam kabla ya kwenda Zanzibar. Kwa hiyo, kwa upande mwingine inaweza ika- *increase cost* ya *operation* kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa utangazwaji huu wa Jiji la Dodoma uende sambamba na uratibu wa shughuli nyingine kama za usafiri kuona kwamba tunapata ile *effectiveness* hasa ya utekelezaji wa mipango mizuri sana ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Tunaomba Shirika letu sio tunaomba nadhani hili lazima liwe linafuatana na hii sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika letu la ndege la *Air Tanzania* liwe na *connection* kutoka Zanzibar mpaka Dodoma inawezekana kabisa ikawa kwa wiki mara tatu, lazima iwe hivyo ili tuweze sasa kupata yaani ile ladha ya Muungano ndio ioneckane kwa sababu tutakuwa sasa zile kazi zinakuwa zinakwenda kila siku, lakini vilevile kutakuwa kuna *facilitation* za kuhakikisha kwamba ushiriki wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kazi mbalimbali katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinafanyika *effectively* bila ya kuongeza gharama kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hili ningeomba sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile inawezekana huu usafiri ni usafiri wa ndege, tunaweza vilevile kuhuisha hata usafiri wa boti ikawa badala ya boti kuondoka saa tisa nusu kutoka Dar es Salaam kwenda Zanzibar tukaongeza muda wa kuondoka kwa ajili ya ku-*catch* up wale wasafiri ambao wanatoka Dodoma wanakwenda Zanzibar. Kwa sasa hivi usafiri huo umekuwa ni shida sana, inabidi lazima kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ku- *incur extra cost* kwa ajili ya kuweza ku-fit in katika *process* za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo kwa sasa hivi zipo Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu yalikuwa hayo machache na nataraji sana Serikali itayachukua na itayazingatia ili kuona kwamba tunapata sana sasa ile ladha ya utekelezaji wa Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kama kutaangaliwa vizuri Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ametangaza Dodoma kuwa Jiji *basically* siku ya tarehe 26 Aprili kwa *indicate* ni siku ambayo tunasherehekea Muungano wetu, kwa hivyo tuone umuhimu utangazwaji wa Jiji hili, umuhimu wa siku iliyotangazwa Jiji hili lakini umuhimu wa utekelezaji wa kazi za Serikali zote mbili katika kuhuisha na kuudumisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Namwita Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta akifuaatiwa na Mheshimiwa Seba Bilakwate.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nichangie katika huu Muswada wa Sheria ya Kutangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi yetu ya Tanzania. Awali ya yote naomba nitoe pole kwa wazazi walioondokewa na watoto wao yaani wanafunzi waliopigwa na hata kufariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya *TWPG* natoa pole nyingi lakini wakati huo huo tunatoa wito kwa Walimu kuwa waangalifu wanapotoa adhabu kwa wanafunzi hawa kwa kuzingatia kwamba wao pia ni wazazi, walezi lakini wakati huo huo kazi ya ualimu ni wito basi watumie taratibu nzuri za kuwaadhibu kutohana na taratibu zilizopo, tunaomba Mwenyezi Mungu aweke roho za Marehemu mahali pema peponi. Amina. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Muswada uliopo mezani la kwanza kabisa naomba niipongeze Serikali kwa uamuzi wake wa kuleta Muswada huu hapa Bungeni.

Kipekee naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa uamuzi wake alioufikia hadi kufikia hatua hii ya kutengeneza Muswada ili Dodoma kuwe Makao Makuu ya nchi yetu ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mfano na nasema kwa dhati mimi mwenyewe, huu ni mfano mzuri wa kiongozi kuwa na maamuzi. Naamini ukienda kwenye ofisi nydingi utakuta mafaili karibu yawafunike na Maafisa wenyewe, sio kwamba wana kazi nydingi, wanashindwa kuamua. Huu uwе ni mfano wa sisi viongozi kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marehemu Samwell Sitta mume wangu, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi, yeye pamoja na marehemu Sir George Kahama walikuwa ndio viongozi wa kwanza Watendaji Wakuu wa Mamlaka ya Ushawishaji Makao Makuu mpaka wamefariki bado hakuna kitu chochote kilichotokea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiangalia kwamba kama tangu mwaka 1973, Mheshimiwa Nyerere marehemu Mungu naye ailaze mahali pema peponi roho yake, mwaka 1973 alitamka mpaka leo hii bado tunajadili jambo hili. Hii inanipa fundisho gani? Inanipa fundisho kwamba sisi viongozi ambao tunachukua nafasi ya wale waliotutangulia ni vizuri tukaangalia mambo gani mazuri waliyoyafanya, lakini mambo gani hawakumaliza tuyamalizie sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Magufuli, Rais wetu kwa kuangalia viongozi waliomtangulia walifanya nini, kitu gani hawakukamilisha yeye anakamilisha, ndio unaona uamuzi wa Makao Makuu ya Dodoma, unaona *Stiegler's Gorge* safi kabisa. Nimejifunza kwamba kama viongozi lazima nifanye maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejifunza pia mambo mengine, sisi Watanzania sio wote, wako baadhi ya watendaji ambao kiongozi akitoa tamko juu ya uamuzi fulani

hawamtengenezei mazingira ili ule uamuzi utekelezeke. Nina mfano hata nikiulizwa naweza kuelezea, iko mifano mingi ya matamko mazuri tu ambayo Marais wetu wametamka lakini watendaji baadhi yao wamehakikisha kwamba ule uamuzi ufanyike hivyo. Labda ni hapa kwetu tu, lakini nadhani kitu kizuri ni pale ambapo baada ya kiongozi kutamka jambo, watendaji wao ni kumtengeneza mazingira ili lile tamko lake liweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiri, kwa hiyo, nachukua nafasi hii kuwashukuru sana wote watendaji Wizara nzima zilizohusika zote mbili TAMISEMI, Katiba na Sheria na wote waliohusika kuhakikisha kwamba wanamsaidia Rais wetu ili tamko lake lianze kufanya kazi, nawapongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe labda kitu kimoja tu, kwa kuwa Dodoma ni katikati na hilo halina ubishi na uamuzi ulishafanyika, niiombe Serikali sasa ihakikishe kwamba njia zote kutoka mikoa yote pamoja na jitihada nzuri iliyofanyika na Serikali yetu kuweka nyangi lakini bado iangalie ni maeneo gani ya mikoa gani ambayo si rahisi wao kufika Dodoma ambapo wataweza kupata huduma wanayoitaka ya ngazi ya kitaifa. Kwa hiyo, ombi langu ni hilo, lakini kwa kifupi tumejifunza na nitaendelea kujifunza kwamba ukiwa kiongozi fanya maamuzi, usiogope kama kuna changamoto utazirekebisha kadri mambo yanavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema naunga mkono taarifa yote ya Kamati yangu ya Utawala na TAMISEMI pamoja na Muswada mzima, hoja nzima iliyowekwa mezani naiunga mkono. Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Margaret Sitta. Mheshimiwa Bilakwate atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil Mwambe.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu muhimu wa kuifanya Dodoma kuwa Makao

Makuu. Awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa nguvu na afya kuwepo Bungeni hapa na kujadili mambo muhimu kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kweli Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli amekuwa na shujaa anafanya maamuzi ambayo ni magumu. Wenzetu walikuwa mara nyingi wanasema tunataka kiongozi atakayefanya maamuzi magumu na hakika Dkt. Magufuli amewajibu kwa maamuzi magumu, jambo ambalo limekaa tangu mwaka 1973 leo anaibuka mwaka 2018 kulifanyia maamuzi kwa kweli ni jambo la kupongezwa na niwaombe wenzangu upande wa pili wasione aibu kupongeza katika hili kwa kweli kile ambacho walikuwa wanakililia leo amewajibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada ni muhimu sana Dodoma kuwa Makao Makuu kwa kweli napongeza, nipongeze Wizara ya TAMISEMI chini ya Mheshimiwa Jafo kwa kulisimamia hili kwa kweli nawapongeza sana. Kuna watu ambao wamekuwa wanasema haya mambo ni mambo ya kukurupuka, niseme kwa kweli Serikali hajakurupuka. Jambo ambalo tunaweza kusema ni kwa kweli lilichelewa lilitakiwa lifanyiwe maamuzi miaka mingi, lakini Dodoma kuiandaa kuwa Makao Makuu halikuanza sasa hata hili jengo la Bunge ilikuwa ni sehemu ya maandalizi kuiandaa Dodoma kuwa Makao Makuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Dodoma inakuwa Makao Makuu, Dodoma ukija kuangalia iko katikati ya Tanzania, lakini maandalizi mengine ambayo niendelee kuipongeza Serikali ukija kuona barabara zinazounga Mkoa wa Dodoma, zinazounga nchi nzima kuja Mkoa wa Dodoma asilimia nafikiri zaidi ya 99 zinapitika kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo hii ilikuwa ni sehemu ya kuiandaa Dodoma kuwa Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine sisi tunaotoka Kanda ya Ziwa kama kule Kyerwa mtu alikuwa kitoka Kyerwa kuja Dar es Salaam kupata huduma za Serikali kwa kweli

walikuwa wanapata shida sana, lakini sasa ni rahisi unatoka Kagera asubuhi jioni unafika Dodoma, kesho unamaliza shughuli yako, unajiandaa kurudi kwetu. Kwa hiyo hili naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niwaombe sana, sio kila jambo linalokuja hapa Bungeni lazima tulipingi, kile kinachofanyika kizuri ndugu zangu tukiunge mkono tusiwe tunapinga kila kitu, watu watatushangaa huko nje. Kwa hiyo, mimi kama Mbunge na Mwanakamati naunga sana mkono hoja hii ya kuipitisha kuwa Dodoma kuwa Makao Makuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limenisikitisha sana lazima tuliseme, nimekuja kugundua ni kwa nini wenzetu walikuwa wanalamika sana kuwa hawana watu wa kuwasalidla ofisini, kweli limethibitika asubuhi nimeona hata hoja ya upande wa pili waliyoleta taarifa yao jinsi ilivyokuwa, hao watu kwa kweli muwafikirie ili wapewe wasaidizi kwa sababu kama hawawezi kuandaa hata taarifa ya kuleta Bungeni kwa kweli wanahitaji msaada, muwafikirie. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niombe sana tunapoleta sheria hii Dodoma kuwa Makao Makuu lazima tuangalie mazingira ambayo ni mazuri. Kwa mfano hili nilishalisemea hata kwenye Kamati, Dodoma sasa hivi inaenda kuwa Makao Makuu, lazima tuangalie yale mambo ambayo yalikuwa yanasurya Dar es Salaam kwa mfano Dar es Salaam unakuta kana maeneo mengine ambayo yako karibu na katikati ya mji bado hata hayajapimwa na hapa Dodoma sasa hivi hii sheria tuna uhakika inaenda kupita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie ujenzi huu unaoendelea kujenga hapa Dodoma kama upo kwenye mazingira ambayo ni sahihi maeneo haya yamepimwa. Kwa mfano, nikienda pale nyuma ya *Martin Luther* pale lile eneo nyuma kidogo halijapimwa, kwa hiyo tuombe Mheshimiwa Waziri tuisitangaze tu kuwa Makao Makuu lazima tuhakikishe

ujenzi unaoendelea mpango Miji iwe sahihi ili ioneckane kweli hapa ni Makao Makuu. Tusitangaze tu lakini tuhakikishe kila huduma zinapatikana ambazo zinaendana na Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na barabara bado barabara nyingi hapa Dodoma hazionekani kama ni Makao Makuu, lakini tunajua kwa sababu ya uamuzi huu ambao umefanywa na Mheshimiwa Rais naamini mambo yanaenda kukamilika na kulingana na taarifa ambayo Mheshimiwa Waziri Jafo amekuwa akitupatia ya kuboresha Jiji la Dodoma tunaamini mambo yanaenda kukaa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, uamuzi huu ni uamuzi sahihi na ni uamuzi ambao unahitaji kuungwa mkono na kila Mtanzania mwenye akili timamu. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri. Nilimwita Mheshimiwa Cecil David Mwambe atafuatiwa na Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba na Mheshimiwa Yahaya Omary Massare ajiandae.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia kwenye mjadala uliopo mbele yetu. Nataka nianze na mambo machache, wakati najenga hoja yangu ili kuweza kuonyesha namna gani sisi kama Bunge tumekuwa tukitoka nje ya utaratibu ambao ndio hasa majukumu yetu sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata mchangiaji aliyetoka sasa hivi sidhani kati ya mambo makubwa matatu ambayo ni kazi yetu sisi ya kibunge alikuwa analifanya lipi kwa maana ya kuisaidia Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbele yako kuna huu Muswada kama ulivyo hapo unasema the Dodoma *Capital City Declaration Act*, 2018, lakini huku ndani kuna mambo mawili ambayo yamechanganywa changanywa, jambo la

kwanza kabisa ni tamko la Rais la kutaka kuifanya Dodoma kuwa jiji. Unaendelea sehemu ya pili ni tamko pia la Rais kutaka sasa Dodoma iwe Makao Makuu ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Bunge na sisi Wabunge ni pamoja na kutunga sheria na kuna watu hapa walikuwa wameshauri toka mwanzo kwamba Rais ameanza hatua ya kwanza ya kutangaza Dodoma kuwa Jiji, kutangaza Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi kabla sheria haijaja hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kimsingi ametupoka sisi kama Wabunge madaraka yetu kimsingi ya kuweza kumshauri kama ambavyo inatakiwa ifanyike. Kwa hiyo, tungepewa kwanza kazi ya kutunga sheria, ndipo tungeendelea kwenye kazi ya kuishauri na kuisimamia Serikali. Hata hivyo, katika mambo yote yaliyopo hapa mbele yetu, hata bajeti ambayo inakuja kufanya hili jambo haieleweki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Simbachawene pale siku ya kwanza kabisa alipoleta lile tamko lake la kutaka tumpongeze Mheshimiwa Rais, kati ya mambo niliyasema wakati nachangia nikamweleza, kwamba utafiti uliofanyika kulifanya Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi, kulifanya Jiji la Dodoma kuwa jiji zinatakiwa pesa takribani shilingi trillioni arobaini kwa ajili ya kufanya hili jambo liweze kukamilika pale. Wataalam wakashauri tufanye utaratibu wa miaka kumi, kumbe hili jambo toka mwaka 1973 Mheshimiwa Halima Mdee hapa kasema utaratibu ndio ulikuwa huo ili kuweza kutenga pesa lazima lifanyike taratibu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona sasa hivi kuna mambo machache yanaanza kufanya tunajenga stendi kule nje ya Mji, kuna barabara hapa zinaanza kujengwa hapa Dodoma, haya ndio maandalizi ya kuenda kulifanya Dodoma kuwa Jiji, maandalizi ya kufanya Dodoma kuwa Makao Makuu, lakini bajeti yake lazima itokane na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumefika wakati tunaanza kudanganyana tunasema kwamba Jiji la Dodoma lina uwezo wa kufanya hizi kazi zake zote, Jiji la Dodoma ndio linaloongoza kwa mapato Tanzania na kuna Mheshimiwa mmoja hapa anachangia anampongeza kabisa Rais kutangaza Jiji la Dodoma kwamba ndio linaloongoza kwa mapato, lakini anasahau kwamba Madiwani waliopo Dodoma akiwemo Mheshimiwa Bonifance ambaye ni Meya wa Jiji la Ubungo na yeye ni mmoja kati ya watu waliosema kwamba Rais alipotoshwa. Sasa yule anazidi kutaka kuutangazia umma kwamba ile taarifa ya Rais ilikuwa sawa. Kwa hiyo, jukumu letu sisi la kuishauri Serikali tunaachana nalo, tunabaki tuu kazi ya kupongeza kimsingi hii sio kazi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadri ya kanuni kazi hii ya kupongeza ni ya mtu aliyeko kwenye kitti siku ambayo hoja ile iko pale mbele, tunapoteza muda mwingsi kwa ajili ya kupongezana, muda mwingsi kwaa ajili ya kusifiana, tunasahau shughuli yetu ya kuvisimamia na kuishauri Serikali kimsingi, ndio tunafikishana hapa tulipo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi yanatokea tuna taarifa kabisa za uhakika kwamba huu Muswada unaokuja hapa lakini ndugu zetu wa Zanzibar ambaa ni sehemu ya Muungano hawakushirikishwa vizuri. Huwezi kwenda Zanzibar ukawaandikia tu barua kama ni watoto wadogo eti kwamba tunataka Dodoma kulifanya kuwa jiji na hapo badala Mheshimiwa Rais kutamka kwamba Dodoma ni jiji, ukategemea wao watakujibu wakiwa na roho safi, hawawezi kukubali. Wale sio watoto wadogo, kunakuwa na utaratibu wa ushirikishwaji, Baraza la Wawakilishi Zanzibar pamoja na Wabunge au Baraza la Mawaziri la Zanzibar pamoja na Baraza la Mawaziri la huku Bara, wakae pamoja kujadili mambo mbalimbali yanayohusiana na Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanakuja hapa na hoja wanasema kwamba Dodoma ni katikati, sasa katikati kutokewa wapi? Hili ndio lingekuwa suala la msingi ambalo

ningefikiri Waziri angelijibu. Kama hapa Mheshimwa Heche kutoka Mara huko kwao Tarime, mpaka kufika hapa Dodoma naongelea habari za kilomita mia tisa mimi nikiwa natokea masasi mpaka kufika hapa naongelea habari za hizohizo kilomita karibu elfu moja na mia mbili, sasa katikati ni wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwenye bajeti zote zilizopita mpaka bajeti ya mwaka huu Wizara mbalimbali tumezitengea pesa kwa ajili ya kufanya Makao Makuu ya ofisi yao kwenye Mji Mkuu au Makao Makuu ya Nchi. Kwa mfano Wizara ya Viwanda na Biashara ofisi ya *TBS* imetengwa shilingi bilioni kumi na tisa ili waweze kujenga Dar es Salaam, na ujenzi ule unaendelea leo hii tunawa-*frustrate* tunawaambia kwamba Makao Makuu ya Nchi yatakuwa Dodoma ofisi zote zitakuwa zinakuja huku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaona na Wizara ya Katiba na zingine zote wanalazimishwa kuja Dodoma lakini hii haishii hapa tu, tunaona maendeleo ya ghafla yanatokea Dodoma kwa sababu kuna wageni wanaohamia. Hawa wageni wanaohamia nikiwemo pamoja na mimi nusu ya maisha yangu, familia yangu iko Dar es Salaam, ndio maana wanasema Serikali hii haieleweki iko barabarani kila siku, iko Dar es Salaam au iko hapa Dodoma kwa sababu muda wote Watumishi wanakuwa kwenye *movement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wamelazimishwa kuhamishiwa Dodoma pasipo kupewa stahili zao stahili, wote wanavilio, pamoja na wao kuwepo hapa lakini wamekuwa na vilio kwamba pesa waliopata haiwatoshi, pesa waliopata sio stahili yao. Sasa tunalazimisha kufanya haya mambo tumeona sisi Malawi, tumeona Zimbabwe na maeneo mengine wakiwa wanafanya hivyo vitu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Taarifa.

MWENYEKITI: Hebu subiri kidogo Mheshimiwa taarifa, Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nimpe taarifa mchangiaji na kama taarifa hiyo ataona hailelewi, nitaomba Bunge lako Tukufu niliwekee uthibitisho. Kama Waziri ambaye nafanya kazi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ninazo taarifa za uhakika na zenye uthibitisho Watumishi wote waliokwisha kuhamia hapa Dodoma wote wamekwishalipwa stahiki zao zote na hakuna hata Mtumishi mmoja anayeidai Serikali fedha na stahiki yoyote ile kwa kuhamia hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimpe tu Mheshimiwa Mbunge taarifa kwamba kwa taarifa hizo ambazo anazichukua huko anapozipata, asipotoshe Bunge hili kwamba Watumishi wamehamia hapa Dodoma na hawajalipwa stahiki zao. Sio kweli na hilo nina uthibitisho na kama Bunge likitaka nilete uthibitisho huo nitauleta ndani ya Bunge lako Tukufu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwambe unasemaje kuhusiana na taarifa hiyo unaikubali au unaikataa?

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo taarifa siipokei kwa sababu hao watu sisi tunakutana nao na kuongea nao mitaani, walichokifanya Serikali ni kwamba watu hawa wanatakiwa walipwe stahiki zao za uhamisho kadiri ya utaratibu wa Kiserikali, atalipwa *per diem* siku ishirini na moja, baada ya pale atalipwa *disturbance allowance*, atalipwa pesa ya kuhamishiwa mizigo. Tulimsikia Rais akisema hawa watu wahame kwa kutumia malori kwa kutoka Dar es Salaam kuja hapa na treni.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu naomba nitumie kanuni ya 64(1)(a) ambayo inasema kwamba Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

MWENYEKITI: Na ipi?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Niikisoma pamoja na kanuni ya 68(1) inayohusu utaratibu.

MWENYEKITI: Na nyingine pia.

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naisoma pamoja na Kanuni ya 63 ambayo inanitaka nitoe uthibitisho wa jambo ninalolisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilihakikishie Bunge hili, narudia kusema mimi kama Waziri mwenye dhamana ya kusimamia awamu zile zote nne za kuhamishia Serikali hapa Dodoma, ninao ushahidi na uhakika Watumishi wa Serikali wamelipwa stahiki zao. Namwomba Mheshimiwa Mbunge ama afute kauli yake, ama alete uthibitisho ndani ya Bunge hili wa Mtumishi huyo ambaye anadai kwamba hajalipwa stahiki zake. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cecil Mwambe, ungekuwa wewe Mheshimiwa unafahamu mambo mengine huwa tunayakuza tu, Mheshimiwa Waziri amelielezea kwa kiwango cha kuweza kulithibitishia Bunge kwamba taarifa zake alizonazo maana ndio anaesimamia shughuli hii. Hiyo sio kanuni.

MHE. HALIMA J. MDEE: Kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Hapana.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa nakuomba ukae tuu chini, Mheshimiwa Halima ye ye ni kweli lazima atoe maelezo ambayo yanalfanya Bunge liamini kwamba huyu aliye kuwa anaongea alikuwa haongei ukweli wa jambo. Yeye ndio umemsikiliza vizuri, sasa ningelikuwa wewe unaenda *straight* tu kutolikuza suala hili kwamba unafuta kauli yako kwamba

Watumishi wa Serikali waliohamishiwa hapa hawajapokea stahiki zao, futa tu hiyo kauli, tunaenda vizuri tu.

MHE. HALIMA J. MDEE: Kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: ngoja, usi....Mheshimiwa hebu kaa chini, Mheshimiwa Mwambe ningekuwa wewe hiyo ndio njia nzuri ya kwenda mbele.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi lakini nikuombe radhi kwanza kabla sijasema nimefundishwa kusema ndio na hapana, lakini ndio na hapana yangu lazima isikilizwe halafu tuweze kufikishana pamoja. Kadri ya taratibu za Bunge na Kibunge anaetakiwa kuthibitisha na imetokea humu ndani mara nyangi ni yule anayefikiri kwamba mimi nimesema uwongo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Tunaanza kubishana? Nimelieleza, kaa tu nimelieleza kwamba ndio maana kama mlifuatilia nilikuwa namwongoza Mheshimiwa Waziri atufikishe kwenye kanuni yenye ya 63 na kweli akaenda mpaka akafika huko. Hiyo sasa inayofuata maelezo mliokuwa mnamfuatilia kalielezea sio kwamba atoe ushahidi humu.

Katika hatua itakayofata kwa sababu sisi tutakuja kuangalia *evidence* ambayo Serikali itaweka hapa kwa Wafanyakazi wa Serikali ambao wamefika Dodoma na wamelipwa haki zao, hilo tutafika, sasa wewe ya kwako tunasema kwa sababu umesema kitu ambacho unaamini hawajalipwa sasa tuambie unafuta kauli au sasa tukutake wewe utele?

MHE. HALIMA J. MDEE: Kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima kaa, kaa tu. Mheshimiwa Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa nafuta kauli, lakini niiambie meza yako pamoja na mimi kufuta kauli ukweli huu bado utaendelea kuishi kwa sababu ndio ukweli uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaendelea hapa na kuna watu hapa naona wanapiga kelele kimsingi kwamba hiki kitu kinawaumiza watu wengi, hatujapinga Makao Makuu ya Nchi kuhamishiwa Dodoma, lakini tunasema hili jambo liende na taratibu zake. Watumishi wapewe stahiki zao, bajeti ieleteweke kwa mfano mambo ya *housing* na mengine, miundombinu ya Dodoma haijawa tayari kukaribisha wageni walio wengi kwa hiyo tunataka haya mambo yafanyike ...

MWENYEKTI: Roma ilijengwa katika siku moja?

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikwambie tu kwa mfano hawa ndugu zetu wa Malawi waliotoa miji pale Blantyre, lakini pia tuna Lilongwe. Kuna Mji Mkuu na Mji Mkuu wa kibiashara hayo yote tunayakubali. Sasa kama nia sisi kuja Dodoma na kuna Waziri hapa anasema Dar es Salaam sasa hivi hakuna foleni kabisa, jambo ambalo ni la uongo, foleni za Dar es Salaam ziko pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni watu wachache sana waliokuja hapa Dodoma wakitokea Dar es Salaam kwa maana ya kuhama nchi kama kweli tumepunguza foleni kwa nini sasa tunajenga daraja linaloanzia hapa *Ocean Road* kwenda kule Masaki kama wanasema hivyo. Miradi mikubwa hii ndio ambayo ndio ingeletwa hapa. Trillioni arobaini ni sawasawa na bajeti yetu ya nchi, tunapoamua tu kufanya kitu kimoja kwa mara moja, shida zake ndio hizi tunazozipata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, yafaa tujifunze wenzenetu wa *South Africa* walianza kujenga mji wao mkuu, lakini baadaye wakatengeneza mji mwagine wa kibiashara sisi tumekuwa na hayo mambo. Tunaongelea hapa habari stahiki za watumishi ambavyo kama hivyo mlivyosema hatuwezi kuthitibsha kwa sababu wale watu hakuna atakayekubali kunipa *payroll* yake au *bank statement* itaonekana analisaliti Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hili jambo hata watumishi wa umma ambao wamestaafu sasa hivi miaka mitatu, miaka minne wanashindwa kulipwa stahiki zao kwa nini tuamini watumishi wanaohamishiwa Dodoma wanalipwa stahiki zao kwa wakati? Kwa hiyo, hili jambo tuliache kama liliyvo kwa sababu wametaka tufanye hivyo lakini kimsingi linawaumiza Watanzania wengi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi jukumu letu kama ambavyo hapa nimesemea mheshimiwa Simbachawene amesimama na Wabunge wengi wa Dodoma, hatupingi moja kwa moja Dodoma kuwa Jiji, Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi yetu, lakini tunachokisema taratibu za kisheria zifuatwe kuhakikisha haya mambo yanakwenda vizuri, Jiji letu litakosa sifa za msingi, *capital* yetu itakosa sifa za msingi. Kwa hiyo lazima twende na utaratibu tupange bajeti inayoeleweka, tena nashukuru Mheshimiwa Simbachawene sasa hivi ndiyo amekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti labda hapo zamani alikuwa hajui kinachoendelea kule, atuonyeshe ni wapi kuna pesa ya kulipia

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwambe. Mheshimiwa Masaba atafuatiwa na Mheshimwa Heche na Mheshmiwa Ezekiel Maige ajiandae.

MHE. GIMBI D. MASABA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nami kwa kupata nafasi ili niweze kuchangia Muswada huu. Naomba niungane na wale wanaosema kwamba Kambi ya Upizani Bungeni hatupingani na hoja ya kwamba kufanya Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi. Tatizo hapa ni taratibu ambazo tunazitumia, ukisoma kwenye huu Muswada hata ule ujanja ujanja unaotumika kupitisha Muswada huu utaelewa kabisa hata kama umesoma ukaacha vyeti shulenii, utajua kabisa kwamba kuna njia ambazo zinatumika ambazo siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunajadili sheria ya kufanya iwe Makao Makuu ambapo masikitiko yangu ni kwamba kwa nini sheria hii haikuja kabla ya kuhamia hapa Makao Makuu. Mheshimiwa Rais alitoa tamko kwamba tunahamia Makao Makuu na ameshafanya utekelezaji, watu wote wamehamia hapa na tamko amelitamka Mheshimiwa Rais na akatekeleza. Leo Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ameleta tupitishe sheria, sasa nataka nitoe masikitiko yangu kwamba kwa nini kwamba sheria hii haikuja kabla ya kuhamia hapa Makao Makuu? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba Mwalimu Nyerere alitamka hapa patakuwa Makao Makuu ya Nchi, lakini kuna maswali tujulize kwa nini Mwalimu Nyerere hakuhamia? Hakuhamia kwa sababu alikuwa hajaleta Muswada Bungeni wa kutunga Sheria ya Makao Makuu. Leo Rais wa Awamu ya Tano ametamka na kuhamia, hivi vitu hata ungemweleza nani unaona namna gani Serikali ya Awamu ya Tano wanavyokosea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu hata kama hutaki kuzungumza unazungumza, kuna vitu ambavyo viro tofauti sana. Leo kuna Wabunge walijaribu kuzungumzia kuhusu suala la taratibu za kufanya kuwa Jiji, lakini kuna watu waliwapinga wakasema hapa tunachodiri sio Sheria ya jiji, bali tunajadili kupidisha sheria ya kufanya iwe Makao Makuu ya Nchi. Sasa najiuliza unawezaje kujadili suala la kupidisha Makao Makuu ya Nchi ukashindwa kujadili umuhimu wa Manispaa ya Mji kuwa Jiji unashindwaje? Kwa sababu hivi vitu viko wazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Mheshimiwa Halima Mdee bosi wangu aliyezungumza kwamba, ukisoma kwa mujibu wa Sheria Na.8 ya mwaka 2007, kifungu cha tano (5) kwamba Bunge ndio lenye Mamlaka ya kupidisha kuangalia hadhi ya namna ya jiji ndio lenye Mamlaka, kwa kujiridhisha kwa mambo matatu. Kuangalia idadi ya watu angalau ifikie laki tano, lakini pia kuangalia mapato angalau yawe yamefikia asilimia tisini na tano, lakini pia kuangalia miundombinu yenywewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sisi tunatangaza kuhamia Makao Makuu ya Nchi ili hali miundombinu bado sio. Barabara kuu ni moja tu hiyo ndio inayosomeka lakini mbwembwe nydingi tunazungumza kuhamia Makao Makuu kufanyaje, jamani kwani ukienda pale *airport* sisi kila siku tunasafiri jamani, tunakwenda kwenye nchi zingine hata ukienda hapo China wenzetu wamepanga miji, sisi tukitaka kupanga miji tunabomolea watu. Serikali inashindwa nini kutenga maeneo mazuri halafu ikaanzisha miundombinu mizuri, kupanga miji mizuri, halafu ndio baadaye tunakuja kutangaza jiji mahali hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunatagaza jiji halafu tunawaambia wanachi waondoke, tunawabomolea, hii sio sawa jamani, tunalazimisha kitu ambacho bado hakijawa vizuri. Pia tukigusa maslahi ya Watumishi sjui nini na nini taarifa zinaanza, kwa nini hatutaki kuuona ukweli kwamba tumekosea. Leo tunapitisha hii sheria halafu tafsiri yake ni nini? Ni kwamba mtasema Bunge limetunga Sheria ya Kuhamia Makao Makuu au Rais ndio ametunga sheria ya kuhamia Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitu ambavyo tunatakiwa kujiuliza. Kwa hiyo, hivi vitu pamoja na kwamba wengine hatujui sheria hivi vitu viko wazi. Tumeona utaratibu wa Majiji, tumeona utaratibu wa Makao Makuu upo wazi. Hii ni nini? Sawa labda kama wameamua kuwafuta Wagogo watani zangu, kuwasuza maana kipindi kile Obama anakuja hapa waliwasomba kutoka Dar es Salama kuwaleta hapa. Sasa yavezekana wameamua kuwafurahisha ili kuondoa ile dhana. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Mheshimiwa John Wegesa Heche atafuatiwa na Mheshimiwa Maige na Mheshimiwa Yahaya Omary Massare ajiandae.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia. Nianze kwa kurejea Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania hasa kile Kipengele cha (c) ambacho kinasema sehemu ya Pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi kusimamia, kushauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele (c) kinasema kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutunga Sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba hii ambayo wote tulipa kuilinda akiwemo Rais inasema kwamba Bunge hili ndicho chombo chenye Mamlaka ya kujadili mpango wowote wa muda mfupi na wa muda mrefu na kuutungia Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti asubuhi na nimewasiliza Wabunge wote wa CCM na kwa kweli sisi hakuna mtu ye yeyote anayesema suala la kuhamia Dodoma ni suala baya, hakuna mionganini mwetu anayesema kuachilia mbali wachache wanaofanya *spinning* kwa sababu ya manufaa yao ya kisiasa kwa sababu wanaweza kuona hapa leo tu hata kesho yake hawawezi kuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema kwamba Mpango wa Taifa amba tulijadili hapa tulipokuja hapa Bungeni na tukaupitisha na tukautungia Sheria. Mpango wa Taifa wa mwaka mmoja tumewapa *challenge* akina Mheshimiwa Jenista kwamba tuonesheni kwenye mpango huo sehemu yoyote mliyoandika kwamba mna mpango wa kuhamia Dodoma kipindi hiki. Wamebakira wanaanza kusema, Dodoma ni katikati, Dodoma ni katikati, Dodoma ni katikati, Dodoma ni katikati ya nini? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunachotaka watuambie kwa watu walioenda Dubai mwaka 2004, ilikuwa ukifika Dubai mnaona *Billboards* kubwa zinaonesha Dubai itakavyokuwa baada ya kuwa New Dubai imejengwa na leo ukienda ukaona picha ulizoziona kwenye *Billboards* na Dubai ndivyo ilivyo sasa hivi. Sasa hawa karne ya 21 wanaleta Bunge hili hapa watu wanajadili vitu *petty petty* tu, yaani hakuna kitu karne ya 21 hakuna mpango, hakuna utaratibu, hakuna nini, Rais akishasema kesho tunahamia kule kwetu Nyamwaga, kesho wote mnabeba mabegi tupo Nyamwaga, eeh! Nyamwaga hapa ndio penyewe sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanatafuta sababu za kuokoteza, mara kuna usalama Dodoma, Mheshimiwa Lissu amepigwa risasi hapa, hapa hapa Dodoma kapigwa risasi hapa wanapopaita sehemu ya usalama, mpaka leo hawajawahi kukamata hata mtu mmoja na hawajawahi kusema nani aliyempiga risasi. Sasa wanaletewa hoja hapa kwamba nchi hii watu wana matatizo ya Vituo vya Afya. Nchi hii tangu kuanza kwake sera ya afya ya kwetu inasema kila Kata itakuwa na Kituo cha Afya, tunapozungumzia Kituo cha Afya tunazungumzia chenye uwezo wa kulaza mtu, chenye uwezo wa kufanya *operation* na chenye uwezo wa kutoa matibabu ya vipimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarime nina Kata 26, tuna vituo vitano na vinne tumejenga kipindi hiki halmashauri inapoongozwa na CHADEMA, tulikuwa na kituo kimoja tu *basically*. Nchi hii mpaka leo Mbunge anasimama anasema tuna Vituo 200, eti Vituo 200 miaka 56, ndio tukae hapa tupigiane makofi kati ya vituo zaidi ya 4,600 wakati huo wanachukua pesa, pesa za walipa kodi maskini eti wanahamia Dodoma, wakati tuna majengo Dar es Salaam, yaani nawashangaa *no wonder* leo wanatafuta watu waunge mkono hoja wanachukua zaidi ya bilioni 80 za watu wanapeleka kwenye uchaguzi wakati watu wanakufa mashulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi hapa nilimwona Mheshimiwa Waziri anajibu wanachukua bilioni 80,

wanapeleka kwenye uchaguzi, Wabunge wanaenda kufanya sijui nini ile, eti kutafuta bilioni mbili. Tunatakiwa kupimwa sijui tunafanyaje kazi kwa kweli yaani bilioni mbili mnaenda pale sijui nini ile, wanaenda kutafuta bilioni mbili wakati bilioni 80 zinachukuliwa kwa kufanya mchezo watu wanaunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto hawana madawati, asubuhi tumeona mama Kikwete anasema shule moja ina watoto 4000 shule moja ya msingi, sio watoto wetu, watoto wenu hawasomi hapo kwa sababu tu ni nanii wanakuja hapa kwa sababu watoto wenu hawasomi hapa makofi kwa kila kitu makofi kujipendekeza, unafiki, kutokujadili mambo ya msingi, tunachukua pesa tunaleta hapa hatuna Vituo vya Afya, hatuna maji (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Heche, kwa heshima zote nakuomba hebu jielekeze kwenye Muswada tu, mimi nakuomba tu.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi, Muswada huu najadili kwamba gharama za kuhamia hapa ni kubwa mno ukilinganisha na mahitaji tullyonayo. Ndicho ninachosema kwamba unapokuwa Kiongozi uko nyumbani kwako una watoto, una elfu 10 mtoto anaumwa na wewe unataka kunywa bia, utapeleka mtoto hospitali kuliko unywe bia ndicho ninachosema, *simple!* Utakuwa mzazi wa ajabu kweli kweli mtoto wako anaumwa wewe una elfu 10 ya kununua dawa, ukaenda kunywa bia halafu unarudi unasema bia ile ilikuwa muhimu sana kwa sababu nilikuwa na mawazo leo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndio maamuzi yenu nyie mpo wengi na mnaweza kufanya *spinning* mnaweza kudhibiti Vyombo vya Habari mkazungumza nyie peke yenu, lakini ukweli wa Mungu utasimama na sisi sio kizazi cha mwisho hapa Tanzania. Nataka niwahakikishie haki ya Mungu kabisa Rais mwingine atakuja, atarudisha hii Dar es Saalam mimi nawaambia, tupo hapa Mungu atuweke wazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo,? Nasema kwa sababu wanafanya mambo ambayo ni *unplanned* yaani wanataka Bunge hili lote Watanzania wamewalipa posho wamekuja kukaa hapa wanakula vizuri mshahara wa Mwalimu ni Sh.300,000/=, tumelipwa hapa Sh.300,000/= kwa siku tunakuja kujadili vitu *petty* ambavyo havina msingi wowote kwa maendeleo ya watu wa nchi hii, hakuna *reasoning*, hakuna mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona Abuja watu walikuwa wanahama kuna mipango. Mwalimu Nyerere mwaka 1973 alisema baada ya miaka 10 kuna mpango mwaka mmoja, mwaka wa pili tutaweka Ofisi, mwaka wa tatu tutafanya hiki, sasa wameleta familia za watu hapa, mama yupo Dar es Salaam, baba yupo hapa, halafu wanadai wamelipa watu wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni huo, Mungu anajua na hata wakitumia mabavu na sisi wengine ambao tunasema ukweli tunajua kwamba hawakuwa na mpango wameshtukizwa tu Tamko, si tunaongea na nyie tu hata kwenye chai. Tamko tu sasa wameleta watu wanaenda kurundika *UDOM*, yaani Chuo kilijengwa watu wasome, eti wamefanya Ofisi na Waziri kabisa eti anaamka anakwenda *UDOM* pale kwenye madarasa ya watoto, wamekata na *ceiling board* eti niko Ofisini hapa. Haya mambo ya kuendesha nchi hii kama imezaliwa leo na inaisha kesho, haya mambo...(*Kicheko/Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Anafuata Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Yahaya Massare atafuatiwa na Mheshimiwa Bobali.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu wa Tamko la Makao Makuu ya Nchi kuhamia Dodoma rasmi lakini upitishwe na Bunge lako hili Tukufu siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitangulie kwa kuunga mkono hoja hii ya Serikali yenye dhamira njema kabisa ya wananchi wa Mkoa wa Dodoma, lakini wananchi wote wa Tanzania Mikoa yote 26 na mingine mitano ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni zuri tena zuri sana toka ilivyotamkwa mwaka 1973 ilifuatia utekelezaji wa Serikali kuhamia Dodoma. Waziri Mkuu wa pili wa Tazania Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa alihamia Dodoma miaka ile ya 1975/1976 na hata Waziri Mkuu aliyemfuatia Edward Sokoine alifanya kazi Dodoma na Dar es Salaam. Salim Mohamed Salim alifanya kazi Dodoma na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuletwa Muswada huu leo miaka mingi baadaye ni tija kubwa kabisa kwa Serikali ya CCM ambaye sasa inaongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. John Joseph Pombe Magufulsi kwa dhamira njema kabisa yakuifanya nchi hii sasa pia tupunguze msongamano mkubwa ulioko katika Jiji kubwa la Tanzania hii Jiji la Dar es Salaam. (*Makofisi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira hii na sifa kubwa za mji wa Dodoma kwamba upo katikati, lakini mimi ni Mbunge ninaye toka katika Mkoa wa Singida Mkoa ambao ni jirani na Mkoa huu wa Dodoma jirani na Makao Makuu ya Nchi lakini Singida ilikuwa sehemu ya Dodoma kipindi cha nyuma. Hivyo, dhamira hii inapaswa kuungwa mkono na wananchi wa mikoa jirani ukiwemo mkoa wangu ambao nawakilisha wananchi wa Manyoni Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faraja ya mji huu wa Dodoma kuwa Jiji, kuwa Makao Makuu ya Nchi kutapelekea sasa mji huu ambao ni mionganini mwa miji michache kabisa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao umejengwa kwa mpangilio mzuri. Ilipotangazwa mwaka 1973 ilifuatia kuundwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu. Mamlaka hii ilifanya kazi nzuri sana ambayo iliupanga

mji huu na leo ni miongoni mwa mji ambao ukiwa angani unaouona kweli mji huu unastahili kuwa Makao Makuu ya Nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto ambazo zipo nakubaliana kabisa kwamba sasa ni wakati muafaka wa Serikali kuhamia Dodoma na kufanya kazi kama inavyofanya sasa. Itarahisisha mikoa ya pembezoni kufika Dodoma kwenda kuona Viongozi wa Serikali. Hapa tunapozungumza Waziri Mkuu yupo Dodoma, Bunge lako Tukufu liko Dodoma, lakini Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yupo Dodoma, Wizara zote, Mawaziri wako Dodoma.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kujivunia lakini katika kutekeleza llani ambayo tuliwauzia wananchi na wakaamini kuchagua chama hiki kwamba kinatekeleza yale ambayo tuliwaambia kwamba tunakwenda kutekeleza llani yetu kwa kufanya haya yafuatayo likiwemo hili la kuifanya Dodoma sasa iwe Makao Makuu ya Nchi. Hivi juzi juzi tu Mheshimiwa Rais alisaidia sana Mji huu wa Dodoma ulipotangazwa kuwa Jiji kwa hiyo umeendelea kuboreshwa na utaendelea kuboreshwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona jinsi Serikali inavyochukua juhudzi za kujenga barabara za pembezoni lakini Mji wa Dodoma sasa unaboreshw. Niombe sasa labda Serikali iangalie suala zima la Miundombinu ya maji kuwashakikishia bwawa lile la Farkwa nalo linawekewa mkazo ili baada ya *population* kuongezeka basi Dodoma kusijekuwa na tatizo la miundombinu hii ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na machache haya ya kuchangia katika jambo hili la kufanya Mji huu wa Dodoma kuwa Makao ya nchi na naunga mkono hoja hii ya Serikali kuleta Muswada huu mwaka huu wa 2018 tarehe 04 Septemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako, Mheshimiwa Bobali atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Phillipo Mbogo na Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed ajiandae.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru, ni mionganini mwa Wajumbe wa Kamati ya TAMISEMI na Utawala, namshukuru Mwenyezi Mungu mionganini mwa Wabunge ambaotumekuwa tumeujadili huu Muswada kwa muda mrefu ni sisi Wajumbe. Tumepata fursa ya kupata mafunzo, semina lakini pia tumekuwa na Mwanasheria Mkuu kwa mara kadhaa tukijadili juu ya Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niunge mkono Hotuba ya Mwenyekiti wangu wa Kamati aliyoisoma hapa leo asubuhi. Pia niunge mkono baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliyosema, sifikirii kama kuna mtu ambaye anapinga hoja ya Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi yetu, sifikirii. Kinachoelezwa hapa ni namna ya kuboresha na wakati mwagine ni *challenge* tunai-*challenge* Serikali juu ya uendeshaji wa jambo hili kwamba kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma ni njia ipi inatumika ni mfumo gani umetumika ndio kinachofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri na Hotuba ya Kamati tume-refer sana kuhamishwa kwa Mji wa Lagos kwenda Abuja mwaka 1991. Hata sisi wakati wa Semina Wanasheria wa Serikali walipokuwa wanakuja walikuwa wanaelezea tu habari ya Abuja tarehe 12 Desemba, 1991 kutoka Lagos kwenda Abuja maelezo yalikuwa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba ni-*challenge* upande wa Serikali kama kweli tumeamua kuiga mfumo wa Nigeria, lazima kuna maswali mawili tuijiliuze, wenzetu Nigeria wakati Rais Ibrahim Babangida anahamisha Makao Makuu kutoka Lagos kwenda Abuja alisema hivi Lagos ni *economic capital* ya *West Africa*. Imekuwa *congested* ina mambo mengi ya kiuchumi yanayofanyika,

sasa naomba tuijulize Dar es Salaam ni *economic capital* ya Tanzania pekee ama ya ukanda wote ya Afrika Mashariki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili alilolisema Babangida ni kwamba anahitaji kwenda Abuja kwa sababu ya kiusalama ili Serikali ipate fursa ya kukaa kwenye sehemu iliyotulia waratibu vizuri mambo ya kiusalama. Nataka kujua kwamba Dodoma na yenyewe imekuwa ni *center* ya usalama wa nchi yetu tumejipanga kihivyo ama tumeamua kuja, Mbunge mmoja amesema hapa kwamba Mheshimiwa Tundu Lissu kapigwa risasi Dodoma na mpaka sasa hata aliyepiga hajulikani hata mtu kuwa *suspected* hayupo. Sasa je, na hili nalo tunalichukuliaje? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la tatu *capital city* inaweza ikawa na mambo mawili *economic capital and political capital*, kwamba kama Dodoma inakuja kuwa *capital city* inakuwa pia *capital city* ya kiuchumi au ya kisiasa pekee? Kama tunaamua kuja kiuchumi na kisiasa tuliweke waz.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunaamua tunakuja kisiasa tufanye hivi naomba nishauri kama Dar es Salaam itaendelea kuwa *economic capital* ya Tanzania kuna haja gani leo Wizara ya Viwanda na Biashara kuhamia Dodoma, kuna haja gani? Kuna haja gani leo Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje kuhamia Dodoma kwa nini zisibaki Dar es Salaam kuendelea kuratibu mambo ya kiuchumi na mambo ya Mahusiano ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya Nigeria wamefanya sio Wizara zote zipo Abuja, Wizara zingine zipo Lagos kuratibu masuala ya kibishara kwa sababu Lagos ni *Centre of Economics*. Wizara ya Viwanda inahitaji ibakie Dar es Salaam, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Wizara zingine mfano Wizara ya Uchukuzi, inahitaji kubaki Dar es Salaam, iendelee ku-manage *airpot* zetu na bandari zetu, lakini Wizara ya Uchukuzi inakuja Dodoma, kule bandari anaratibu nani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima tuweze mikakati kwamba kama tunakuja Dodoma, tujue kwamba tunakuja *as a political capital* siyo *economic capital*. *Economic Capital* itaendelea kubaki kuwa Dar es Salaam. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani inawezekana ni kwenye maneno kuna tofauti, lakini kwenye utekelezaji naona kama mnafanya hivyo kwamba wanaendelea kuifanya Dar es Salaam kuwa ni *economic capital*. Wanajenga *interchange, flyover, standard gauge railway* Dar es Salaam. Maana yake ni kwamba Dar es Salaam *is still an economic capital* na wanaitambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama hilo ndiyo jibu, lazima tuliweke sawa kwamba tunakuja Dodoma *as a political capital, not as an economic capital*. *Capital City* yoyote lazima iwe na *element* mbili, kuwa *Capital City* ya kisiasa na ya kiuchumi. Kwa hiyo, naomba kaka yangu Mheshimiwa Jafo atakapokuja kujibu hizi hoja, atujibu kwamba tunakuja *full tukiwa economic and political* ili Watanzania waweze kuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, unaposema *capital city*, sisi kwenye Kamati tulikuwa tunajadili, hivi Dar es Salaam ilikuwa *Capital City*, kulikuwa na sheria ilioitambua? Jibu ni kwamba hakuna, lakini ilikuwa *Capital City* kwa sababu moja. Ikulu ya nchi iko Dar es Salaam. Unapozungumza *Capital City*, unazungumzia *State House* ndiyo kipaumbele namba moja. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nilikuwa natamani mtu wa kwanza kuhamia Dodoma angekuwa Mheshimiwa Rais kabla hata ya Mawaziri. *State House* ndiyo *element* inayoidentify kwamba hapa ndiyo *Capital City* ya nchi. Huwezi leo kwenda Nigeria tunakosema ukakuta Ikulu iko Lagos.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata huyo Ibrahim Babangida mwaka 1991 alianza kuhamia ye ye ndiyo Wizara zikaanza kumfuata. Sasa sisi tunaanza Wizara, Idara, Ikulu

iko Dar es Salaam. Hii kwanza ni gharama, mnasafiri sana Waheshimiwa Mawaziri kwenda huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya ni mambo ya msingi sana lazima tuyazingatie. Kwa hiyo, tusingisifie kwa Waziri Mkuu kuhamia, Waziri Mkuu ni kitu kimoja. Ikulu ya nchi inapaswa iweipo hapa na mtu wa kwanza aliypaswa kuja Dodoma ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema, sisi hatupingi Muswada huu wala hatupingi sheria hii ya Dodoma kuwa *Capital City*. Tunachokifanya ni kutoa *challenge* na tungependa kuona Serikali wakizifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la muhimu sana, tunahamla Dodoma kuja kuwa *Capital City*, yako mambo ya msingi ya kuyaangalia na sisi kwenye Kamati tuliraise hiyo *issue*. *Issue* hii ya Muungano ndugu zangu nawaambia siyo *issue* ndogo, ni kubwa kabisa. Hii ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunapoamua kuwa *Capital City* ya nchi lazima *partner states*, pande zote mbili za nchi ziwe *consulted* na ziamue. Wala siyo suala la kihistoria kwamba mwaka 1973 watu walikuwa *consulted*, hapana. Hatutungi sheria hapa leo kwa sababu ya hotuba ya Baba wa Taifa mwaka 1973, tunatunga sheria kwa sababu ya hotuba ya Rais wa Awamu hii. Kwa hiyo, yeye ndio alipaswa kuwa-*consult upande* wa Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu aje atueleze kwa upande wa Zanzibar wamefanya *negotiation*, wamekubaliana kwa kiwango gani? Kwa sababu jambo hili liko kwenye mkataba wa Muungano. Kama liko kwenye mkataba wa makubaliano yao kwamba Makao Makuu yatakuwa Dar es Salaam, leo wanapohama kwenda Dodoma, wamewashirikisha? Wameauliza? Wameafikiana? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, yangu yalikuwa hayo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Richard Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Rukia Ahmed na Mheshimiwa Juma Kombo Hamad.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Ofisi ya AG kwa kuleta Muswada huu. Ni jambo ambalo limekuwa la miaka mingi maana tangu matamko yatoke na mambo mbalimbali yaliyofanyika, ni miaka ambayo wengine ndio tulikuwa tumezaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la Muswada huu wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi limejieleza kwa faida zake ambazo ni nyingi lakini kwa uchache tu, kwanza suala la urahisi wa kufika Makao Makuu, tunaona Dodoma ni katikati ya nchi ya Tanzania, hata sisi tunaotoka Katavi tumeponguziwa kilometra karibuni 460 kufika Dar es Salaam. Maana kilometra 700 tu unafika hapa Dodoma na ni muda ambao utakuwa ni *economical* kwa watu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la kiuchumi, tunavyotanua na kuhamisha Makao Makuu ya nchi tunaongeza fursa mbalimbali kwa maeneo mengine. Kwa mfano, sasa hivi katika mji huu tutaweza kuongeza ajira kwa wananchi ambao tumehamia hapa, wengi wamenunua viwanja, wamejenga. Kwa hiyo, biashara zimeongeka hapa. Tukiangalia tu barabara ya kwenda Medeli hapa, *shoppers* anajenga hapo, kwa hiyo, ajira zitaongezeka. Kwa hiyo tunavyotanua Makao Makuu pia tutaboresha mji na hata namna nyingine ya kiutalii tunaweza kuongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna masuala ya maendeleo kijumla. Wengi mmeona kodi za nyumba zilivyokuwa hapa Dodoma kabla na baada ya kutangazwa kuhamia kwa Makao Makuu na vitu vingi bei zimebadilika. Viwanja bei zimebadilika, kodi za nyumba bei zimebadilika, kwa hiyo, mapato ya wananchi katika hili Jiji la Dodoma yameweza kuongezeka kwa watu ambao wanamiliki mali ambazo hazihamishiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya kiusalama kama nchi kiujumla hayalengi tu kwa usalama wa mtu mmoja mmoja, tunaangalia usalama kiujumla wa nchi. Kwa hiyo, hatuangalii usalama wa mtu mmoja mmoja kama matukio yanafanyika nchi nzima, Dar es Salaam yenyewe ndiyo inaongoza kwa matukio na ni nchi nzima matukio yanafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la kuhamishia Makao Makuu tunapongeza Serikali za Awamu zote ambazo zimepita kuanzia wazo ambalo lilitolewa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Nyerere baada ya kutoa tamko na utekelezaji ulianza. Mwaka 1979 tulikopa fedha tuka nchi ya Brazil na ndiyo tukajenga kiwango cha lami hii barabara ya kuja Dodoma mpaka ikafika hapa. Kwa hiyo, yote haya yalikuwa ni maandalizi ya kuhamia Dodoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona Bunge lilihama kutoka Karimjee – Dar es Salaam na tukaanza na ukumbi wa Msekwa na ukaja huu ukumbi mpya. Yote haya ni maandalizi ya kuhamia Makao Makuu Dodoma. Chuo Kikuu na vyuo vingine vimejengwa. Kwa hiyo, yote hayo yalikuwa ni maandalizi ya kuhamia katika huu Mji Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kupendekeza katika huu Muswada, kuna kipengele ambacho kinampa Mheshimiwa Rais kuweza kubadilisha mipaka ya Mji, basi tuone namna bora kama wachangiaji wengine ambavyo wameweza kuchangia, namna Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino ilivyo na Halmashauri ya Jiji inakuwa kama inaizunguka. Kwa hiyo, kama kiutawala tunaweza kutanua eneo vizuri, basi ikipendezwa tuweze kubadilisha maeneo ya mipaka na angalau hata lkulu yetu ya Chamwino ihamie iwe chini ya Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la miundombinu. Tunajua kuna mipango mizuri sana ambayo Serikali imeshaitoa, namna ambavyo magari yatakuwa hayaingii katikati ya mji. Basi ujenzi huo ukikamilika, tuombe sasa iende sambamba na uboreshaji wa miundombinu ya

ndani ambayo ni ya zamani ambayo ilianzishwa na *CDA*. Kwa mfano, barabara za *Area D* ambazo ni za lami zina mashimo mengi sana ambapo inapaswa yakarabatiwe maana inakuwa ni nafuu upite kwenye barabara ya vumbi kuliko kupita barabara za *area D* za lami ambazo zimekuwa na mashimo mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa mamlaka husika, *TARURA* na nyingine ziweze kukarabati hizo barabara ili angalau mtu apite maeneo ambayo yako safi na salama zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na dhana inaonekana kwamba kuhamia Dodoma hakuna kipaumbele na matokeo yake ni kwamba fedha au gharama hizo zipelekwe kwenye huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge ambao wanazungumzia kuhusu gharama za kuhamia Dodoma hazifai, tupeleke kwenye Vituo vya Afya; Waheshimiwa Wabunge wote hapa tunaingia kwenye Halmashauri na Halmashauri zetu ziko kwa mujibu wa Katiba. Utengenezaji wa bajeti, Serikali Kuu haiingilia Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kila mtu kwenye Halmashauri yake aangalie kutokana na mapato ya ndani, ni kati ya asilimia 40 mpaka 60 wanatakiwa wapeleke kwenye miradi ya maendeleo. Kwa hiyo, kama una upungufu wa Zahanati, vyumba vya madarasa, Vituo vya Afya, tumia mapato ya ndani ya Halmashauri uweze kukidhi matatizo yaliyoko kwenye Jimbo lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango kazi ambao Serikali inakuwa unauleta lazima utekelezwe wote *at parallel*. Huwezi ukasema u-concentrate na kitu kimoja umalize ndiyo uende kwenye kitu kingine. Miradi mingine inakuwa ya kimkakati kwa ajili ya kuzalisha pesa uweze kuingiza kwenye miradi mingine. Kwa hiyo, lazima vyote viende kwa pamoja na iendane na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho tu kwa kumalizia, suala la kupunguza msongamano wa watu kuhamia kwenye miji ya kibiashara la lenyewe litapungua. Tukiangalia sasa hivi watu wengi siyo tu watumishi wa Serikali na Taasisi zake kwamba wamehamia Dodoma, hata baadhi ya wafanyabiashara wengi wamehamia hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili nalo linaongeza tija katika mji huu na kupunguza msongamano kwenye Jiji la kibiashara kama Jiji la Dar es Salaam. Kwa hiyo, tunapoanzisha miji mipya, tunapunguza kwa namna fulani asilimia fulani ya msongamano kwenye miji mingine ambayo iko *too concentrated* kama Jiji la kibiashara la Dar es Salaam. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako. Mheshimiwa Rukia, halafu atafuatia Mheshimiwa Mbarouk.

MHE. RUKIA AHMED KASSIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia furasa nami nichangie katika hoja hii tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili la kuutangaza Mji wa Dodoma kuwa ni Makao Makuu ya nchi ni Jambo jema sana na kwa kweli naipongeza Serikali kwa jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya mambo ni lazima Serikali sasa ijipange kuyatekeleza ili ile hadhi na azma ya Dodoma kuwa Jiji na Makao Makuu ya nchi ipatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba *master plan* ya Mji huu wa Dodoma ilitengenezwa zamani sana tokea uhai wa Mwalimu Nyerere. Baadhi ya nchi walizoiga *master plan* yetu kwa mfano kama wenzangu walivyosema Abuja na Accra Ghana miji yao imekuwa ni mizuri kupita mfano, lakini sisi tuliotengeneza *master plan* hii bado

hatujaanza kuitekeleza. Kwa hiyo, naiomba Serikali, sasa ni wakati muafaka wa kutekeleza azma hii. Katika kuitekeleza kwetu, basi tusiwaumize wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Wagogo wa Dodoma pamoja na makabila mengine ambayo yako Dodoma ambao ni wazawa, kuna baadhi yao wameumia sana. Kuna baadhi ya wazawa wa Dodoma, Manispaa pamoja na Watendaji wa Kata wamechukua maeneo yao bila ya kuwafikiria watu hawa watakaa wapi? Nasema jambo hili kwa uchungu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mama mmoja ambaye ana asili ya Kinyamwezi. Mama huyu kafyatuka anapita akilia peke yake njiani. Huyu mama anaitwa mama Kashinde. Alikuwa na nyumba yake pale karibu na *Meriwa Secondary School*. Nyumba yake illipigwa *grader ikapita* barabara. Matokeo yake hata kiwanja hakupewa na eneo lile ni kubwa na ni eneo ambalo aliritithi kutoka kwa wazee wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mama huyu ana watoto yatima, hajui aende nao wapi? Kapewa kiwanja mtumba. Hivi kweli mtu mwenye miaka 75 anaweza tena kujenga nyumba akaweza kwenda kukaa mtumba? Huu ni uonevu. Kwa hiyo, hawa wenzetu walolipokea jambo hii, naomba Serikali iwafikirie ili ile furaha yao izidi na sisi tuliokuja hapa kuhamia kama wenyeji wetu ili nao waweze kutuunga mkono katika jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mama huyu ana eneo kubwa sana alilorithi, Mtendaji pamoja na Manispaa wamelichukua, wamesema eti wanawapa watu ambao wana Taasisi. Hivi Taasisi gani itakayochukua eneo la mtu wakapewa bila mwenyewe kupewa hata sehemu ya kukaa? Ana watoto wake wengine wamejenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilimfuata mpaka huko kwake nikaona, kwa sababu mimi sipendi jambo la kuhadithiwa, napenda nione. Nilipokwenda, nikaona ana

mtoto wake mmoja kajenga nyumba, CDA walimpa kiwanja akanitajia mpaka namba ni 50. Kuna mtu kajenga chumba kimoja tu mbele na mwingine kajenga chumba vile vile, wamemwambia hapa hatuwezi kukupa, tunammilikisha mtu mwingine kwa sababu kiwanja hiki wamepewa watu saba. Hii ni dhuluma. Namwomba Waziri wa Ardhi na watu wa Manispaa, dhuluma hii wasiendelee nayo. Wazawa wa Dodoma ambao walikuwa kwenye ardhi yao wapewe *priority* ya kupewa kwanza maeneo ya kujenga wao baada ya kupimwa ndiyo baadaye wapewe wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, nitajielekeza kwenye watumishi wa Serikali. Kuhamia kwa Mji wa Dodoma ni jambo jema na wafanyakazi wa Serikali walipokuja wamekuja kwa furaha kubwa lakini matokeo yake hawana sehemu za kukaa. Wengi wao wanakaa kwenye *guest*, wengine wamepanga kwa watu, wameacha familia zao Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ijenge kwa haraka sana nyumba za kukaa watumishi wa Serikali ili wasiendelee kuchoshwa na jambo hili na kuwa na maisha magumu kwa sababu mtu familia yake inapokuwa mbali naye maisha yanamwendea vigumu. Naiomba Serikali ijenge nyumba kwa haraka ili watumishi wa Serikali wasiendelee kupata shida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nitazungumzia kuhusu miundombinu. Wenzangu wengi wamesema, lakini tatizo lililojitokeza katika Mji wa Dar es Salaam ni miundombinu kutokupangwa mapema kabla mji ule kuongezeka. Kwa hiyo, kabla mji huu haujaanza kuongezeka watu wengi, Serikali ijipange kutanua hizi barabara. Kwa mfano, barabara inayotoka *CBE* – Mpwapwa ni nyembamba sana. Kwa hiyo, kabla watu hawajaanza kujenga mle barabarani, naomba Serikali ianze kutanua ile barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko tullionalo halikidhi haja ya idadi ya watu iliyoongezeka. Naomba Serikali iharakishe sana kujenga soko hapa Dodoma. Stendi ya mabasi iko

mbali. Ingawa iko mbali, eneo tulilonalo ni la kuazima. Naomba Serikali ijenge haraka ili hadhi ya Dodoma kuwa ni Jiji ipatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono jambo hili mia kwa mia. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Rukia. Nataka Mheshimiwa Kombo Hamad, si jirani yako eh!

MHE. JUMA KOMBO HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, name nakushukuru kwa kupata fursa hii ya kuchangia. Kwanza, nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye ametujaalia kuja tena katika Bunge hili la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na mchango wangu wa hoja ambayo iko mezani kwa kunukuu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ukienda kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 4(1) naomba kwa ruhusa yako niisome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasema ifuatavyo: "*shughuli zote za mamlaka ya nchi katika Jamhuri ya Muungano zitatekelezwa na kudhibitiwa na vyombo viwili vyenye mamlaka ya kiutendaji, kwa maana ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaendelea kwa kusema: "*vyombo viwili vyenye mamlaka ya kutekeleza utoaji haki*" kwa maana ya Mahakama Kuu ya Zanzibar na Makama Kuu ya Tanzania Bara au Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hiyo ya 4(1) inaendelea "*na pia vyombo viwili vyenye mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Umma kwa maana ya Bunge na Baraza la Wawakilishi.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inazungumzia vyombo viwili vyenye

mamlaka ya kutunga sheria, lakini leo chombo kimoja kikajipa mamlaka kila siku kutunga sheria kwa niaba ya chombo kingine. Hii siyo haki. Kama kuna kitu ambacho kinafanywa isivyo halali. Kama kuna kitu kinafanywa kibabe na kinyume na sheria na Katiba ya Tanzania na Zanzibar ambazo zote mbili ninazo, basi ni kitendo cha kutunga sheria bila kuishirikisha Zanzibar. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukilalamikia mambo mengi kwamba Zanzibar tunaonewa, hatushirikishwi, hatupewi haki sawa na mdau mwингine wa Muungano huu. Tumekuwa tukisema vitu vingi, lakini bado dhara hizi na ubabe huu unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, donda hili linaloendelea dhidi ya muungano wetu, *I am sure* litaendelea, lakini ipo siku litaathiri Muungano huu. Tutakuja kutaka kuurejesha sasa, lakini kazi ya kuurejesha itakuwa kubwa na haitawezekana tena kwa sababu tu ya kutotii sheria na Katiba za nchi tulizonazo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hizi wakati zinaungana, zilikuwa na mamlaka sawa. Nia njema ya Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere na nia njema ya Abeid Amani Karume, ilipaswa ibebwe na ifanyiwe kazi na hata viongozi wa leo. Siyo tu kwamba tumerithi, tunaendeleza, lakini hatujali wala hatuthamini juhudhi ya upande mmoja kwa sababu tu uwezo wa kusema, uwezo wa kutenda tumenyang'anywa na hatunao. Hii siyo halali na tutaendelea tu kusema kwa sababu hatuna namna nyingine ya kufanya. Tutaendelea kusema na kulalamika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa tu, mwaka 1973 wakati Mwalimu Nyerere anatangaza nia ya kuhamishia Makao Makuu Dodoma, Rais wa Zanzibar alikuwa Aboud Jumbe Mwinyi. Aboud Jumbe Mwinyi wakati anatunga kitabu chake cha *The Partnership*, kitabu hiki kimeandikwa na Aboud Jumbe Mwinyi; *The Partnership*, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar miaka 30 ya Dhoruba. Muungano huu ukiwa na miaka 30, Jumbe aliuita kwamba ni Muungano wa dhoruba

kwa sababu tu ya kutothaminiwa upande mmoja wa Muungano; kwa sababu tu ya kuonekana Zanzibar siyo chochote siyo lolote; kwa sababu tu ya kuonekana Zanzibar haina hadhi wala haina nguvu wala haina la kufanya ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au ndani ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Jumbe alilalamikia kitendo cha Nyerere kutangaza nia ya kuhamishia Makao Makuu Dodoma, leo mwaka 2018 tunapitisha Sheria ya Kuhamishia Makao Makuu Dodoma bila kuishirikisha Zanzibar. Huu ni msiba mkubwa na ni dharau iliyovuka mipaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni dharau iliyovuka mipaka kwamba hatujali, tunafanya tunavyotaka, basi fanyeni. Endeleeni kufanya, lakini Wazanzibari tupo, tutaendelea kusema, tutaendelea kutetea, Wazanzibari wanatusikia, wanatuelewa na wanafahamu kinachoendelea na wanaifahamu dhuluma ambayo inaendelea na wanafahamu dhuluma ambayo wanafanyiwa kwamba leo inapitishwa sheria... (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Serikali ipo Dar es Salaam...

MWENYEKITI: Hii dhuluma ni ipi ambayo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaifanya Zanzibar? Ni ipi dhuluma hiyo? Unaweza ukonisaidia nikaelewa?

MHE. JUMA KOMBO HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni dhuluma kwamba tunapitisha sheria. Ibara ya (2) imezungumza kwamba sheria hii itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Zanzibar haikushirikishwa, ni dhuluma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhuluma siyo lazima unyang'anywe mali au unyang'anywe nyumba, hii ni sheria. Hili ni jambo kubwa linalotuhusu pande zote mbili, siyo kutetea tu kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunifahamu.
(KichekoMakofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali ipo Dar es Salaam, masafa ya kuondoka Dar es Salaam na Unguja ambapo ndiyo kwenye Makao Makuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ndege ni dakika 15, kwa boti ni saa moja na nusu umeshafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dada yangu pale alisema, leo kumtoa Afisa wa Serikali Zanzibar kuja Dodoma ni siku tano. Anachukua siku tano, asafiri kutoka Unguja alale Dar es Salaam, Dar es Salaam achukue basi afike Dodoma, pengine siku ya tatu yake ndiyo kuna kikao, halafu aondoke Dodoma siku nydingine yake afike Dar es Salaam, alale Dar es Salaam siku ya pili achukue boti, siku tano. Tumekuwa tukilalamikia vitu vingi bila kupatiwa majibu. Vikao tunavyoambiwa vinakaa havina athari yoyote, havina *impact* yoyote, havina tija yoyote. *(Makofi)*

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Haya, Mheshimiwa Mbarouk, utafuatiwa na Mheshimiwa Jaku.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia kuweza kukutana na kuzungumza masuala ya nchi yetu katika Bunge letu hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwanza niseme nadhani jambo hili lilitakiwa lifanyike muda mrefu sana kutoka 1973 mpaka leo ni miaka mingi imepita. Sasa sijui labda kikwazo kilikuwa ni nini mpaka leo ndiyo tunahamia Dodoma na kuitisha sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalosema, ni kweli Serikali inahamia Dodoma, lakini ukiangalia baadhi

ya vigezo nya kuwa Makao Makuu ya nchi bado havijatimia. Sasa naishauri tu Serikali kwamba ijue ina kazi kubwa na safari bado ni ndefu. Kwa mfano, wamesema waliosema, lakini mimi nasema sasa hivi hata *bus stand* imekuwa ni shida, ndiyo kwanza inaanza kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata uwanja wa ndege wa kisasa hatuna na tunategemea kwamba baadhi ya Mabalozi au Viongozi kutoka nchi mbalimbali, kwa kuwa Serikali itakuwa imehamia hapa, nao watatakiwa kuja hapa. Sasa kitendo cha kwamba, atue Dar es Salaam halafu afanye *connection* nyingine ya usafiri kuja Dodoma, huo bado ni upungufu katika uanzishwaji wa Makao Makuu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo halitoshi, bado Dodoma ilitakiwa iwe na masoko ya kisasa, iwe vilevile na *community centre*, masuala ya *tourism and information centre* na mambo kadha wa kadha. Pamoja na hayo, bado hata huduma zile za kijamii ambazo zinahitajika kama vile maeneo ya masoko, hata hizo *community centres* bado hazipo. Kwa hiyo, naona iliikuwa Serikali ifanye haraka kuweka miundombinu ambayo itasadia kurahisisha hizo huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulisema ni mpangilio wa maofisi yanavyojengwa. Moja ya sababu zilizosababisha Dar es Salaam kuwa na foleni nyingi ni huduma nyingi za Serikali kuwekwa upande mmoja. Sasa nashauri, maofisi haya ya Serikali pamoja na Wizara yasiwekwe katika eneo moja tu; yanapowekwa katika mtindo huo, ndiyo foleni zinapokuwa nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza wafanyakazi wanapotoka kwenda katika ofisi zao, lakini pia hawa wananchi wanaotaka huduma nao watakuwa wanasababisha foleni zisizokuwa na sababu. Kwa hiyo, miundombinu au ofisi zijengwe kutokana na hali nzima ya kijografie. Pawe na usambazaji wa ofisi ili huduma zipatikane maeneo tofauti watu wasielemee upande

mmoja. Hata huo usalama pia ni vizuri ikiwa hizi Ofisi za Serikali zimesambazwa kutokana na hali ya kijiogafia ya Mji wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nalionা, tumeona kwamba hata hizi huduma za Serikali au shughuli za Kiserikali ama hizi sikukuu za Kitaifa; kwa mfano, hakuna uwanja ambao umeandaliwa hapa wa shughuli za Kiserikali au Sikukuu za Kitaifa. Sasa utakuta shughuli zote zinazofanyika tunafanya katika Uwanja wa Jamhuri, uwanja ambao *original* yake ni uwanja wa michezo ya mpira. Kwanza tunafanya uharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri basi tungkuwa na eneo maalum la uwanja ambao utakuwa unajulikana kwamba hapa panafanyika shughuli za Kiserikali na kuondoa uharibifu wa kiwanja kile ambacho ni cha michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo halitoshi, amezungumza msemaji aliyejipa hapa, ameitaja Katiba Ibara ya (4), lakini ni kweli ukiangalia Tanzania ni Muungano wa nchi mbili. Inapokuwa nchi mbili zimeungana, basi kweli lazima haki itendeke. Ukienda katika hii *preamble* kwenye ukurasa wa tatu hapa, kwenye *application*, pana sehemu namba mbili imesema: "*This Act shall apply to Mainland Tanzania as well as in Tanzania Zanzibar.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirudi kwenye kitabu cha Kamati sasa, wametajwa wadau hapa. Nafikiri ingekuwa ni vyema kweli kama kwenye hawa wadau napo angalau japo NGOs moja nayo kutoka Zanzibar ingetoa maoni, lakini hakuna. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wametajwa hapa wadau kwamba ni Chama cha Wanasheria, *Tanganyika Law Society*, kimetajwa Kituo cha Sheria cha Haki za Binadamu *Legal and Human Right Centre*, imetajwa Taasisi ya Twaweza, Kimetajwa Chuo cha Mafunzo ya Serikali za Mitaa Hombolo, ametajwa Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma, lakini ukiangalia wadau kutoka Zanzibar hawapo...

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi niseme pamoja na kwamba yanazungumzwa kwamba kwenye Kamati watu walijadili...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbarouk, hebu subiri taarifa hiyo.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naheshimu sana mchango wa mzungumzaji anayeendelea. Amezungumzia mchango wa *NGOs* mbalimbali kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu kumkumbusha kwamba, Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika ni Mzanibari.

MBUNGE FULANI: Haihusu.

MWENYEKITI: Unasemaje kuhusiana na Taarifa hiyo Mheshimiwa Mbarouk?

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei taarifa kwa sababu, hapa imetajwa kwamba ni *Tanganyika Law Society* haikutajwa Tanzania. Sasa hiyo taarifa siipokei. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachosema ni kwamba mambo mengine yanapofanyika hakuna haja ya kutetea jambo ambalo kila mtu anaona wazi kwamba hii ni dhuluma. Wakati mwengine tunajititia doa bila ya sababu. Kila mchangiaji anayesimama, hakuna anayepinga kuhamishiwa Makao Makuu Dodoma, lakini tusitoe mwanya wa watu wengine kulalamika kwa sababu hili jambo tunaona ni dogo, lakini linaweza kugeuka kama tone la mafuta ya taa juu ya meza. Tone moja tu la mafuta ya taa, moja tu ukiliangusha juu ya meza usiku, asubuhi unakuta meza yote imelowa. Hilo nimetoa kama ushauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwenye suala zima la fidia. Ni kweli kwamba Makao Makuu yanahamia Dodoma, lakini wapo wananchi ambao wana mashamba, wapo ambao wana maeneo, lakini maeneo yao yanachukuliwa. Ukienda katika Sheria Na. 4 ya Mwaka 1999 inasema: "*whether you have a title deed or not, so long you have been there for a long time customary law recognise you as the owner of the land.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa wananchi maeneo yanachukuliwa kwa kisingizio tu kwamba Makao Makuu inahamia Dodoma na ardhi ni mali ya Serikali. Hii sheria inakiukwa. Ametaja mzungumzaji mmoja hapa, lakini wapo watu wengine ambao maeneo yao yamechukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yupo bwana mmoja anaitwa Gilbert, kuna bwana mwingine anaitwa Msafiri na kuna dada anaitwa Anna na mwingine Mariam, hawa ni watu ambao niko nao, ni majirani zangu kidogo. Maeneo yao yanachukuliwa na Sheria Na. 5 inasema hakuna ardhi ya bure hata kama kuna mradi wa maendeleo ya Serikali, lazima Serikali mwenye eneo lake na taasisi inayotaka kuleta maendeleo watu wakubaliane kwanza. Hata hivyo, kinachotokea wananchi wetu wanadhuluiwa, wanachukuliwa maeneo hali ya kuwa wengine wanaambiwa watapelekwa Mtumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sehemu hiyo wanayochukuliwa na ukifkiria huko Mtumba anakwenda kukabidhiwa kiwanja wakati yeye ameshakuwa ni mtu mzima, hajiwezi tena, hana kipato cha kuweza kujenga makao. Kwa hiyo, nashauri kwanza hata kama unataka kupitishwa mradi wa maendeleo, wananchi wa eneo hilo walipwe fidia yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulisema ni suala zima la miundombinu. Kwa mfano, barabara, kweli barabara zinajengwa, lakini hazina vivuko vyatuhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri basi, hata hapa kwenye Bunge, jana katika *briefing* lilizungumzwa na baadhi ya Wabunge wenzetu wameshapata ajali pale. Kwa nini basi halijengwi daraja kama lile la Manzese au la pale Buguruni? Isiwe Bungeni tu, hata maeneo mengine ambayo ni barabara kubwa kwa wananchi yajengwe ili kuepusha ajali na kuokoa maisha ya Watanzania. (*Makofii*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jaku, dakika tano. Mheshimiwa Jaku, kama hayupo basi, kwa heri.

Haya, tunaendelea sasa na upande wa Serikali. Tutaanza na Mheshimiwa Mavunde dakika 10, Mheshimiwa EngineerManyanya dakika tano, Mheshimiwa Nditiye dakika tano na Mheshimiwa Kandege dakika 10. Tunaanza na Mheshimiwa Mavunde.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Awali ya yote napenda nichukue fursa hii kwanza kabisa kuipongeza sana Serikali yangu ya CCM kwa Awamu zote kuanzia wakati wa Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, wakati wa Rais Mstaafu Mwinyi, wakati wa Mzee Mkapa na wakati wa Mzee Kikwete. Wote hawa kwa pamoja waliendelea kuyaishi na kutekeleza kwa vitendo yale maamuzi ya mwaka 1973 ya kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa sababu ukiangalia kwa mujibu wa historia ya Dodoma inavyosema, katika mwaka 1912 mpaka mwaka 1915 eneo la Dodoma hapa katikati lilikuwa lina majengo 26 tu ambapo wakati wa ukoloni Wajerumani waliona umuhimu wa kuifanya Dodoma kuwa sehemu ya Makao Makuu yao ya shughuli mbalimbali na wakachagua eneo la katikati kuwa sehemu ya Makao Makuu ya shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1932 Waingereza pia na wenyewe waliona umuhimu wa kuifanya Dodoma kuwa sehemu ya Makao Makuu yao kwa shughuli mbalimbali. Kwa hiyo, suala hili la Makao Makuu ya Dodoma halijaanza leo, limeanza tangu wakati wa ukoloni, waliiangalia Dodoma, wakaona umuhimu wake wakaipa sifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1973, kama wenzangu walivyosema, yalifanyika maamuzi makubwa sana ya kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi. Tunashukuru kwamba baada ya miaka mingi tangu uamuzi huo, Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imefanya mambo makubwa sana kwa maamuzi sasa ya kuhamishia kivitendo kabisa Serikali yote kuwa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba uamuzi huu ni sahihi na umekuja kwa wakati muafaka. Nasi kama wananchi wa Dodoma tunamuunga mkono sana Mheshimiwa Rais na tuko tayari na tumeshaupokea ujio huu wa Makao Makuu na tunatoa ushirikiano wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yanatokana na llani ya Uchaguzi ya CCM. Ibara ya 151(a); mimi nilipata bahati ya kuwa mmoja kati ya watu walioandika llani ya Uchaguzi ya CCM. Moja kati ya eneo ambalo tulilisema kwamba lazima tulifanyie kazi ni kuitambua Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi kwa mujibu wa sheria hasa baada ya kuwa kuna tamko la mwaka 1973, lakini tukasema sasa iwe kwa mujibu wa sheria. Leo nasimama hapa kwa furaha kubwa kwamba Chama changu kimetekeleza llani yake ya Uchaguzi kwa leo kuleta Muswada wa sheria wa kuitambua Dodoma kama Makao Makuu ya nchi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye sheria yenye. Sheria hii ambayo leo tunaijadili, kwa kweli inaleta jambo lenye tija sana kwa wananchi wa Dodoma kwa kiu yao kubwa ya kutaka kuwepo na utaratibu maalum wa kuitambua Dodoma kama Makao Makuu. Kwa ujio wa sheria

hii maana yake ni kwamba, tunakwenda kutengeneza utaratibu sasa wa kisheria wa kuitambua Dodoma na kwa mujibu wa Kifungu cha 4(1) cha Muswada huu kimetamka rasmi sasa kwamba Dodoma inatambuliwa kama Makao Makuu ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 4(2) cha sheria hii kimeweka pia utaratibu mzuri kwamba, hakutakuwa na mabadiliko mengine yoyote yatakayofanyika katika maamuzi haya pasipo kupitishwa na *two third* ya Wabunge wote katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii inatupa *assurance* kwamba, uamuzi huu wa Serikali utaendelea kulindwa kwa sheria hii ambayo tunaitunga na ni jambo ambalo sasa linafanya Dodoma kwa utambuzi wake huu na sisi tupate amani kwamba Dodoma itaendelea kuwa Mkao Makuu ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa hoja pia hapa kuhusu kuupanga Mji wa Dodoma na miundombinu ya Dodoma. Katika hili naomba niwambie Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kama watu hawana taarifa sahihi siyo vyema kuzungumza mambo ambayo hawana uhakika nayo. Katika Jiji la Dodoma kati ya miji ambayo imepangwa vizuri Tanzania Dodoma ni mmojawapo. Hili halina ubishani. Dodoma ni kati ya miji iliyopangika vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha miezi sita tangu mwezi wa Tatu mwaka huu mpaka mwezi wa Tisa vimepimwa zaidi ya viwanja 20,000 ambavyo lengo lake ni kuufanya mji huu sasa uwe umepangika na kuondoa ujenzi holela. Hivi sasa ninavyozungumza mpango ule wa *Master Plan* ya Dodoma ambapo kuna baadhi ya watu, hasa Mheshimiwa aliyetoka kuchangia hivi sasa alikuwa anabeza kwamba hata shughuli za Kitaifa tunategemea Uwanja wa Jamhuri, hatuna sehemu ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika *Master Plan* ya Dodoma ambayo itakwenda kuzinduliwa rasmi nafikiri Desemba mwaka huu, utaona katika maeneo ambayo yamepangwa vizuri, eneo la Mtumba ambako ndiyo

kutakuwa kuna Mji wa Serikali na Mabalozi wote wako pale, pale inakwenda kujengwa *park* kubwa ya Kitaifa ambayo Mheshimiwa Rais, Viongozi wa Kitaifa wote wakitaka kuhutubia Taifa watakuwa na eneo maalum, kama ilivyo Marekani vile, atakaa sehemu, eneo maalum, atahutubia Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, eneo hilo la Mtumba ambako tumewapa viwanja Mabalozi na Mji wa Serikali umeshapangwa vizuri. Ninavyozungumza hivi sasa, miundombinu yote imeenda ya maji na umeme, imebaki ya barabara tu. Tukumbuke haya mambo huwa hayawezekani *over night* tu, miji yote imejengwa kwa utaratibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa hoja hapa kuhusu barabara kwamba Dodoma hakuna barabara za kutosha, barabara nyingi za vumbi. Narudia tena kwa wale wote ambao hawana takwimu sahihi, wasizungumze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Dodoma ndio Jiji la pili ukichukua Halmashauri zote nchi nzima, Manispaa za Wilaya na Majiji yote, Dodoma ndiyo ya pili kwa mtandao wa barabara za lami. Kwanza ni Kinondoni, ina kilomita 136 na ya pili ni Dodoma ina kilomita 130.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu wa fedha tumetenga kiasi cha shilingi bilioni tano kwa ajili ya kuongeza barabara za lami, lakini tuna mradi wa *TSP* wa shilingi bilioni 40.9 ambao utaongeza kilomita 26 za barabara za lami. Tafsiri yake ni nini? Tafsiri yake ni kwamba mwakani Dodoma ndiyo itakayoongoza nchi nzima kwa mtandao wa barabara za lami. Hakuna Jiji lolote, Manispaa yoyote wala Halmashauri yoyote ya Wilaya itakayofikia Dodoma kwa mtandao wa barabara za lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumza pia hoja ya kwamba hakuna miundombinu, masoko na vivutio mbalimbali. Wiki tatu zilizopita na Mheshimiwa Jafo alikuwepo kwenye kushuhudia, umesainiwa mkataba wa

shilingi bilioni 78. Mkataba huo unakwenda kujenga miundombinu ya Dodoma likiwemo soko ambalo limezungumzwa hapa hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kujenga soko la kisasa nafikiri kuliko mengi ya Afrika Mashariki na Kat; tunakwenda kujenga stendi kubwa ya mabasi ambayo itakuwa ina uwezo wa kuegesha mabasi, magari madogo, bajaji na bodaboda 600 kwa wakati mmoja. Hali kadhalika zinakwenda kujengwa barabara ambazo ni *outer na inner ring roads* za kuondoa msongamano katika eneo letu hili la Dodoma. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napata mashaka nikiona watu wanazungumza mambo ambayo hawayafahamu. Uamuzi wa huu ni sahihi na Serikali illichokifanyi ni sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kwa kumalizia hoja yangu, Waheshimiwa Wabunge wengi wa Upinzani wamesimama hapa wanasema, sisi tuna hoja moja tu kwamba Dodoma ni katikati ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaongezee nyingine...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa.

NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU KAZI, AJIRA NA VIJANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa *Eng. Stella Manyanya*, dakika tano.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niungane na wale wanaopongeza Muswada huu na kwa kweli kwa heshima kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa maamuzi makubwa na mazito anayoyafanya katika kuhakikisha kwamba nchi yetu inapiga mchaka mchaka wa maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kwa wale wanaomheshimu Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, hawawezi kuwa kinyume na Muswada huu. Vilevile Muswada huu unatokana pia na maamuzi mazito ambayo yalifanyika siku ya kishujaa wakati Mheshimiwa Rais wetu tarehe 25 Julai, 2016 alipotoa maagizo ya Serikali kuhamia Dodoma. Hakuachia hapo, vilevile tarehe 26 Aprili, 2017 alitoa tena maamuzi ya kishujaa ya kindugu ya kusema kwamba sasa Dodoma liwe ni Jiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitanukuu kamili lakini ni kwamba nakumbuka alisema hivi: "Tanzania tuna Majiji matano, lakini Makao Makuu ya nchi siyo Jiji, kwa sababu zipo?" Kwa hiyo, ina maana ni mtu ambaye amekuwa akifikiria akiona ni kwa nini mambo yamekuwa tofauti wakati Dodoma ilikuwa inastahili toka siku nydingi iweze kupewa hadhi yake kama Makao Makuu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa najiuliza, hivi ni vivu kwa sababu sasa Dodoma inapewa haki yake au ni nini? Kama siyo vivu, basi wote tutaungana mkono kuhakikisha kwamba haya mambo mazuri ambayo yamepangwa yanafanyika vizuri na tunayatekeleza ipasavyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi siku tulipoambiwa kwamba tunahamia Dodoma kama Serikali niliogopa kidogo na mpaka tuliulizana na wenzetu, hivi inawezekana? Kumbe imewezezana, Serikali iko Dodoma,

wafanyakazi wapo Dodoma na huduma zimezidi kuwa nzuri na wananchi wengi wanafurahia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kwamba ndugu zangu hebu tuachenii mambo ambayo kila wakati tuwe kama tunavutana tu. Siyo vibaya kuchangia katika kuboresha, lakini kukataa mambo ambayo ni ya msingi nadhani pia inatuvunjia heshima yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba maandalizi kama ambavyo imezungumzwa yalianza siku nydingi. Sisi kweli Serikali baadhi yetu tupo pale Chuo Kikuu cha *UDOM*, lakini na yenyele ilikuwa ni katika mchakato huo huo wa kuhamia Dodoma. Tatizo liko wapi? Kwa hiyo, nilitegemea kwamba wote tutaungana mkono katika kutoa mbinu mbalimbali ya kufanya Jiji hili la Dodoma, Makao Makuu yetu ya nchi yawe mazuri, yapendeze, yavutie na yawe na urembo kama ambavyo sisi wenyele tunapendeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kwanza nisije nikasahau, niwahamasishe wawekezaji mbalimbali wa viwanda na biashara kuja kuwekeza Dodoma. Dodoma ni mahali pazuri kwa kufanya biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuatilia sana, kuna watu ambaao ni wagumu sana katika kufanya maamuzi. kwa upande wa sisi Wanasyansi tunasema kuna *emitter* na *followers*, kwa hiyo wenyele kazi yao ni ma-*follower*, mpaka kwanza wengine waanze ndiyo wao wafuate. Ukifuatilia hata kwenye jambo hili, nafananisha na suala la umeme. Kwa muda mrefu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Shukrani. Mheshimiwa *Engineer Atashasta Nditiye*, dakika tano.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na ndugu yangu Mheshimiwa Anthony Mavunde kwamba pamoja na mipango mbalimbali ya Serikali ya Mkoa wa Dodoma kuhakikisha barabara zinapitika lakini Wizara yangu kupitia bajeti ya Serikali Kuu iliopitishwa mwezi wa Sita, vilevile tuna mipango yetu ya kuhakikisha kwamba barabara nyingi sana, zile za *inner and outer ring roads* zinarekebishwa. Natoa shukrani za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge hasa wale wote ambao walisema ndiyo kwa bajeti ya Serikali yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge ambao kwa kweli kwa wingi wao wote, karibu wote hawana *doubt* wala kipingamizi na Makao Makuu kuhamishiwa hapa kwamba sisi kama Serikali kwa upande wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano tumejipanga vizuri sana kuhakikisha kwamba barabara zetu zote zitakuwa imara na zinapitika wakati wote katika Jiji letu hili la Dodoma. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuwatoa hofu hasa Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa kutoka maeneo ya Zanzibar kwamba Wizara yangu kupitia Sekta ya Uchukuzi tumeendelea kufanya utaratibu wa kuhakikisha kwamba Shirika letu la Ndege sasa linakuwa na safari za mara kwa mara kutoka Zanzibar kupitia Dar es Salaam mpaka Dodoma na maeneo mengine tena ya nchi kuhakikisha kwamba mji wetu unafikika kwa urahisi sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunapozungumza, kuna taratibu za mwisho mwisho kabisa zinaendelea kukamilishwa na Shirika letu la Ndege kuhakikisha kwamba kwa kuanzia mwisho wa mwezi huu kutakuwa na safari ya kutoka Zanzibar kupitia Dar es Salaam mpaka Dodoma. Ndege hiyo itaungana na ndege nyingine ambayo

itakuwa iko Dar es Salaam kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma siku za Jumatatu asubuhi. Hata hivyo, Ijumaa jioni pia tunaendelea kufanya utaratibu wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na ndege mbili ambazo zitakuwa zinatoka Dodoma kwenda Dar es Salaam mpaka Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala lililoonjelewa na ndugu yangu Mbunge wa Bahi ambaye alizungumzia uboreshaji wa uwanja wetu huu uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie pamoja na Wabunge wenzangu kwamba uwanja wetu huu uliopo mpaka sasa hivi kuna shilingi bilioni 3,700 ambazo Serikali kupitia *TAA* wametoa kwa ajili ya kulipa fidia tuweze kupanua uwanja wetu kwa mita 150 zaidi ili huo uwanja sasa uweze kutumika masaa 24. Kabla ya wiki mbili tuna hakika hizo pesa zitakuwa zimelipwa kwa wananchi ili angalau waweze kupisha upanuzi wa uwanja huo tuweze kuruka masaa 24. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ili niokoe muda, tayari taratibu mbalimbali za ujenzi wa uwanja mpya wa Msalato zimeanza. Marejeo ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina tayari yamekamilika kwa asilimia mia moja na sasa hivi kinachomalizika ni michoro, lakini tuna uhakika wa kupata fedha kwa sababu tupo kwenye mazungumzo ya mwisho kabisa na *African Development Bank* kwa ajili ya mkopo rahisi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa uwanja huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini baada ya hapo tutapata huo mkopo na tutatangaza tenda kwa ajili ya kupata Wakandarasi makini na wazuri amba watatujengea uwanja mkubwa na wa kisasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nichangie hayo kuhusu upande wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer Nditiye*, Mheshimiwa Josephat Kandege, dakika kumi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa uliyonipatia ili niweze kuchangia hoja yetu ambayo ililetwa mezani kwako leo na ikapata wachangiaji wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha sisi sote kushiriki tukiwa na afya njema. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba kipekee nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa busara ambao Watanzania walishubiri kwa muda mrefu na sasa ndoto ambayo ilikuwa ikiotwa na Watanzania ya Makao Makuu kuwa Dodoma imetimia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Kamati yetu chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Jasson Rwekaza ambao kiuhanika wameutendea haki Muswada huu. Muswada ulikuwa unaonekana kama ni mfupi sana lakini umesheheni mambo mazito kweli kweli; na Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kuchangia, hakuna mtu ambaye alitarajia kwamba wangeweza kuchangia kwa kiasi hiki kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ambalo tunakubaliana sote, hakuna hata Mbunge mmoja ambaye hakubaliani na Muswada ambao umeletwa na ndiyo maana hapo kwako huna hata *addendum* moja ambayo inapingana na hoja ambayo imeletwa na Wizara yetu. Naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatofautiana tu katika *style* ya kusema, lakini nia njema unaiona. Unaweza

ukazunguka lakini mwisho wengine wanashindwa kuunga mkono, lakini kimoyomoyo wanakuwa wameunga mkono. Kama wasingeunga mkono ungeona *addendum* zipo hapo. Kwa hiyo, kipekee naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niptie baadhi ya maeneo ambayo yamechangiwa, tukianzia na Mheshimiwa Rweikiza ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati yetu ambayo inafanya kazi nzuri kabisa. Katika maeneo ambayo walipata wadau kuchangia, wadau waliomba kama inawezekana Muswada huu ukaunganisha na sheria nyiningine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupita kwa Muswada huu kuwa sheria, inafungua sheria nyiningine ambazo zitakuja zitungwe ili kuwezesha Makao Makuu *i-operate* kwa namna ambavyo tunatarajia. Isinge kuwa rahisi bila kuanza na Muswada huu kupita kuwa sheria ili kutangaza Dodoma kama Makao Makuu ya nchi rasmi ili vyovvye vile sheria nyiningine zije kutungwa katika namna bora ya kuendesha Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa hatutendi haki tukidhani kwamba kwa *operation* jinsi ilivyo, kwa muundo wa sasa, Makao Makuu yetu ambayo tunatamani yalingane na hadhi ya nchi yetu ya Tanzania, yanaweza kuwa vizuri kwa sheria hizi zilivyo. Kwa hiyo, ni vizuri tukubaliane kwamba tutavuka daraja tukifika wakati huo. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Miswada italetwa ili tuwe na namna bora ya kuenenda na kuhakikisha kwamba Jiji letu la Dodoma linakuwa katika hali ambayo sisi sote tunatamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ambayo ililetwa na Mheshimiwa Japhary ambaye ni Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii, akasema kwamba vikao vya kisheria havikufuatwa. Naomba nimtoe hofu kwamba hakuna hata moja ambalo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inafanya bila kuwa *cautious* kuhakikisha

kwamba taratibu na sheria zote zinafuatwa, vikao vyote vya kisheria vimefuatwa na mpaka kufikia hapa tupo salama salmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ally Saleh amesema kwamba Zanzibar haikuhusisha. Naomba nimtoe wasiwasi, naamini kabisa alipo pale ni sauti ya Wazanzibari kwa sababu tusingeweza kuwajaza Wazanzibari wote wakaingia humu. Yeye ni mwakilishi na amekuwa akifanya kazi nzuri pamoja Wazanzibar wengine ambao wanasema kwa upande huo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tukubaliane sisi sote kwamba...

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tukubaliane kwamba ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambalo lina uwakilishi kutoka pande zote mbili na kwa namna ambavyo tunaenda vizuri, leo hii asubuhi Mheshimiwa Kakunda, Naibu Waziri, ameondoka kwenda Zanzibar kwenda kushirikisha Baraza la Mapinduzi Zanzibar jinsi ambavyo tunataka mambo haya yaende vizuri tukiwa tunashirikisha pande zote. Hii ni kwa sababu nia ya dhati njema iko pale. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa nasema ni kwamba ili tuwe na uelewa wa kufanana isije ikaonekana kwamba wengine hawalelewi hili ndiyo maana mwenzangu ameondoka kwenda Zanzibar kwenda kujadiliana na Baraza la Wawakilishi Zanzibar kuhusiana na tamko hili la uanzishwaji rasmi wa Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Saleh amesema kwamba Watanzania hawajawahi kuhusisha. Naomba nimkumbushe kwamba mwaka 1973 jumla ya matawi yaliyoulizwa yalikuwa 1,559 juu ya Makao Makuu ya nchi

kuhamia Dodoma. Jumla ya matawi 842 yalisema Makao Makuu yaendelee kubaki Dar es Salaam na jumla ya matawi 1,017 yalisema Makao Makuu ya nchi yahamie Dodoma.

WABUNGE FULANI: TANU.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikiwasikiliza kwa ustaarabu kabisa. Ni vizuri nimalize, dakika kumi siyo nyingi sana Mheshimiwa Halima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Msigwa amesema kwamba tumekurupuka, vipaumbele ni vingi, lakini naomba nimhakikishie kwamba katika vipaumbele na sisi Wana-CCM ambao tulienda kujinadi kwa Wana-CCM na tukapewa ridhaa ni pamoja na kuweka bayana kwamba tunaenda kuhamia Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni jambo ambalo lilikuwa katika mpango wetu mahsusii siyo kwamba tumeamka nalo jana. Wakati tunaenda kuomba kura kwa wananchi 2015 tulilisema bayana na tukaaminiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wajumbe ambao wamesema kwamba *master plan* iliyokuwa imepangwa kwa wakati ule itakuwa imepitwa na wakati. Ni kweli, ndiyo maana ipo haja ya kuipitia kwa kadri ya wakati na sisi tupo *flexible* kuhakikisha kwamba Jiji letu la Dodoma linakuja kuakisi sura hasa ya Tanzania ambayo tunaitaka, Tanzania ambayo tulikuwa tunaiota, sasa tunakwenda kutekeleza. Maana sura ya kwanza ya Taifa lolote ni Makao Makuu ya Nchi na Dodoma ndipo ambapo tunakusudia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa baada ya Muswada huu kuwa sheria, hakika tutakuwa tunahitaji bajeti *special* ya kuhakikisha kwamba Dodoma inajengeka ili iakisi taswira ya Tanzania ambayo tunaitamani. Maana siyo kwamba kila tukienda nchi za wenzetu, ukienda Afrika ya

Kusini unaanza kutamani jinsi Pretoria na Johannesburg zilivyojengwa na wenzetu nao kuna baadhi ya vitu walivikosa wakasema tunataka kujenga miji yetu iwe ya kisasa na hiki ndicho tunaenda kufanya Dodoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa heshima zote, kama nilivyo tangulia kusema, hoja hii imeungwa mkono kwa pande zote na ndiyo maana hakuna *addendum* hata moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Josephat Kandege kwa mchango wako mzuri na mfupi. Sasa namwita mtoa hoja ahitimishe hoja yake kwa muda usiozidi dakika 30. Mheshimiwa Jafo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda sana kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha sisi sote kwa usalama na uweza wake kwanzu kurejesha katika Bunge hili tena kwa mara nyingine, lakini kwa kuweza kupitia mjadala huu tokea asubuhi mpaka saa hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kazi kubwa alioifanya na mpaka leo hii tumeleta Muswada huu Bungeni ili Waheshimiwa Wabunge waweze kujazia nyama na mwisho wa siku hii *declaration* iweze kupita rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu wazi kwamba nami nilidiriki katika Bunge la Kumi na hapa ilifika muda kwamba kila mtu alikuwa anasema, kwa nini Serikali mnasema Dodoma na kwa nini Dodoma hamfanyi uwe mji wa Vyuo Vikuu kwa sababu Serikali mmeshindwa kuhamia Dodoma? Leo hii nimeona katika Bunge hili la Kumi na Moja ilani imeelekeza, Mheshimiwa Rais anatekeleza ilani na Mheshimiwa Spika alikuwa akisherehesha hili. Leo hii tumeona kwamba Waheshimiwa Wabunge wote na Serikali kwa

ujumla wetu tunapitia mjadala wa Muswada huu ambapo mwisho wa siku tutakuwa tunasema Dodoma ndiyo Makao Makuu yetu rasmi kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kiwango kikubwa Muswada huu umechangiwa na Wabunge wengi. Hapa naona kwamba Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuongea wako 32 na wale waliochangia kwa maandishi wako watatu. Ukiona ndani ya muda mfupi tumepata sherehe kubwa sana ya Wabunge hivi, hii ni hekima kwamba kila mtu alikuwa na hamu ya jambo hili na mwisho wa siku Wabunge wote wameshiriki, nami nimefurahi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli niseme wazi kwamba, nilipokuwa nikiwafuatilia Waheshimiwa Wabunge wote, nillichogundua ni kwamba katika Wabunge wote, kila mtu ana nia njema na Muswada huu na hii kuwa sheria isipokuwa ni maboresho tu ya uchangiaji, na ndiyo sarakasi zenyewe za Bunge, la sivyo Bunge halipendezi. Kwa hiyo, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge katika pande zote mbili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majina ya wachangiaji nitawasilisha kwa *Hansard*, yatakuwa yamerekodiwa. Niende moja kwa moja katika hoja lakini niwashukuru sana Waheshimiwa Naibu Mawaziri, kwanza walipokuwa wakichangia, pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya kutoa fafanuzi mbalimbali. Nami kazi yangu itakuwa ni ndogo sana kwa sababu mambo mengi sana kwa upande wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali alitoa ufanuzi katika suala zima la Sheria ya Jiji, sitaki niende tena huko. Kwa upande wa Wabunge wengi sana walijadili hoja mbalimbali zenyewe kuweka muktadha wa kusaidia kuona jinsi gani sheria hii ina umuhimu sana kwetu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kuna hoja moja kubwa sana ambayo *ili-surface* ya suala zima la Zanzibar kwamba mbona haikushirikishwa katika hili? Naishukuru

kwanza Kamati kwa sababu chini ya Mheshimiwa Rweikiza na Mheshimiwa Mama Mwanne Mcemba na Kamati yote ya Bunge kwa ujumla wake, Mheshimiwa Bobali na watu wote, wameshiriki nya kutosha na tulijaza nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie kwamba *consultation* ya maelekezo yenu yote Kamati tuliweza kushirikisha maeneo yote ya Kiserikali, mambo yote yamekuwa mazuri. Kwa hiyo, naomba niwatoe shaka Waheshimiwa Wabunge katika eneo hilo kwamba jambo hili tunalojadili hapa lina baraka zote, wala msiwe na hofu. Hii ni kazi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Serikali ni kusikiliza maelekezo ya Wabunge na Kamati ya Bunge. Naishukuru sana Kamati ya Bunge, bahati nzuri ilifanya *diversification* ya huu Muswada mara nyingi sana ikashirikisha wadau mbalimbali na siyo maelekezo yao. Ni kweli niseme kwamba tulipata maelekezo nasi tukafanya ushirikishaji wa aina yote. Kwa hiyo, niwatoe shaka Waheshimiwa Wabunge wote kwamba jambo hili ushiriki wake umekwenda vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tupo katika mchakato mwininge wa sheria ya jinsi ya kuendesha Jiji la Dodoma. Sheria hii nadhani itasomwa tena kwa mara ya kwanza siyo muda mrefu sana, ndiyo maana hapa unaona timu ya Naibu wangu, Naibu Waziri wa Muungano vilevile na timu ya Wanasheria, leo hii wanakutana na wenzetu wa Zanzibar kwa upande mwininge wa sheria nyingine. Lengo kubwa ni kwamba jambo la Dodoma sasa liende vizuri wala lisiwe na mashaka ya aina yoyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasi kama Watanzania na hasa Waheshimiwa Wabunge ninyi naomba niwaambie, katika watu ambao wataweka *legacy* ambayo haijawahi kufanywa na mtu yejote ni ninyi Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili ambao mko humu ndani. Wenzetu wengine wengi walipita humu ndani, walijadili, hata akina Mheshimiwa Mzee Lubeleje walipokuwa katika Ukumbi wa Karimjee pale mwaka 2000 wamejadili jambo hili. Mpaka Mheshimiwa

Lubeleje amekuja hapa, lakini mara hii sasa sheria hii inakuja Bungeni kwa mara ya kwanza, ninyi Waheshimiwa Wabunge mna heshima kubwa sana katika nchi hii kwa kweli. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja mbalimbali zilijadiliwa na hasa kuhusu nini kifanyike katika Jiji la Dodoma. Watu wengine walizungumza wakasema kwa nini sasa tunaelekeza huku tunaacha miundombinu ya afya hakuna? Naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge, nchi yetu kwa kweli imejielekeza sana na ninyi mnafahamu, katika mambo ya kihistoria ambayo tunayafanya Tanzania kama nchi ni sasa hivi. Ukiangalia Waheshimiwa Wabunge wengine wanasesma kwa nini tusijadili Sekta ya Afya? Dada yangu, Mheshimiwa Ummy Mwalimu hapa ni shahidi, anafahamu naye ni *custodian* wa Sera ya mambo ya Afya; na siku zote tunasema kwamba hata kuhamia Dodoma, hatukuacha uwekezaji mkubwa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata Sekta ya Afya katika suala zima la dawa, tumeongeza bajeti ya dawa kutoka shilingi billioni 31 mpaka shilingi billioni 269. Hii maana yake Serikali inafanya kazi kubwa sana. Ujenzi wa miundombinu kihistoroia haijawahi kutokea ndani ya mwaka mmoja kujenga vituo karibu 210 na tunajenga vituo vingine. Hata hivyo, tunajenga hospitali nyingine za Wilaya 67 mpya. Hii ni *investment* Serikali inafanya, tunahamia Dodoma na tunafanya mambo mengine makubwa ndani ya nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine walizungumza kwamba mbona miundombinu haiko sawasawa? Bahati nzuri Mheshimiwa Mavunde alizungumza, nami nilikuwa mgeni rasmi hapa, Waheshimiwa Wabunge wakumbuke siku ya tarehe 14 Mei, wakati na-table hapa bajeti yangu nilikuwa nazungumzia Jiji la Dodoma. Wakati natoka mlangoni hapa, mtu mmoja akaniambia Mheshimiwa Jafo, hii sasa nadhani ni *comedy*, hakuna kitu kama hicho kitakachofanyika. Nilimwambia tutajenga stendi, tutatengeneza soko na tutaweka *ring road*, Dodoma hii tutaifanya ibadilike. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie, siyo muda mrefu sana, tumesaini mkataba wa shilingi bilioni 77.6, hilo ni eneo moja ambalo tunajenga soko la kisasa na Mheshimiwa Mavunde amesema haliko popote hapa nchini kwetu. Tunajenga stendi ya kisasa yenye ekari 84, hakuna hapa nchini kwetu. Juzi juzi tayari kazi ya ujenzi wa barabara mbalimbali tunazitengeneza. Hata sasa hivi kule Nala tunajenga stendi ya malori ambayo hakuna nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii watu wengine na Waheshimiwa Wabunge mnafahamu, hata hizi taa ambazo mnaona zinakwenda katika uwanja huu wa zamani wa *airport* tumezihamisha kwa sababu tumejenga pale barabara mpya kupitia *TARURA*. Kwa hiyo, tuna *investment* kupitia miradi ya *TSP* na tuna *investment* kupitia *TARURA*. Kwa hiyo, niwatoe shaka, katika Jiji ambalo litakuwa *unique* ndani ya Tanzania, ni Jiji la Dodoma, hakuna lingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo tumetoa maelekezo, ni marufuku kujenga kiholela Dodoma, kwa sababu tunataka jiji lenye sura tofauti kwa sababu ndiyo Makao Makuu ya nchi yetu. Upimaji unaendelea; tumeshapima viwanja zaidi ya 20,000. Sasa hivi tuna mpango wa kupima viwanja vingine zaidi ya 20,000 maeneo ya Mkonze na maeneo mengine kule ndani ndani, maeneo ya Mtumba kule mbele. Tunafanya hivi ili Dodoma iweze kubadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie, hata ujenzi wa nyumba zetu, kwa ajili ya mustakabali wa kuwa na Jiji la Dodoma, tumetoa maelekezo, nanyi Waheshimiwa Wabunge naomba niwasihii, najua mmenunua viwanja. Tunajenga Dodoma kwa sura tofauti. Ukitaka kujenga uliza, bati yako ina rangi gani? Ukiijenga kiholela maana yake utapata taabu tena kupiga rangi pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia yetu ni nini? Dodoma itakuwa na ladha tofauti. Kuna ukanda utakuwa na bati ya bluu, kuna ukanda utakuwa na bati nyekundu, kuna ukanda

utakuwa na rangi nyingine. Hiyo ndiyo Dodoma mpya, ndiyo Makao Makuu ya Nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika suala zima la kufanya Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali imejipanga vizuri. Niwasih sana, wakati mwengine kwa sababu najua tuko *busy* sana tukiwa hapa Dodoma, tutembee maeneo mbalimbali, hata ikiwezekana kuna maeneo mengine hayatembeleki lakini unaweza ukatembea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Waheshimiwa Wabunge, nendeni mkatembee hata dampo japokuwa siyo vizuri kutembelea dampo, lakini unaweza ukaenda dampo, ukawa na chipsi zako unakula. Hii ni *unique structure* ya Dodoma. Dampo la Dodoma huwezi ukakuta hata inzi mmoja kwa ajili ya maandalizi ya Makao Makuu ya Jiji la Dodoma. Hakuna kitu kama hicho maeneo mengine yoyote. Tunafanya *investment* ili Dodoma yetu iweze kuwa katika mazingira hayo mazuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine, watu wanasema *economic justification*; na ndugu yangu hapa Mheshimiwa Bobali alizungumza. Hili linaelezeka. Naomba niwaambie jambo moja, watu tunasahau kuna sayansi ya kimaumbile. Ndiyo maana hata Mungu mara nyingi akituelekeza jambo, anatuambia jambo hili lina manufaa sana kwa watu wenyewe kutafakari. Sayansi ya maumbile inatuelekeza, jambo lolote linafanikiwa na linakuwa zuri sana endapo linaanza katikati. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukiliangalia yai ambalo kuku anataga, nenda ndani utaangalia utaona *nuclear*. Hata ukiangalia mboni ya jicho lako ambalo linakupa uwezo kuona ile *lens* haiwezi ikakaa pembezoni, hiyo ni sayansi ya kimaumbile, Mungu ameumba hivyo. Hata wewe mwanadamu, siku moja chukua *tape measure* jipime, katikati hapo utaona kumbe ndiyo kuna masuala ya utaratibu wa kibinadamu. Kwa hiyo, habari zozote za kufanya mambo

yabadilike kwa kasi ni sayansi ya maumbile. Naomba niwaaambie, inawezekana wanadamu hatujatafakari hilo kwa kina. Naombeni mkafanye hiyo *research* ya sayansi ya kimaumbile. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo linakupa nini? Maana yake linakujuza kwamba kumbe Dodoma kukiwa ndiyo Makao Makuu yetu ambayo tumeelekeza, kutasaidia uchumi chechefu katika maeneo mbalimbali. Leo hii utakuja kuona Miji kama Iringa, Tabora, Singida na mingine, watu kijiografia wataweza kutanuka katika ile *multiplication* ya uchumi. Ndiyo maana nawaambia ni sayansi ya kimaumbile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa dada yangu ananiwekea maji, nikidondosha tone hapa utakuta maji yanaanza kububujika yanakwenda pembezoni. Maana yake ni kwamba kitu chochote ukikiweka *strategically* katikati zaidi jambo hilo linapata manufaa mazuri zaidi. Kwa hiyo, naomba niwaaambie, nendeni mkatafakari; ukifika usiku tandika kitanda fikiria sayansi ya kimaumbile, utakuja kuona hatujafanya makosa katika jambo hili la kuhakikisha kwamba Dodoma kunakuwa Makao Makuu yetu ya nchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa zilikuwepo hoja mbalimbali lakini jambo kubwa ni kwamba leo hii tumwangalie mkazi wa Kakonko karibu na Burundi. Wakati mwingine anapotaka kupata huduma yoyote kwenda Dar es Salaam akili imwambie anapokuja Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fikiria mkazi wa *Mbamba Baykule Nyasa* kwa dada yangu, Mheshimiwa *Eng. Manyanya*, mwambie ama kwenda Dar es Salaam au kuja Dodoma. Mfikirie mkazi wa Tarime umbali apime kutoka Tarime kwenda Dar es Salaam na kutoka Tarime kuja Dodoma. Hii ndiyo maana nawaambia ni sayansi ya kimaumbile. Tukifanya hivi tutaitendea haki nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie kwamba jambo hili lilikuwa na tafakari ya muda mrefu isipokuwa ninyi Wabunge wa Bunge hili na Mheshimiwa Rais. Ilani ilielezea, sasa tunaenda kufanya maamuzi ya kisheria siyo ya kibabaishaji. Sasa tunatengeneza Sheria ya Makao Mkuu ya nchi yetu, Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili niseme kwamba nimefurahi sana kwa sababu nami naingia mionganoni mwa watu walioweka historia kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wanavyoweka historia humu. Hawa Waheshimiwa Wabunge watatajwa, *Hansard* zitasema Bunge la Kumi na Moja, hawa watu ndio pekee waliofanya maamuzi kuliko watu wengine wote kutengeneza sheria. Ni wangapi walipita lakini walishindwa kujadili sheria kama hii? Ni ninyi peke yenu, *unique!* Ninyi ni watu maalum sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapa ikiwezekana kila mmoja tupige picha pale nje kwa kumbukumbu. Maana mmetengeneza historia ambayo haijawahi kuwekwa na mtu mwingine yeoyote, wengi wameshindwa. Rais ameamua, Waheshimiwa Wabunge tumefanya, tunajadili toka asubuhi kwa ajili ya kuhakikisha sasa tunapata Makao Makuu kwa mujibu wa sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana. Hoja nydingi zimeshasemwa kuhusu suala zima la upimaji, uchumi na usalama. Ukiangalia usalama wetu Dodoma ikiwa Makao Makuu huwezi ukataka tena *justification* yoyote, iko wazi kabisa kwamba nchi yetu tunapoweka Makao Makuu hapa Dodoma hali ya kiusalama ikoje?

Kwa hiyo, hivyo viashiria vyote vilitusababisha kama nchi kwa pamoja kuamua, na leo hii sasa tunazungumza suala la kisheria kusema kwamba Dodoma tuiweke kwa mujibu wa sheria kuwa Makao Makuu yetu ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine ni ya kiushauri. Niseme kwamba sisi kama Serikali tumeyachukua na hasa suala zima la uwekezaji mkubwa ili mji wetu uendelee kuwa *unique* wengine waweze kuja Tanzania kujifunza zaidi. Haya kweli yatatokea, kwa sababu tumeshaanza maandalizi yake na yanaenda vizuri. Hata mpango wa bajeti mwaka huu, nenda kasome kitabu changu kile cha Ofisi ya Rais TAMISEMI kuhusu Dodoma, utaona mambo yote ya uwekezaji kwa ajili ya Dodoma kwamba sasa litakuwa jiji zuri la kisasa na Watanzania tutajivunia na watu wengine watakuja kujifunza kupitia Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi kama nilivyosema yameshajadiliwa, yameshachangiwa. Sasa kwa ufupi zaidi naomba niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwa umoja wetu waridhie kwamba Muswada huu uweze kupita kuwa Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa muktadha wa kwamba tujenge nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(*Makofii*)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imeungwa mkono na Bunge Zima. Tunashukuru. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Serikali Kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi wa Mwaka 2018 (*The Dodoma Capital City (Declaration) Bill, 2018*)

Ibara ya 1

Ibara ya 2

Ibara ya 3

Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja, taarifa.

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imepitilia Muswada wa Sheria ya Kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi (*The Dodoma Capital City (Declaration Act, 2018)*, ibara kwa ibara na kuukubali bila mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja illiamuliwa na Kuafikiwa)*

NAIBU SPIKA: Walioafiki nafikiri wameshinda. Kwa hiyo tunaendelea, Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (*A Bill for an Act to Declare Dodoma City to be the Capital City of the United Republic of Tanzania*).

(Kusomwa Mara ya Tatu)

(Muswada wa Sheria ya Kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi wa Mwaka 2018 (*The Dodoma Capital City Declaration, Bill 2018*) Ulipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hiyo ndiyo hatua muhimu katika utungaji wa sheria kuhusiana na Muswada huu. Naelewa katika kuchangia kulikuwa na mkanganyiko kidogo tu.

Waheshimiwa Wabunge, mllichokifanya ni hivi, Muswada huu ulikuwa unapendekeza tu, hatua ya kwanza ni kupata tamko la Mji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kisheria kuititia sheria hii au Muswada huu kama ulivyokuja. Ukipitishwa na bunge hiyo ya kutamka, sheria itamke, sasa ndiyo hatua ya pili kwamba Jiji la Dodoma ndiyo linatamkwa kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hii.

Yanayofuata sasa ili kuwezesha sura ya Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ni Dodoma yafanywe na sheria nyingine ambazo yawezekana Bunge lilitatunga au lilitatunga sheria nyingine. Hiyo kazi mliyoifanya leo ina maana hiyo.

Kwa hiyo, nawashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na timu yako. Pia kuititia kwako, namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania kuliwezesha hili. Hayawi hayawi, yamekuwa.
(Makofî)

Vile vile Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu naye amelisukuma sana jambo hili o mpaka wengine mwisho mkawa mnasema anafanya hivyo kwa sababu anatokea eneo hili. Anatokea eneo hili ndiyo, lakini hii ndiyo sehemu ya Tanzania ambayo tuliamua ndipo yawe Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano. *(Makofî)*

Kwa hiyo, ndugu zangu, leo ninyi ni sehemu ya historia ya nchi kwa suala hili kuititia rafiki yangu, Mheshimiwa Jafo, ni historia kubwa. Mnaweza mkaiona leo ni kitu kidogo, lakini ni kitu kizuri sana.

Nawashukuru sana kwa ushirikiano wenu mliotoa wakati naongoza kikao hiki, lakini yamekwenda vizuri. *(Makofî)*

Kwa hiyo sina matangazo ya ziada, nitamke tu kwamba shughuli za leo tumemaliza. Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho, Siku ya Jumatano, saa tatu asubuhi.

(Saa 1.25 Usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 5 Septemba, 2018, Saa Tatu Asubuhi)